**6 MEI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA TATU**

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 6 Mei, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

Mwenyekiti *(Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: -**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Maswali; tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu. Nilimwita Mheshimiwa Emmanuel John Khambay, Mbunge wa Babati Mjini, sasa aulize swali lake.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Ninaomba marekebisho kidogo kwenye swali langu isomeke kwa kumbukumbu zaidi kwenye *Hansard,* Kijiji, iwe ni Kijiji cha Mamire badala ya Manire.

Na. 253

**Ujenzi wa Barabara kutoka Kona ya Mrara – Lango la Hifadhi ya Tarangire**

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Barabara kilometa 24 kutoka Kona ya Mrara hadi Lango la Hifadhi ya Tarangire kwa upande wa Kijiji cha Mamire kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa niaba ya Waziri Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel John Khambay, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa barabara ya kutoka kona ya Mrara hadi Lango la hifadhi Tarangire kwa upande wa Kijiji cha Mamire yenye urefu wa kilometa 24 kwa kiwango cha lami ambayo itachochea

maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa wananchi wanaopitiwa na barabara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Serikali imeanza uboreshaji wa barabara hii yenye urefu wa kilometa 24 kwa kufanya usanifu wa kilometa 0.8 na kujenga kwa tabaka la lami pamoja na ujenzi wa daraja la Mrara kwa gharama ya shilingi milioni 944.88 ambapo mkandarasi amepatikana ili kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kwa tabaka la lami pamoja na ujenzi na matengenezo ya Barabara za Jimbo la Babati Mjini kwa kutenga bajeti kwa awamu, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khambay, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Nina maswali mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kutambua umuhimu wa machinjio iliyopo ndani ya Halmashauri ya Mji wa Babati, kuna kipande ambacho kinahitaji lami, kipande cha kutoka *Junction* ya kuelekea Ikulu mpaka Machinjioni na kwenye Machinjio kuelekea kwenye *Junction* ya Barabara ya Babati - Arusha. Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha kipande hicho cha barabara kwa kiwango cha lami kwa manufaa ya wananchi wa Jimbo la Babati Mjini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, je, ni lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Hangoni mpaka *Junction* ya kuelekea Ikulu inayopitia Kwere kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Emmanuel

John Khambay, Mbunge wa Jimbo la Babati, amekuwa mfuatiliaji wa mara kwa mara kuhusiana na miundombinu ya barabara katika Jimbo la Babati Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeweka mpango mkakati kwenye bajeti zake. Kwanza kuna bajeti za kawaida za *TARURA* katika Mji wa Babati, na pili, tuna Mradi wa *TACTIC* ambao pia itakwenda kuboresha barabara za lami na kujenga miundombinu mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu barabara ambayo ameisema Mheshimiwa Mbunge, ya *Junction* kwenda Ikulu, *Junction* kwenda Babati. Nimhakikishie tu kwamba, Serikali kwa ujumla wake tumeainisha maeneo yote muhimu ambayo yanahitaji huduma za kijamii na maeneo kama ya kimasoko, stendi, vituo vya huduma, na shule. Maeneo haya yote yanapewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mipango yetu ya bajeti tutahakikisha tunatenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara hizo kwa kiwango cha lami au changarawe kwa kadiri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nimhakikishie tu kwamba hata hiyo barabara nyingine ambayo ameitaja tutaendelea kuitengea bajeti kwa awamu kuhakikisha kwamba Wananchi wa Jimbo la Babati Mjini wanapata barabara bora kwa shughuli za kiuchumi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Barabara ya kutokea Tabata - Mwananchi kuelekea Savana – Mawezi, ni barabara ya kimkakati na Serikali imekuwa ikiahidi mara kwa mara kuijenga, lakini hivi hapa ninapoongea hiyo barabara haipitiki na wiki mbili zilizopita tumepoteza mtoto wa Darasa la Saba kutokana na maji kujaa kwenye ile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kwa Serikali, ni nini maelekezo ya Serikali ya dharura ya kuweza kusaidia barabara ile iweze kupitika kwa kipindi hiki cha mvua wakati tunasubiri sasa utekelezaji wa ujenzi wa hiyo barabara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ziko barabara ambazo zimeathiriwa na mvua nyingi ambazo zinaendelea kunyesha hapa nchini na katika Mkoa wa Dar es Salaam, na bado mvua zinaendelea kunyesha. Kwa hiyo, tunafahamu kwamba barabara hii ya Tabata - Mwananchi - Mawezi ni moja ya barabara ambayo imeharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kwanza, kuwapa pole wananchi wa eneo hilo kwa kumpoteza mtoto, na nitumie nafasi hii kutoa wito kwa walezi, wazazi na wananchi kwa ujumla kujaribu kuwa-*guide* vizuri watoto wetu katika kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha. Madimbwi ya maji yamekuwa mengi, tujaribu kuwa-*guide* na kuwasimamia kwa karibu ili kuondoa madhara ya aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tumeshapokea barabara hii ya Tabata – Mwananchi – Mawezi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, *TARURA* na tumeshakubaliana na Meneja wa *TARURA*, Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na Wilaya ya Ilala kwamba, mapema iwezekanavyo baada ya mvua kukatika, ijengwe barabara ile ifanyiwe matengenezo iweze kupitika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tumekubaliana kwamba maeneo yote ambayo yanaweza kurekebishwa kwa dharura ili kuwezesha wananchi kupita, yaweze kufanyiwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninawasisitiza Meneja wa *TARURA* - Ilala na Dar es Salaam, wafike eneo hilo waone

kinachoweza kufanyika kwa dharura ili kuwezesha wananchi kuendelea kupita kwa usalama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona, Mheshimiwa Mashimba Ndaki.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni takribani mwaka sasa mkandarasi anayejenga kipande cha barabara kilometa mbili kutoka katikati ya Mji wa Malampaka kwenda Kituo cha Afya cha Malampaka apewe kazi, lakini ameondoka kwenye *site* kwa sababu hajalipwa fedha zake. Ni lini Serikali itamlipa mkandarasi huyu ili aweze kuendelea na ujenzi kwa kiwango wa lami katika kipande hicho? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mbunge wa Jimbo la Maswa Mashariki kwamba, tunafahamu kuna mkandarasi ambaye alipewa kujenga barabara katika eneo la Malampaka kuelekea Kituo cha Afya cha Malampaka; na tunafahamu kwamba kutokana na changamoto za kiutendaji, na pia za kifedha, alisimama kwa muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na Wananchi wa Maswa Mashariki, kwamba tayari tumeshapokea andiko na maombi kutoka Halmashauri ya Maswa kutoka kwa Meneja wa *TARURA* na tayari Serikali iko kwenye taratibu zetu za mwisho za kuhakikisha kwamba tunapata fedha hiyo na kumlipa mkandarasi ili arejee, aweze kukamilisha ujenzi wa barabara hiyo. Kwa hiyo, barabara hiyo itakamilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itafanya kazi hiyo mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuna wachangiaji wengi sana leo, na wote mnajua, hatukumaliza jana. Kwa hiyo, maswali ya nyongeza tutayapunguza sana. Tuendelee na swali linalofuata. Nimwite sasa Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, aulize swali lake.

Na. 254

**Utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC*-Bunda Mjini**

**MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza kutekeleza Mradi wa *TACTIC* unaopaswa kujengwa Jimbo la Bunda Mjini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Bunda ni miongoni mwa Miji 45 inayotekeleza Mradi wa *TACTIC* nchini. Mji wa Bunda upo kundi la Tatu la utekelezaji lenye Miji 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *TACTIC* umekamilisha usanifu wa miradi ya kundi hili la tatu ikiwemo Mji wa Bunda wenye Barabara nane zitakazojengwa kwa lami. Jumla ya kilometa 5.21 pamoja na Ujenzi wa Stendi kuu ya mabasi, na Soko kuu katika mji wa Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha usanifu wa miradi hii, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaendelea na taratibu za kifedha ili kuanza utekelezaji wa miradi katika kundi hili ukiwemo mradi wa Mjini wa Bunda, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwanza, niipongeze Serikali kwa hii miradi ya *TACTIC* kwani inabadilisha miji kabisa na kwenda kuchechua uchumi kwenye maeneo husika. Sasa ningependa kujibiwa maswali yangu mawili ya nyongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali hili nimeuliza zaidi ya miaka minne na nilishaambiwa kila kitu kimekamilika, bado ujenzi kuanza na Bunge hili hili nimeliuliza nikaambiwa kila kitu kimekamilika ujenzi unaanza *tire three*. Wananchi wa Bunda wanataka kujua lini? Kwa sababu hili jibu nimeshajibiwa sana, lini mradi unaanza? Ndiyo fahari yao, na wanausubiri kwa hamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mwanzo kwenye huu mradi ilikuwa machinjio ya kisasa; lilikuwepo na dampo lijengwe, na hizi kilometa za lami hapa zimepungua. Mwanzo zilikuwa kilometa 21. Nini kimesababisha hivi vingine vyote vimeondolewa kwenye mradi, imebaki stendi, soko pamoja na barabara kilometa tano badala ya kilometa 21?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Bunda Mjini, dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya angependa kuona leo hii barabara yote kilometa 25 imejengwa kwenye Jimbo la Bunda, na hiyo ndiyo dhamira ya Serikali yetu, na ndiyo dhamira ya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ndiyo maana aliuleta mradi huu mahususi kwa miji 45 ili kuchachua Uchumi, na kuwezesha miundombinu yetu kuwa bora zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumetekeleza awamu ya kwanza, awamu ya pili, tuko hatua mbalimbali, lakini awamu ya tatu, tumeshafanya usanifu na tunaendelea na utaratibu wa kifedha ili kuanza utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni kweli Mheshimiwa Mbunge ameuliza kwa muda mrefu, na kwa sababu ninafahamu ni dhamira ya kutaka kazi hii ifanyike mapema, Serikali iliweka mpango tangu mwanzo kuanza awamu ya kwanza, baada ya muda fulani tumekwenda awamu ya pili, baada ya muda fulani tumekuja awamu ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hatukupanga kuanza miradi hii *tire three* kwa pamoja. Vinginevyo tusingekuwa na sababu ya kuweka makundi matatu kama tungeanza pamoja. Kwa hiyo, makundi matatu yaliwekwa kwa sababu tunakwenda kwa awamu na kundi hili la tatu sasa la miji takribani 18 ndiyo tuko hatua za mwisho za kuanza utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini kwamba Serikali itakwenda kutekeleza kama ilivyoweka mpango wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, miradi hii ilifanyiwa usanifu lakini kutokana na upatikanaji wa fedha tumeendelea ku-*review* upana *(scope)* wa hii miradi kadiri muda unavyozidi kwenda ili kuwa na miradi ambayo inatekelezwa kutokana na upatikanaji wa fedha iliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haimaanishi kwamba miradi hiyo mingine haitatekelezwa, tunatekeleza kwanza miradi hii kwa awamu hii kutokana na uwezo wa kifedha uliopo, lakini baada ya hapo tutaendelea Serikali ni endelevu na bajeti ni endelevu, tutandelea kutekeleza miradi hiyo. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Bulaya kwamba hata hayo maeneo mengine Serikali itaendelea kuyatekeleza kwa awamu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakuona, Mheshimiwa Omary Msigwa.

**MHE. OMARY M. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Wino - Matumbi iliyopo katika Jimbo langu la Madaba ni barabara muhimu kwa uwekezaji, lakini imekuwa

ikijifunga kila wakati. Je, ni lini sasa Serikali itakwenda kuijenga kwa kiwango cha changarawe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Msigwa amefuatilia kwa karibu sana kuhusiana na miundombinu ya barabara katika Jimbo la Madaba, nami nimhakikishie, yeye mwenyewe ameleta taarifa za uhitaji wa barabara na Meneja wake wa *TARURA,* ameleta na Ofisi ya Waziri Mkuu, tayari tumeanza utaratibu wa kutafuta fedha kwenda kutekeleza barabara hizo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakuona Mheshimiwa Japhet Hasunga.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni lini Mradi wa *TACTIC* unaohusu barabara, soko na stendi ya mkoa utaanza kutekelezwa kwenye Mji wa Vwawa, ambao tumekuwa tunaahidiwa karibu zaidi ya miaka minne? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Vwawa ni moja ya miji 45 kwenye Mradi wa *TACTIC* na uko awamu ya tatu yenye miji 18, na nimhakikishie tu kwamba, sasa tunaelekea kuanza utekelezaji wa awamu ya tatu ya miji 18, ikiwemo Mji wa Vwawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, nimwite sasa Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Bagamoyo, aulize swali lake.

Na. 255

**Mradi wa *TACTIC* Jimbo la Bagamoyo**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza utekelezaji wa Mradi wa *TACTIC* katika Jimbo la Bagamoyo baada ya usanifu kukamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Jimbo la Bagamoyo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Mji wa Bagamoyo ni miongoni mwa miji 45 inayotekeleza Mradi wa *TACTIC* nchini wenye barabara zenye urefu wa jumla ya Kilometa 4.5 pamoja na ujenzi wa barabara hizo kwa kiwango cha lami. Mradi huu pia utahusisha ujenzi wa stendi kuu ya mabasi Bagamoyo katika Kata ya Nia Njema, eneo la Kichemchem.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kukamilisha usanifu wa miradi hii, Serikali kwa kushirikiana na Benki ya Dunia inaendelea na taratibu za kifedha kabla ya kuanza utekelezaji wa Miradi katika kundi hili ukiwemo Mji wa Bagamoyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwanza, niishukuru Serikali kwa kuifanya Bagomoyo iwe sehemu ya miji 45, na hata jibu la swali hili kuitamka Bagamoyo kama Halmashauri ya Mji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, wananchi wa Kata za Dunda, Magomeni na Nia Njema walishajiandaa, wakabomoa nyumba zao na maeneo yao ya biashara kwa barabara zinazotaka kujengwa; hata hivyo, hali ni mbaya barabara hazipitiki ikiwemo pia stendi yetu. Ninatambua jibu limesema kuna stendi itajengwa; hii ni ya mkoa, lakini tuna hali mbaya kwenye stendi ya Bagamoyo, kwani iliyopo sasa inajaa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni kuna haja ya kuja na mpango wa dharura wakati tukisubiria mradi huu mkubwa wa *TACTIC?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa tarehe 29 mwezi wa nne nilifanya ziara katika Jimbo la Bagamoyo kwenye maeneo ambayo yameathirika kwa kiwango kikubwa na mvua; kwenye Kata ya Mapinga maeneo ya Kwakibosha, Kimele, Changoyela, Minazi minane, pia maji yameingia kwenye Kata ya Nianjema, je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya *TARURA* kuja na mpango wa dharura kwa yale maeneo ambayo hayapitiki kabisa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua Serikali inajipanga kuzijenga baada ya mvua kwisha, lakini sasa hivi wananchi wamezungukwa na maji na barabara hazipitiki na wawekezaji wanaojenga viwanda ikiwemo Kiwanda cha *Oasis* pale Mapinga wanashindwa kufika katika maeneo yao. Je, Serikali iko tayari?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana dada yangu Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Bagamoyo. Ni kweli kwamba ziko barabara ambazo zimeathiriwa na maji kutokana na mvua nyingi ambazo zimeendelea kunyesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza tulishatoa maelekezo, na maelekezo haya yanaendelea kutekelezwa na Mameneja wa *TARURA* ngazi ya wilaya na mkoa kote nchini kwamba, maeneo yale ambayo yameathiriwa na mvua na barabara hazipitiki kabisa. Ikiwa kuna uwezekano kitaalamu wa kufanya matengenezo na kuwawezesha wananchi kuendelea angalau kupita kwa kipindi hiki wakati tunasubiri hali ya hewa ikae vizuri na kujenga kwa hali ya kudumu, wafanye hivyo mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kipindi cha miezi mitatu minne iliyopita imepeleka zaidi ya shilingi bilioni 21.4 kwenye halmashauri zetu, kwenye majimbo yetu, kwa ajili ya kurekebisha barabara hizi kwa dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii nimwelekeze pia Meneja wa *TARURA* Bagamoyo na Mkoa wa Pwani kuendelea kufuatilia kwa karibu maeneo yote yaliyotajwa na Mheshimiwa Mbunge, ambayo ni Sarunda, Magomeni, Nianjema, Mapinga na maeneo yote ambayo yanaweza kurekebishwa kwa dharura yarekebishwe. Yale ambayo lazima tusubiri hali ya hewa ikae vizuri, kwa sababu hatuwezi kujenga barabara juu ya maji, basi tuwaombe kwamba taratibu za maandalizi yafanyike kwa ajili ya ujenzi huo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Cornel Magembe.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Serikali imekuwa ikifanya usanifu katika Mji wa Chato katika ujenzi wa soko kuu pale mjini Chato, pamoja na barabara ya kilometa nne za Mji wa Chato ikiwemo soko la samaki pale Kasenda, Kata ya Muganza. Usanifu ule umechukua muda mrefu na kila mwaka tunakuwa tunaahidiwa kwamba mradi ule wa *TACTIC* unakwenda kuanza kutekelezwa. Sasa ninaomba kupata majibu sahihi, ni lini sasa utekelezaji wa miradi hii mitatu unakwenda kuanza? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Magembe, Mbunge wa Jimbo la Chato Kaskazini, kwamba ni kweli Mji wa Chato ni miongoni mwa miji 45 iliyoko kwenye Mradi wa *TACTIC*, na mji huu uko kwenye *TACTIC* Awamu ya Tatu, hii ambayo sasa tumekamilisha usanifu wake. Tunaelekea sasa kuanza taratibu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia kwa ajili ya kuanza ujenzi wa

miradi hii. Tunafahamu kuna soko, kuna barabara na miundombinu mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie tu kwamba Serikali iko kwenye hatua nzuri ya kuanza utekelezaji wa mradi huu na wananchi wa Chato na Mheshimiwa Mbunge ninawaomba wawe na amani, Serikali itakwenda kutekeleza mradi huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Ninamwita sasa Mheshimiwa Mdowe Haji Kombo, Mbunge wa Nungwi, aulize swali lake.

Na. 256

**Kujenga Ukuta katika Fukwe za Bahari – Nungwi Kiungani**

**MHE. MDOWE HAJI KOMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga ukuta katika Fukwe za Bahari ya Nungwi Kiungani ili kuzuia bahari kuingia katika makazi ya watu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kwagilwa Reuben kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mdowe Haji Kombo, Mbunge wa Nungwi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na athari

za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo mmonyoko wa fukwe unaosababisha bahari kuingia katika makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza hili, Serikali imefanikiwa kupata ufadhili kupitia Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi *(Green Climate Fund)* ambapo jumla ya dola za Marekani 500,000 sawa na takribani shilingi bilioni 1.3 za Kitanzania zimetolewa na mfuko husika kwa ajili ya kutekeleza mradi katika mwaka wa fedha 2025/2026 na 2026/2027 wa kuimarisha utayari wa Kisiwa cha Zanzibar kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Mradi huu utaanza mara baada ya tathmini ya athari hizo kukamilika. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. MDOWE HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Nungwi wanataka kujua, ni lini tathmini hiyo itakamilika? Kwa sababu kuanzia mwaka wa fedha wa 2023/2024 majibu ya Serikali yalikuja kuhusu tathmini. Ninanukuu; Waziri wa wakati huo alijibu: "Kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar imetenga fedha jumla ya shilingi milioni 650..."

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kombo, utakuwa kama unachangia, uliza tu swali.

**MHE. MDOWE HAJI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa tathmini hiyo itakamilika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kadiri siku zinavyokwenda, hali inazidi kuwa mbaya. Sasa tunataka kujua sisi kama wananchi wa Nungwi, ni zipi hatua za dharura ambazo Serikali zitaichukua kukabiliana na hali ile pale? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, ameshafika ofisini kwetu takribani mara

tatu au mara nne kwa ajili ya kufuatilia jambo hili. Hata jana alikuwepo ofisini kwetu. Tayari imeshafanyika tathmini ya awali kwa Zanzibar yote, na tumebaini maeneo karibia 148 ambayo yameathirika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hayo maeneo 148, maeneo 123 yako Pemba na maeneo 25 yako Unguja. Serikali baada ya kufanya tathmini hiyo imeanza kutekeleza mradi wa mabadiliko ya tabianchi kukabiliana nayo katika ngazi ya jamii. Tayari tumeshaanza kwa awali na halmashauri 11 kule Zanzibar na halmashauri 54 Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua inayofuata baada ya tathmini hii kukamilika, tunakwenda kufanya tathmini ya kubaini gharama kwa kila eneo ambalo limeathirika yakiwemo maeneo anayotokea Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili, ametaka kujua ni hatua za dharura ambazo Serikali inachukua. Kwenye eneo la Mheshimiwa Mbunge Wilaya ya Kati tumebaini maeneo matatu ambayo yameathirika zaidi kuliko maeneo mengine. Maeneo hayo ni Wadi ya Cheju, Wadi ya Chakwa, pamoja na eneo la Wadi ya Ubago.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti hii tunayokwenda kuitekeleza kwenye bajeti ambayo Bunge hili limetupitishia, tumetenga kwa nchi nzima kwa maana ya pande zote mbili kupitia Fungu 31, zaidi ya shilingi bilioni 31 ambazo zitatekeleza miradi hii ya mabadiliko ya tabianchi kwa awamu na awamu itakapofika tutajielekeza kwenye maeneo hayo ya Cheju, Chakwa na Ubago. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Selemani Kakoso, swali fupi.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya tabianchi yamelifanya Ziwa Tanganyika kuwa na mwelekeo tofauti uliosababisha wananchi wa Kata ya Ikola, Isengule, na Karema kukosa makazi baada ya ziwa hilo kuvamia

makazi ya wananchi. Je, ni lini Serikali itaenda kujenga tuta kwenye maeneo ya kata hizo tatu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu kwenye swali la msingi, Serikali kupitia Mradi huu wa Mabadiliko ya Tabianchi tunatekeleza mradi huu kwa awamu kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali itakapopata fedha, wananchi hao tutakwenda kuwahudumia kwa kujenga kuta kwenye eneo hilo kama ambavyo tumefanya kule Mikindani na kule Sepwese Pemba.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi kama huu wa tabianchi ulifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, na ulikuja kwenye halmashauri kwenye majimbo mawili ya Bunda na Mwibara. Umetekelezeka Jimbo la Mwibara, ni lini sasa utatekelezeka Jimbo la Bunda? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu kwenye swali la msingi, kwa upande wa Tanzania Bara, mradi huu tunautekeleza kwenye halmashauri 54 na tunautekeleza kwa awamu kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha, na mradi huu tutautekeleza kwa mwaka huu wa fedha unaoisha na mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maeneo yote ambayo tumeyaainisha ikiwemo maeneo ya jimbo lake, tutakwenda kutekeleza mradi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Afya. Ninamwita sasa Mheshimiwa Fadhili Fabian Ngajilo, Mbunge wa Iringa Mjini, aulize swali lake.

Na. 257

**Huduma za Afya za Kibingwa Nyanda za Juu Kusini**

**MHE. FADHILI F. NGAJILO** aliuliza: -

Je, lini huduma za kibingwa za magonjwa kama moyo, kansa, mapafu, figo na ini zitatolewa katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali Kanda ya Mbeya na hospitali za rufaa za Mikoa ya Mbeya, Iringa, Njombe na Songwe zinatoa huduma za ubingwa katika fani za magonjwa mbalimbali ikiwemo moyo, saratani, mapafu, figo na ini. Hospitali ya Kanda ya Mbeya inatoa huduma za ubingwa bobezi katika fani za upasuaji wa moyo, upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu, matibabu ya mfumo wa chakula na ini, huduma ya mfumo wa upumuaji pamoja na huduma ya upasuaji kwa watoto wachanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha utoaji wa huduma za saratani katika kanda hii, Serikali inatekeleza mradi wa ujenzi wa kituo cha huduma za saratani mkoani Mbeya ambacho kitakuwa sehemu ya Taasisi ya *Ocean Road*. Kukamilika kwa mradi huu kutawezesha wananchi kupata huduma za ubingwa za saratani katika kanda hii, hivyo kuwapunguzia gharama za kufuata huduma hizi katika Taasisi ya Saratani *Ocean Road* Jijini Dar es Salaam. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fadhili Ngajilo, swali la nyongeza.

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa

Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwekeza sana kwenye huduma za kibingwa katika nchi yetu. Sisi Kanda ya Nyanda za Juu Kusini tunanufaika sana na huduma hizi. Sisi Nyanda za Juu Kusini tunategemea sana hospitali ya kanda ile iliyopo pale Mbeya.

**MWENYEKITI:** Uliza maswali.

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Mweyekiti, huduma zetu za moyo na kansa bado zina changamoto. Upande wa kansa, tunaomba ule mtambo wa saratani wa kuchoma mionzi uweze kuletwa kwa haraka kwa sababu sasa hivi tunapata huduma tu za *chemo* kwa maana ya matibabu ya dawa.

Mheshimiwa Mweyekiti, swali la pili. Imekuwa ni gharama sana kwenye huduma hizi za kibingwa. Nini kauli ya Serikali kuhusu utaratibu wa "*Medical Exemption*", yaani utaratibu wa kupunguza gharama za huduma hizi za kibingwa kwa wananchi wetu hasa wananchi wangu wa Jimbo la Iringa Mjini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Fadhili kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwatetea Wananchi wa Jimbo la Iringa Mjini na wa Kanda ya Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza, ni kweli kabisa kwamba tunajenga sasa jengo la mionzi katika hospitali yetu ya Mbeya, na jengo hili linatarajiwa kukamilika ifikapo Desemba mwaka 2025. Jengo hili litagharimu takribani shilingi bilioni 11. Hivyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, lakini na wananchi wote wa Mkoa wa Mbeya kwamba mtambo huo tutakwenda kuufunga kwenye jengo hilo pindi utakapokamilika mwaka huu ili huduma hizi ziweze kuanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu gharama za matibabu kwa kutumia msamaha, kwanza kabisa, hapa nimpongeze Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye

ameendelea kulipa gharama za matibabu kwa wagonjwa ambao hawana uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bajeti ya mwaka 2025/2026 Serikali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 34 kuwahudumia wagonjwa wa msamaha. Hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, wagonjwa ambao hawana uwezo, wataendelea kuhudumiwa na Serikali kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo katika hospitali zetu, na wagonjwa hawa watapata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan tayari ameshaanzisha huduma ya Bima ya Afya kwa Wote, ambapo 14% ya Mfuko huu utakwenda kuwahudumia wagonjwa ambao wana magonjwa sugu ikiwemo magonjwa haya ya moyo, figo pamoja na saratani. Hivyo, niwaombe Watanzania wote, wale wenye uwezo wajiunge kwenye Mfuko wa Bima Afya kwa Wote na wasiyokuwa na uwezo Serikali itawalipia ili kuweza kupata huduma hizi kwa karibu zaidi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Damas Ndumbaro.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kuna hospitali maalumu ya rufaa katika Manispaa ya Songea iliyoko katika Kata ya Mwengemshindo. Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa kama *MRI* na kutoa huduma za kibingwa katika hospitali hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza niendelee kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Ndumbaro kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwapigania wananchi wa Songea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali hii ya Rufaa ya Songea inatoa huduma nane za kibingwa, na sote ni mashahidi kwamba Mheshimiwa Rais alipohutubia Bunge, ametuelekeza tuongeze

huduma za kibingwa. Hivyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mwongozo wetu wa 20 kwenda 30 hospitali zote za rufaa zitakwenda kutoa huduma za kibingwa 17.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo tunaendelea kujiandaa kwa kuendelea kununua vifaa, kuendelea kuwasomesha watumishi kupitia *Samia Scholarship Program,* lakini na kujenga miundombinu ili kuweza kutekeleza huduma hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge anazihitaji katika jimbo lake. Ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Tinnar Chenge.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kwa kuwa Hospitali ya Mkoa wa Simiyu ni hospitali ya rufaa, na kwa kuwa hospitali hii haina daktari bingwa wa mifupa, je, ni lini Serikali itapeleka daktari bingwa wa mifupa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Mama yangu, Mheshimiwa Chenge kwa kazi nzuri anayoifanya ya kuwapigania wananchi wa Mkoa wa Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Rufaa ya Simiyu ni moja ya hospitali inayotoa huduma za kibingwa, na hospitali hii inatoa huduma za kibingwa sita. Ninaomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeendelea kutoa ajira za watumishi ili kukabiliana na changamoto za watumishi na hasa watumishi bingwa. Hivyo pindi watakapopatikana na kupata kibali cha ajira, basi hospitali hii ya Simiyu itapelekewa mtaalamu huyu wa mifupa ili wananchi waweze kupata huduma hizi za kibingwa za mifupa karibu na mkoa wao. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Ninamwita sasa

Mheshimiwa Baraka Ulimboka Mwamengo, Mbunge wa Kyela, aulize swali lake.

Na. 258

**Ujenzi wa Barabara ya Ipyana – Kasumulu – Ileje kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO** aliuliza: -

Je, lini Barabara ya Ipyana – Kasumulu – Ileje itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa niaba yake, Naibu Waziri, Mheshimiwa *Eng.*Geodfrey Kasekenya.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Baraka Ulimboka Mwamengo, Mbunge wa Kyela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Ipyana – Kasumulu – Ngana – Ndembo – Ileje eneo la Isongole lenye urefu wa kilometa 114.3 ambapo kwa sasa kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii imefikia 96%. Aidha, Serikali imeanza ujenzi wa barabara hii sehemu ya *Isongole II* – Ndembo pamoja na barabara ya kuingia Ndembo – Isoko yenye urefu wa kilometa 52 ambapo ujenzi umefikia 10.75%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sehemu ya Ipyana – Kasumulu – Ngana hadi Ndembo kazi ya kufanya uthamini wa nyumba na mali kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaoathiriwa na mradi huo inategemea kuanza hivi karibuni.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Baraka Mwamengo, swali la nyongeza.

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, eneo lile la Barabara hiyo ya Ipyana – Kasumulu kwa kipindi hiki cha mvua imeathirika sana na maeneo makubwa ambayo yanakwamisha magari kupita ni eneo hilo, hasa kipande cha eneo la Igoma, je, Serikali itakuwa tayari kupeleka fedha za dharura, ili kuendelea kuikarabati hiyo barabara wakati tunasubiri huo mradi mkubwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa, Serikali tayari imesema kuwa, imeanza kipande, *section* ile ya upande wa Ileje, je, awamu ya pili itakuwa tayari sasa kuanza kipande cha Ipyana – Kasumulu – Ngana, ili wananchi waone Serikali inajali, kama ilivyoandikwa kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi? Ninashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, hii ni barabara ya changarawe, ambayo katika kipindi cha mvua na hasa ule Ukanda wa Kyela ambao una mvua nyingi, huwa barabara nyingi zinakuwa zimeharibika. Huu ni mwezi wa Tano, kwa hiyo, ninamwelekeza Meneja wa Mkoa wa Mbeya afike eneo la barabara kuangalia kama sasa tunaweza tukaanza utengenezaji wa kawaida, na kama sivyo, basi aweze kuhakikisha kwamba, mkandarasi ambaye atatengeneza barabara hiyo katika matengenezo ya kawaida, anatengeneza na kurekebisha yale maeneo ambayo sasa yanafanya hiyo barabara isipitike kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la pili, barabara hii inaunganisha Mkoa wa Songwe na Mkoa wa Mbeya, kwa maana ya Wilaya ya Ileje na Wilaya ya Kyela. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ombi la kuanza upande mwingine Serikali itasikiliza, lakini ninafahamu Mheshimiwa Mbunge pia ni mtaalamu wa barabara. Kuna vigezo kadhaa ambavyo vinaangaliwa, hasa kulingana na ushauri wa mhandisi mshauri, barabara ianze wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo barabara zinaanza katikati, nyingine zinaanza mwisho. Kwa hiyo, tutaangalia, kama kutakuwa na vigezo hivyo vya kuanza upande huo wa Ipyana, haitashindikana kufanya hivyo, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakuona Mheshimiwa Anne Kilango Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwa kuwa, Mheshimiwa Waziri alikuja Same tukapita Barabara ya Mwembe – Miamba – Ndungu, kwa siku nzima tulipitia barabara hii, sasa ninaomba kuuliza swali, je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nilipita hiyo barabara na ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kwamba kwanza ni kweli hiyo barabara ilikuwa haijafanyiwa usanifu. Maana yake ilikuwa haijafanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Ndiyo tupo kwenye hiyo kazi ya kufanya usanifu wa kina wa barabara hiyo, ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muda mrefu sasa Serikali imetuahidi ukarabati wa Barabara ya Moshi – Arusha pamoja na kulipa fidia na kujenga Daraja la Kikafu. Serikali ina mpango gani sasa kuanza kutekeleza ahadi hii ambayo imekuwa ya muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inatekelezwa kwa kutumia fedha ya Serikali ya Tanzania, lakini pia, ikisaidiana na wenzetu wa *JICA*. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, mazungumzo yote yamekamilika, na *no objection*

kwa maana ya kuwa na utayari wa kufanya hiyo kazi, imeshatolewa na wenzetu wa *JICA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tupo kwenye hatua za mwisho kabisa ikiwa ni kutangaza hiyo kazi, kulipa fidia kwa wale watakaoathirika, lakini pia, na kujenga hilo Daraja la Kikafu ambalo tunalihamisha lilipokuwa na kuliweka sehemu nyingine, hasa kutokana na ukweli kwamba, daraja lililopo linaleta changamoto kubwa sana ya ajali. Kwa hiyo, tupo kenye hatua za mwisho kabisa.

**MWENYEKITI:** Ninakuona Mheshimiwa Aysharose Mattembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa, barabara inayoanzia Singida Mjini hadi Ilongero, kibali cha kujenga kilometa kumi zinazoanzia Mtipa kwenda Makao Makuu ya Jimbo la Ilongero kimetoka. Ninapenda kujua ni lini sasa Serikali itampata mkandarasi kwa ajili ya kujenga kilometa hizo kumi? Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hiyo ilikuwa imetangazwa, na mkandarasi alikuwa amepatikana mmoja, ambaye baada ya majadiliano ilionekana kwamba bei yake iko juu sana na hivyo kulazimisha barabara hiyo kutangazwa upya ili iweze kuwa ndani ya bajeti ambayo tunategemea barabara zetu zinajengwa kwa kiwango hicho, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Bado tuko Wizara hiyo hiyo. Ninamwita sasa Mheshimiwa Silyvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, aulize swali lake.

Mheshimiwa Koka hayupo. Mheshimiwa Selemani Jafo, kwa niaba.

Na. 259

**Ujenzi wa Barabara ya *TAMCO* – Mapinga**

**MHE. DKT. SELEMANI S. JAFO K.n.y. MHE. SILYVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya *TAMCO* hadi Mapinga utakamilika kwa kiwango cha lami baada ya kusuasua kwa muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Barabara ya *TAMCO* – Mapinga unatekelezwa kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza inahusisha sehemu ya kuanzia *NIDA* hadi Pangani, kilometa 3.8, na awamu ya pili inahusisha sehemu ya Pangani hadi Mapinga, kilometa 14.62. Ujenzi wa barabara hii unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2027. Aidha, Serikali inaahidi kuipa kipaumbele barabara hii kama sehemu ya kupunguza msongamano kwenye Barabara Kuu ya Dar es Salaam kwenda Morogoro, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Jafo, kwa niaba.

**MHE. DKT. SULEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana, ninafahamu kandarasi pale inaendelea, lakini *speed* bado siyo ya kuridhisha. Je, nini mpango wa Serikali, kwa nia njema ile ile ya kumsukuma sasa mkandarasi ilimradi aweze kukamilisha ile kazi kwa lengo la kuwasaidia watu wa Bagamoyo, kwa dada yangu Mheshimiwa Subira na watu wa Kibaha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Barabara ile inatengeneza *ring road.* Ukitoka upande wa Bayamoyo, pale Baobao mpaka unafika Kibaha, na kutoka Kiluvya kuja Kisarawe pale, kilometa 22.9. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha kile

kipande cha kilometa 22.9 kutoka Kiluvya Madukani mpaka Mpuyani nacho kinaanza kazi mara moja? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba, hii barabara Serikali inaipa kipaumbele sana kwa sababu ni kweli itasaidia sana kupunguza msongamano kwenye Barabara Kuu ya Dar es Salaam na Morogoro. Tunaipa kipaumbele kuhakikisha kwamba, mkandarasi analipwa aweze kukamilisha hiyo barabara, ambayo tuna hakika itakuwa ni muhimu sana kwa kupunguza foleni. Kwa hiyo, kipaumbele ni kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba, kama tutaiunga hiyo barabara mpaka Kisarawe itakuwa inatengeneza *ring road,* ambapo watu wengine wanaweza wakapita huko. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari tumekamilisha usanifu wa hiyo barabara kutoka Kibaha hadi Kisarawe, kwa hiyo, tunachosubiri tu ni fedha tuweze kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza ujenzi kwa kiwango cha lami wa Barabara ya Ipogoro – Idete. Barabara hii imeishia Kibaoni. Ni lini sasa kilometa 16 za kutoka Kibaoni kwenda mpaka Dabaga itamaliziwa kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokea pongezi za Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge wa Kilolo, kwa niaba ya Serikali. Hasa niseme, hii ndiyo kazi nzuri ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kukamilisha hicho kipande hadi Dabaga, tutaendelea kwa sababu, tunafanya kwa awamu.

Kwa hiyo, baada ya kukamilisha awamu ya pili, ni kukamilisha hicho kipande, cha kilometa kama 66, ili barabara yote iweze kuwa ya kiwango cha lami tukizingatia kwamba, uzalishaji wa huko wa mbao na matunda ni mkubwa sana, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, bado tupo katika Wizara hiyo. Ninamwita sasa Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 260

**Ujenzi wa Barabara ya *Old Shinyanga* – Iselamagazi**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza:-

Je, lini Barabara ya kutoka *Old Shinyanga* hadi Iselamagazi, Makao Makuu ya Halmashauri ya Shinyanga *DC*, itajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya *Old Shinyanga* hadi Iselamagazi yenye urefu wa kilometa 25 ni sehemu ya Barabara ya Salawe – Solwa hadi *Old Shinyanga*, yenye urefu wa kilometa 80.1. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami imekamilika. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, upembuzi yakinifu umefanyika. Ni lini fedha zitapatikana?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Barabara ya *Old Shinyanga* kwenda Njia Panda ya Nyasamba – Mwanza imeanza

kujengwa kwa kiwango cha lami. Kuna sehemu imekamilika zaidi ya miaka minne na tayari imeanza kuharibika. Nini Kauli ya Serikali kwa Mkandarasi yule, ambaye anajenga hiyo barabara na tayari imeharibika kabla haijakamilika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara ni hatua. Hatua ya kwanza, tumekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina. Ukifanya hivyo, maana yake ni maandalizi ya kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, bajeti bado hatujaitoa, tusubiri bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kuisanifu tu barabara hii, maana yake ni kwamba Serikali ina mpango wa kuijenga kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili kwamba barabara imetengenezwa miaka miwili imeharibika, ninaomba hili tulichukue. Pia, ninamwelekeza Meneja wa Mkoa wa Shinyanga pamoja na *TANROADS* Makao Makuu waweze kwenda kuiangalia barabara hiyo waweze kutoa taarifa, tatizo ni nini, ili hatua stahiki, kama kuna uzembe umefanyika, basi tuweze kuchukua hizo hatua. ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chacha Wambura.

**MHE. CHACHA M. WAMBURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona na kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Katika Mji wa Geita tunayo Barabara inayotoka Geita mpaka Kahama, ambayo ni tegemezi kubwa sana katika uchumi wa Mji wa Geita. Mkandarasi amesaini mkataba tarehe 01 Mwezi wa 10 na mpaka sasa barabara ile imeshindwa kuanza kwa sababu tu yule mkandarasi hajalipwa *advance*. Sasa je, ni lini Serikali itamlipa *advance* yake ili aweze kuanza kutengeneza ile barabara?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Geita hadi Kahama imeanza kujengwa na Serikali kwa kiwango cha lami, na hasa kipande cha kutoka Kahama hadi Kapola. Barabara hii tunavyoongea, mkandarasi yupo, anaendelea kuijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara ilikuwa imegawanywa katika vipande viwili, kutoka Ilogi – Nyarugusu hadi Mtakuja – Geita, ambapo mkandarasi tayari amesaini na tunachosubiri ni kumpa *advance,* ili kuunga Mkoa wa Geita na Mkoa wa Shinyanga, kwa maana ya Miji ya Geita na Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua hilo ndiyo eneo ambalo kwa kweli, lina uzalishaji mkubwa, na pia, ndiyo madini mengi yako hapo. Kwa hiyo, Serikali, tunaamini katika bajeti inayokuja, hiyo barabara tutaanza kuijenga kwa sababu kinachosubiriwa ni kumlipa *advance* mkandarasi, ambaye tayari alisaini mkataba.

**MWENYEKITI:** Tumekuelewa Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Kawawa, kwa kifupi.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa hii nafasi. Ninaipongeza Serikali kwa kuanza ujenzi wa barabara ya kutoka Mnazi Mmoja mpaka Masasi. Sasa kuna hii barabara inayotoka Masasi mpaka Nachingwea, Nachingwea mpaka Liwale, kilometa 175. Pale tumeambiwa tutajengewa kilometa 75 kuanzia Liwale mpaka Kiangara. Mkandarasi amepatikana, lakini bado hajalipwa fedha na hajaanza kazi. Ni lini sasa Serikali itatoa fedha ili mkandarasi huyu aanze kazi kutoka Liwale kuelekea kiangara?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea hela katika bajeti inayokuja. Tumepanga bajeti,

ikipitishwa tutamlipa huyo mkandarasi *advance* ili aanze kujenga hiyo barabara, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Makete – Mbeya, mmemlipa fedha mkandarasi na mvua imesimama, anatakiwa aanze kufanya kazi. Ni ipi Kauli ya Serikali, hususan, kutokana na mkandarasi vifaa alivyonavyo *site,* havitoshelezi kuifanya kazi, na Serikali haijamtembelea. Ni lini Serikali itafika na kumpa vitendea kazi?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa tu maelekezo kwa sababu, mkandarasi tumemlipa fedha arejee *site* na aanze kazi ya ujenzi wa barabara hiyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuishie hapo. Bajeti ya Ujenzi inakuja, kwa hiyo, mtakuwa na nafasi ya kuongea na Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Ninamwita sasa Mheshimiwa Emmanuel Peter Cherehani, kwa niaba yake Mheshimiwa Azza Hamad, aulize swali.

Na. 261

**Fedha kwa Ajili ya Ujenzi wa Kituo cha Polisi, Ushetu**

**MHE. AZZA H. HAMAD K.n.y. MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatoa fedha, kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi, Ushetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kujenga Kituo cha Polisi, Ushetu, kwenye kiwanja chenye ukubwa wa mita za mraba 6,456 kilichopo katika eneo la Nyamilangano. Fedha, kwa ajili ya ujenzi wa kituo hicho zinatarajiwa kutengwa na kutolewa kwenye Bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha 2027/2028. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Azza Hamad, kwa niaba ya Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Sasa ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, wananchi wa Jimbo la Ushetu na Halmashauri ya Ushetu wameonesha haja kubwa ya kuwa na Kituo cha Polisi katika Kijiji cha Nyamilangano. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kutenga fedha, angalau kidogo kidogo, ili kuanzisha ujenzi wa kituo hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, wananchi wa Mji Mdogo wa Tinde wameonesha haja kubwa ya kuwa na Kituo cha Polisi, wametenga eneo na tayari wameandaa matofali 3,000 pale. Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuweka fedha kidogo kidogo, ili Kituo cha Polisi cha Tinde nacho kiweze kujengwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Azza kwa niaba ya Mheshimiwa Cherehani kwa maswali yake mawili madogo ya nyongeza. Ukweli ni msingi na ni muhimu kwa wananchi wa Ushetu kuweza kupata kituo katika eneo hili ambalo amelitaja la Nyamilangano kama ambavyo imeombwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imeshatoa taarifa ya msingi kwamba imeshapanga utaratibu wa ujenzi wa kituo hicho katika kipindi cha mwaka 2027/2028. Hilo lipo kwa mujibu wa mpango wa Serikali wa miaka mitano wa ujenzi wa vituo 75 vya Wilaya vya Polisi kikiwepo hiki ambacho nimekitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuhusu umuhimu wa kuanza kutenga fedha kidogo kidogo, ninataka nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya Serikali kuwa tutawaunga mkono wananchi wa Ushetu na sisi hata kama kupitia vyanzo vingine ikiwemo fedha za tuzo na tozo ama kwa fedha za matumizi ya kawaida na sisi tuweze kuweka mkono wetu kuunga mkono jitihada hizo za wananchi. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kafiti Kafiti, swali la nyongeza.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Ilemela ninapenda kuiuliza Serikali, ni lini itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi chenye hadhi ya wilaya katika Wilaya hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Kafiti Kafiti Mbunge wa Ilemela ambaye naye kama ambavyo walivyo Waheshimiwa Wabunge wengine, ameona umuhimu pia wa kuwa na Kituo cha Wilaya katika Jimbo la Ilemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, kama nilivyotoa majibu ya msingi kwamba tayari tunao mpango ndani ya kipindi cha miaka mitano unaoanza 2026 - 2030 wa kuhakikisha kwamba vituo vyote vya Polisi vya ngazi ya Wilaya ambavyo ni 75 viwe vimejengwa. Hivyo, niwaahidi pia wananchi wa Ilemela kwamba kituo chao cha Polisi nacho kitakuwa katika mpango huo na tutaweza kutenga fedha kwa mujibu wa hali ya bajeti kuhakikisha kuwa tunajenga kituo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa sasa waridhie na waendelee kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita ya kujenga Kituo cha Polisi ambacho kipo katika eneo la *Tunza Road* ambacho ni kituo cha Daraja C ili kituo hicho kianze kutoa huduma na baadaye tuweze kujenga kituo cha ngazi ya Wilaya.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea ndani ya Wizara hiyo nimwite Mheshimiwa Asha Juma Kombo, Mbunge wa Mfenesini, aulize swali lake.

Na. 262

**Ujenzi wa Kituo cha Polisi Mfenesini**

**MHE. ASHA JUMA KOMBO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga upya Kituo cha Polisi cha Mfenesini?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Asha na ninampongeza. Hivyo kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Juma Kombo, Mbunge wa Mfenesini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mpango wa kujenga kituo kipya cha Polisi Daraja "C" katika eneo la Mfenesini, ambacho kitagharimu kiasi cha fedha shilingi 165,228,990. Fedha hizo zinatarajiwa kutengwa kwenye bajeti ya Serikali ya mwaka wa fedha wa 2027/2028. Ninaomba kuwasilisha.

**MHE. ASHA JUMA KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini tuna maswali madogo mawili (a) na (b).

(a) Kwa kuwa, kiwango hiki cha fedha kinatengwa kwa mwaka wa fedha wa bajeti ujao, kwa nini Serikali isifikirie

kuongeza kiwango hicho cha fedha na kutujengea Kituo cha Polisi Daraja A?

(b) Kwa kuwa, Kituo cha Polisi cha Mfenesini kina eneo kubwa na linavamiwa na wananchi, je, Serikali haioni haja ya kutenga fedha na kukizungushia uzio kituo hicho?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Asha Juma Kombo kwa kuwa karibu sana na wananchi wake, pia kuwa karibu na Watendaji wetu wa Jeshi la Polisi katika Kituo cha Polisi Mfenesini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza kwa maswali yake mawili ya msingi ambalo swali la (a) anataka kujua kama hakuna uwezekano wa kituo hicho cha Polisi kupandishwa hadhi kwenda kwenye Daraja A.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, Kituo cha Polisi cha Mfenesini ni kituo cha Kata. Katika utaratibu wa ujenzi wa vituo vya Polisi tuna hatua tatu kwa nne. Hatua ya kwanza ni Daraja C ambacho kina uwezo wa kuwa katika Kata. Hatua ya pili ni Daraja C kinao uwezo wa kuwa katika ngazi ya Kata. Hatua ya pili, ni Daraja B kina uwezo wa kuwa katika ngazi ya Wilaya. Hatua ya tatu ni Daraja A ambacho kinakuwa katika ngazi ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Mjini Magharibi ambapo Jimbo lake lipo, kuna Kituo cha Polisi cha Daraja B pale Mwera ambacho kinaendelea kumaliziwa ujenzi wake. Tuna Kituo cha Daraja A kilichopo Mwembemadema kinaendelea kutumika kama Kituo cha Polisi cha Mkoa. Hivyo, katika mpangilio huo, eneo la Mfenesini kwa kuwa halijapewa hadhi ya kiutawala kipolisi kuwa ni Wilaya, maana yake litapaswa kubeba hadhi ya Daraja C.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa swali lake la pili ambalo ni la uzio katika eneo hilo, kwanza nimhakikishie

Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo la Jeshi la Polisi lililopo Mfenesini hadi sasa bado halijavamiwa na lipo salama. Ni eneo lililopimwa na limetolewa hati tarehe 17 Oktoba, 2021. Hati hiyo ina eneo lenye ukubwa wa *square meter* 5,624. Hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Jeshi la Polisi linaendelea kulinda eneo hilo na kuhakikisha kuwa lipo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ushauri wake wa kuzungushia uzio eneo hilo tunaendelea kulichukua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, utakuwa na nafasi ya kujibu zaidi wakati wa uchangiaji, ninadhani kwa majibu uliyoyatoa yanatosha kabisa.

Mheshimiwa Waziri, ninakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi, sasa nimwite Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, aulize swali lake.

Na. 263

**Safari za Mchana za *SGR* Dodoma - Dar – Dodoma**

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI** aliuliza: -

Je, lini Treni ya Mwendokasi itaanzisha safari za Mchana kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam na kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa niaba yake Naibu Waziri, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mbunge wa Mwanakwerekwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania linaendelea kutoa huduma ya usafiri wa treni kila siku kwa njia ya treni Dar es Salaam hadi Dodoma. Aidha, safari za treni kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma kwa siku ni treni nane na safari za treni kutoka Dodoma hadi Dar es salaam kwa siku ni treni nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upangaji wa safari za treni unaendelea kuboreshwa ambapo ukamilikaji wa mifumo ya uendeshaji utakapokuwa imefika 100%, shirika litaongeza safari za treni ili kukidhi hitaji kubwa la wateja hasa wateja wetu wanaotoka na kuelekea Zanzibar ili waweze kuunganisha na usafiri wa treni na huduma nyingine za usafiri wanapotoka au kuelekea Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kuwaomba wateja wetu kuwa wavumilivu katika kipindi hiki ambapo shirika linaendelea na ukamilishaji wa mifumo. Mifumo hii inatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa 2026/2027.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kassim Hassan Haji.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninamshukuru Naibu Waziri kwa kujibu majibu kwa ufasaha, lakini ninaomba niwape ushauri tu. Kwa kuwa treni hizi zinaondoka muda wa saa moja na nusu kupishana, kwa nini wasisogeze mbele hizi safari ikawa kama moja inaondoka saa tatu na nyingine iondoke saa saba mchana ili kuweka hawa watu wa katikati waweze kupata nafasi ya wao kusafiri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashauri sana Wizara waende wakaliangalie hilo, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, umepokea ushauri?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru. Mheshimiwa Neema Mgaya, swali la nyongeza.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, usafiri wa treni ni usafiri wenye bei nafuu zaidi ukilinganisha na usafiri mwingine; na kwa kuwa, Nyanda za Juu Kusini ni wakulima wazuri, wakubwa wa zao la parachichi pamoja na *horticultural* kwa ujumla ikiwepo Njombe, je, Serikali mmejipanga vipi kuhakikisha kwamba mnaweka mfumo wa *cold room* kwenye baadhi ya mabehewa ya reli ya *TAZARA* ili kuweza kuwasaidia wafanyabiashara hawa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Neema Mgaya kwa jinsi anavyofuatilia usafiri wa reli hususan kwenye upande wa *TAZARA* ambao upo Nyanda za Juu Kusini na inaunganisha na nchi zetu za Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kutokana na hili Shirika letu la *TAZARA* ambalo tulikuwa tunafahamu lilijengwa miaka ya 1970 wakati wa Mwalimu Nyerere, kipindi chote hicho lilikuwa likiendeshwa kwa uwezo wa chini. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya maamuzi kwa kushirikiana na viongozi wenzake wa China na Zambia na sasa hivi ninavyozungumza reli hiyo inakarabatiwa upya ili ule uwezo uliojengewa wa kusafirisha mzigo wa kutosha iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa aweze kuvumilia. Ushauri wake tumeupokea ili pengine katika maboresho hayo tuweze ku-*consider* na hicho alichokizungumza kuweka *cold room* maalum kwa ajili ya kuweza kusafirisha mazao au bidhaa muhimu kwenye ukanda huo ambao ni pamoja na parachichi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji. Ninamwita Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba, Mbunge wa Busokelo aulize swali lake.

Na. 264

**Mapitio ya Miradi ya Maji katika Jimbo la Busokelo**

**MHE. LUTENGANO G. MWALWIBA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafanya mapitio ya miradi ya maji Busokelo ili kubaini changamoto kwa baadhi ya miradi kutofanya kazi ipasavyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Lutengano George Mwalwiba, Mbunge wa Jimbo la Busokelo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha mapitio ya awali ya skimu zote 35 zilizopo Jimbo la Busokelo, ambapo skimu 19 zinatoa huduma ya maji ipasavyo wakati skimu 16 zinahitaji ukarabati kutokana na changamoto ya uchakavu wa miundombinu ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha uendelevu wa huduma ya maji, Serikali imekamilisha ukarabati wa skimu za maji 12 kati ya 16 zilizobainika kuwa na changamoto ambazo ni Kandete, Lwangwa, Kisegese, Kifunda, Ntapisi, Nswigala, Ikanu, Ipelo, Kalinga, Nyandege, Malyasi na Mpombo ambapo kwa pamoja zimegharimu zaidi ya shilingi bilioni 2.25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kupitia bajeti ya 2025/2026 Serikali inaendelea na ukarabati wa skimu ya Kabembe sambamba na upanuzi wa skimu ya Ikanu kwa gharama ya zaidi ya shilingi milioni 580.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kufanya mapitio na kukarabati miradi yote yenye changamoto ya uchakavu wa miundombinu nchini ikiwemo ya Jimbo la Busokelo kadiri fedha zinavyopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lutengano Mwalwiba, swali la nyongeza.

Waheshimiwa Wabunge, waliowasha *mic* tunaomba mzime, hakutakuwa na swali la nyongeza zaidi ya hilo hapa kwenye swali hili la maji.

**MHE. LUTENGANO G. MWALWIBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Ninaipongeza Serikali kwa majibu yake mazuri, lakini pamoja na majibu hayo, hali ya maji katika Miji ya Lwangwa, Isange na Kandete bado siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ipatayo kama mitatu; mradi wa Ntaba ambao unahudumia vijiji vinne vya Kambasegela, Mbambo, Kapulampunguti. Miradi hiyo mkandarasi amesimama, haendelei kufanya kazi kwa sababu ya kukosa fedha pamoja na mradi wa Kabembe. Je, ni lini Serikali sasa itapeleka fedha ili kuweza kutimiza azma njema ya Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwapatia wananchi wa Busokelo majisafi na salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba wanafanya ukarabati wa miradi mingine ambayo ufanisi wake unaonekana siyo mzuri kutokana na kwamba ni miradi ya muda mrefu zaidi ya miaka 20. Ni lini sasa kazi hiyo itakamilika ikiwepo kubadilisha chanzo cha Kalinga katika Kata ya Isangi? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kazi nzuri sana anayoifanya kwa ajili ya wananchi wake wa Busokelo.

Ninamhakikishia, tutaendelea kushirikiana naye kutatua changamoto ya upatikanaji wa majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi na kwa maelekezo na falsafa ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kumtua Mama ndoo kichwani, Busokelo mpaka sasa tunao upatikaji wa huduma ya majisafi na salama kwa 90%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua bado tunayo miradi ambayo inaendelea, bado ina changamoto, lakini kama ambavyo nimejibu katika jibu la msingi, Serikali inaendelea kutenga fedha ili kuhakikisha kwamba tunakarabati miundombinu ambayo imechakaa na skimu zote ambazo zilikuwa na changamoto ili kuhakikisha kwamba zinaweza kutoa huduma iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Ntaba ambao Mheshimiwa Mbunge ameutaja, mpaka sasa umefikia 50% ya utekelezaji wake. Mradi huu unagharimu zaidi ya shilingi bilioni 1.987. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, mradi huu tunaenda kupeleka fedha ili mkandarasi aweze kuukamilisha na wananchi wa Busokelo wapate huduma ya majisafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mradi wa Kabembe, mradi huu ambapo kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 tumetenga kiasi cha milioni 184 kwa ajili ya kwenda kuutekeleza. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Serikali iko makini kuhakikisha kwamba inawatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la chanzo cha Kalinga ndicho chanzo ambacho kinatumika katika Kata ya Isange. Changamoto yake ni kwamba kuna kipindi kinajaa tope na wananchi pale wanashindwa kupata huduma iliyokusudiwa. Kwa muktadha huo, tunatumia fursa hii kuwaelekeza wataalamu wetu waende wakafanya tathmini na kujiridhisha aina ya hatua inayotakiwa kuchukuliwa katika chanzo hiki, ama kama ni kubadilisha chanzo, ama kukikarabati ili kisiwe na changamoto ya

kujaa tope. Lengo ni kuhakikisha kwamba chanzo hiki kitoe huduma ambayo imekusudiwa kwa Watanzania. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Eng*. Andrea Kundo, ninakushukuru sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Nimwite Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, aulize swali lake.

Na. 265

**Kuimarisha Mifuko ya Uwezeshaji Wanawake**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuanzisha au kuimarisha mifuko maalum ya uwezeshaji kwa wanawake?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Mahawanga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, inatekeleza mpango madhubuti wa kuimarisha mifuko ya uwezeshaji kiuchumi ukiwemo Mfuko Maalum wa Maendeleo ya Wanawake *(Women Development Fund)* ambao upo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Mfuko huo unatoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wanawake wajasiriamali, iwe ni mtu mmoja mmoja au vikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mkakati endelevu uliopo ni kuimarisha mfuko huo badala ya kuanzisha mifuko mipya

sambamba na kuimarisha uwezeshaji wanawake kupitia miradi mbalimbali ya kisekta ya kukopesha wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, Serikali kupitia Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI iko katika hatua za mwisho za kuanza utoaji wa mikopo maalum kwa wanawake kupitia mradi wa pamoja utakaotekelezwa kwa ushirikiano na Benki ya Dunia, hatua itakayoongeza wigo kwa wanawake wengi kunufaika na mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuimarisha uwezeshaji wanawake kiuchumi kwa kushirikiana na sekta binafsi, taasisi za fedha na wadau wa maendeleo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga, swali la nyongeza.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani katika kufuatilia na kutathmini mikopo wanayopewa wanawake ili kuhakikisha kwamba mikopo hii inaleta tija na matokeo chanya kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni namna gani Serikali imejipanga kushirikiana na taasisi binafsi na benki ili kuleta tija zaidi na kuongeza wigo mpana kwa wanawake kupata mikopo na kurejesha kwa wakati?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Janeth Mahawanga. Ni Mheshimiwa ambaye ana-*deal* sana na makundi ya wanawake,

hususan kuhamasisha kukusanya vikoba, na vikundi mbalimbali. Hii inapelekea kuuliza maswali yenye tija sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina mkakati katika kufuatilia na kutathmini kama wanawake hawa wanaokopa wanapata matokeo chanya kiuchumi. Tayari sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum tunafanya hivyo. Hili linafanywa zaidi na maafisa wetu maendeleo ya jamii ambao wako mpaka ngazi ya kata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kule chini wanaendelea kuwafikia wanawake, kutoa ushauri, na vilevile wanahakikisha kwamba mikopo ile inaelekezwa kwenye malengo. Vilevile kuhakikisha kwamba wanawatia moyo kwamba wanaweza. Kuanzia ngazi ya vijiji kule, kupitia Maafisa Maendeleo ya Jamii ambao wapo kwenye kata, wanafanya kazi hii. Hivyo, mikopo hii hatuitarajii iwe mikopo chechefu au mikopo ile ya kuumiza kama mikopo ambayo mingine inaumiza mitaani, bali inakuwa yenye matokeo chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili juu ya kushirikiana na taasisi binafsi, pamoja na benki, sisi kama Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, tayari tunahusiana na benki takribani zote nchini. Ukifika pale kwenye Benki ya Azania utakutana na Mwanamke Hodari *Program*. Hii *program*, mwanamke anakopeshwa kwa riba rafiki, hivyo anaweza kukopa hata shilingi milioni 200 au shilingi milioni 300, shilingi milioni moja kulingana na *collateral* aliyonayo, andiko la mradi au maelezo ya mkopaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CRDB* pia wana *IMBEJU Program,* pia wanasisitiza wanawake kukopa kwa malengo na kulipa kwa wakati. *NMB Bank, NBC*, Benki ya Kilimo, vilevile tunapenda kuona kwamba wanawake wanashiriki kwenye shughuli za kilimo za kisasa, hivyo kule pia wanapewa mikopo. Wachimbaji wadogo wadogo wanawake, pia wameweza kujiunganisha, wanakopeshwa kwenye benki na wanaweza wakafanya vizuri sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru. Tunaenda kwenye swali la mwisho, Mheshimiwa Tamina Haji Abbas Mbunge wa Viti Maalum aulize swali lake.

Na. 266

**Elimu kuhusu Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)***

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutoa elimu kuhusu uwepo wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF)* ili wanawake wengi zaidi wanufaike na mikopo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tamima Haji Abass kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mikakati ya Serikali ya kutoa elimu kuhusu uwepo wa Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF),* ili wanawake wengi zaidi wanufaike na mikopo hiyo ni pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali, zikiwemo taasisi za fedha, kutoa mafunzo ya ujasiriamali na uendeshaji wa biashara kupitia makongamano ya kiuchumi ambayo hufanyika kikanda; kushirikiana na Wizara ya Fedha, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; na kufanya mafunzo ya ujasiriamali kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, Wizara inaendelea kuitaarifu mikoa na halmashauri juu ya uwepo wa mfuko huu na kuwaelekeza wafikishe taarifa husika kwa wananchi kupitia njia mbalimbali za mawasiliano, pamoja na

kupitia majukwaa ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa na wananchi, ambapo watekelezaji wakuu wa kazi za mfuko huu ni Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi zote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tamima Haji Abass, swali la nyongeza.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni kwa kiasi gani mfuko huu umewanufaisha wanawake tangu umeanzishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani wa kusimamia marejesho kwa wakopaji wa mfuko huu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri. Maswali yake ni mafupi, na majibu yako pia yawe mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Tamima kwa maswali mazuri. Hadi sasa sisi kama Wizara ni zaidi ya shilingi 1,400,000,000, tayari wanawake wameweza kunufaika na masharti ni nafuu. Kuhusu kusimamia marejesho, hii ni kazi yetu sisi sote viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaendelea kutoa elimu kwa wenzetu ambao tunawasemea, na vilevile kabla ya kupewa fedha wanapewa elimu ya fedha, lipa kwa hekima na vilevile rejesha kwa wakati. Kwa hiyo, tunaendelea kuona kwamba wapewe ndani ya mfuko ukiwa ndani ya Wizara kwa masharti nafuu, kabla hawajaendelea na usumbufu wa marejesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukapeleka hili kwenye vyombo vyetu vya fedha, kule ambako mpaka sasa wengi wetu tumeona kwamba wanalalamika masharti ni mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, sisi kwa umoja wetu Waheshimiwa Wabunge, kila mmoja ana kundi kubwa nyuma

yake, kila mmoja akiweza kusisitiza mtu akope na kulipa kwa wakati, basi wengi wataweza kurejesha ili wengi waweze kukopa.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kipindi cha maswali. Nina matangazo machache ya wageni waliopo ndani ya Ukumbi wa Bunge. Tunaanza na wale waliokaa Jukwaa la Spika.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Waziri wetu wa Maji, hawa ni Mhandisi Mwajuma Waziri, Katibu Mkuu Wizara ya Maji; Mhandisi Ruth Koya, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini; Mhandisi Abdallah Mkufunzi, Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Taifa wa Maji; Dkt. Maulid Maulid Mwenyekiti wa Bodi ya Chuo cha Maji; Mhandisi Ngosi Mwihava, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA)*; Mhandisi Romanus Mwangingo, Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira *DAWASA*. Karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile wapo Ndugu Salehe Taleb, Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Chunya; Mhandisi Herbert Kashilila, Mwenyekiti wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Nyasa; Mhandisi Wolta Kirita, huyu ni Mkurugenzi Mkuu Wakala wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Vijijini *(RUWASA);* Prof. Adam Karia, huyu ni Mkuu wa Chuo cha Maji; Wakili Haji Nandule, huyu ni Afisa Mtendaji Mkuu Mfuko wa Taifa wa Maji; Mhandisi Charles Mafie, huyu ni Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira, Wizara ya Maji; Ndugu Christina Akyoo, huyu ni Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Wizara ya Maji. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Heri Chisute, Mkurugenzi wa Ubora wa Maji, Wizara ya Maji; Mhandisi Nancy Mduma, Mkurugenzi Msaidizi Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira, Wizara ya Maji; Mhandisi Aron Joseph, Mkurugenzi Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dodoma; Mhandisi Mariam Majala, Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira RUWASA. *(Makofi)*

Pia tunaye Ndugu He Jun Joseph, Mkurugenzi wa Kampuni ya China *Civil Engineering Construction Company*; Mhandisi Aziz Mutabuzi ni Mkurugenzi wa Ufundi RUWASA; Mhandisi Mkama Bwire, Afisa Mtendaji Mkuu Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira DAWASA; Mhandisi Jabiri Kayilla, Meneja wa RUWASA Mkoa wa Geita; Ndugu Happiness Wilbroad, Mkurugenzi Mkaazi wa *Water for People*; Mhandisi Ngwisa Mpembe, Mjumbe wa Bodi wa *Tanzania Private Sector Foundation*. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Aweso ni familia yake kutoka Mkoani Tanga; Ndugu Omari Aweso, baba mdogo wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Mtanga Aweso, shangazi wa Mheshimiwa Waziri na Diwani wa Kata ya Ngamiani Kusini Tanga Jiji; Ndugu Kauthar Tarimo, huyu ni mke wa Mheshimiwa Waziri. Ahsante sana. *(Makofi/Vigelegele)*

Tunaye Ndugu Mwadawa Habibu, yeye ni dada wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Khadija Aweso, dada wa Mheshimiwa Waziri; Mhandisi Mbaraka Ally, Meneja RUWASA Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Mheshimiwa Mhandisi Kundo Andrea Mathew, Naibu Waziri wa Maji. Hawa ni Ndugu Nkeyenge, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Bariadi Mjini; na Ndugu Judith Ringia, yeye ni Kaimu Mkurugenzi Halmashauri ya Mji wa Bariadi. Karibuni sana. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Kundo ana wageni wengine 27 ambao ni Madiwani kutoka Halmashauri ya Mji wa Bariadi na Waheshimiwa Viti Maalum. Wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Jafar Rajab Seif, Naibu Waziri wetu wa TAMISEMI kutoka Taasisi ya *Blessed and Charity Foundation* ya Jijini Mwanza, wako pale. Mgeni mwingine wa Mheshimiwa Jafar, Ndugu Rhobu Kilango, yeye ni Afisa Itifaki wa Taasisi ya *Embassy Protocol* kutoka, Jijini Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Yupo mgeni wa Mheshimiwa Cosmas Mtesigwa Bulala, Ndugu Donald Limbe, ni mpiga kura wake kutoka Kwimba, Mkoani Mwanza, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Patali Shida Patali, yeye ni Mchungaji Elly Lufingo kutoka *Free Church In Christ*, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wawili wa Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, hawa ni wapiga kura kutoka Chunya mkoani Mbeya. Wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Mariam Nassoro Kisangi, hawa ni Watumishi wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Jijini Dar es Salaam, wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Vile vile wapo wageni 14 wa Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, hawa ni Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotoka Mkoa wa Katavi. Wako pale. Pia Mheshimiwa Sumry ana mgeni mwingine, huyu ni Sheikh wa Mkoa Katavi, Sheikh Mashaka Kakuluku, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 18 wa Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa, hawa ni viongozi vijana kutoka mikoa mbalimbali nchini, wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuna kundi la wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Hawa ni wachungaji 45 wa *Paradise Christian University* kutoka Mikoa ya Mwanza na Kigoma, wako pale, karibuni sana. *(Makofi)*

Vilevile tunao viongozi nane wa Taasisi ya Ruvuma *Development Organization* kutoka Songea Mkoani Ruvuma, wako pale, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 33 na walimu tisa Shule ya Sekondari Agape kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi 100 na walimu 10 wa Shule ya Awali na Msingi ya Chemchem kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa na Katibu wa Bunge kwamba, wanaopenda kujiunga na Chama cha Wabunge Maskauti Tanzania (CHAWAMATA) wanatakiwa wajioredheshe majina yao katika Ofisi ya Katibu wa Bunge, kuanzia leo tarehe 6 - 8 Mei, 2026. CHAWAMATA ni chama ni cha hiari chenye lengo la kukuza malezi ya vijana na kushiriki masuala ya kijamii. Hivyo, Waheshimiwa Wabunge wote wanaopenda au wenye historia ya kupitia skauti wanaombwa wajiorodheshe.

Haya ndiyo matangazo kwa sasa.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na hoja iliyo mbele yetu ya Wizara ya Maji. Tuna wachangiaji wengi leo, kwa hiyo, muda wetu umezidi kupungua, tutachangia kwa dakika tano. Tutaanza na Mheshimiwa Mwantumu Mzamilu Zodo, atafuatiwa Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko, Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, ajiandae.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaomba nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira yake ya dhati ya kutaka kumtua mwanamke ndoo kichwani, na dhamira hiyo tunaiona. Ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote,

akiwepo Katibu Mkuu, dada yangu Mwajuma, kwa kweli tunawaona Wizara hii wanavyokimbizana, na wote ni mashahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda ni mfupi sana leo, ninaomba niende moja kwa moja tu kwenye miradi michache, ambayo ninataka kuiongelea, hasa ya mkoa wetu wa Tanga. Sisi kwenye Mkoa wetu wa Tanga, mradi mkubwa ambao unaenda kuwa mkombozi wa maeneo mengi, ni ule mradi wa miji 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwenye mkoa wetu, maeneo ambayo yana changamoto kubwa za maji hasa, ni Kilindi, Handeni, Muheza na Korogwe. Kupitia mradi huu wa miji 28, ambao sasa hivi uko takribani 77% unaenda kuwa mkombozi kwa maeneo haya niliyoyataja, mpaka kwenye Jimbo lile la Mheshimiwa Waziri, Pangani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara kuongeza nguvu kwenye mradi huu. Mradi huu upo katika hatua nzuri, kubwa zaidi ni fedha. Wote tutakuwa mashahidi, tangu jana kila mtu anayesimama hapa kuongea, na ndiyo maana nikasema nianze kumshukuru Mheshimiwa Rais, kwani kila mtu kwenye jimbo lake kuna mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kuna mradi umekamilika au kuna mradi unaendelea, lakini miradi ipo inatekelezwa. Tutakuwa mashahidi wote, kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, pamoja na timu yake yote ya Wizara, tunawaona kwanza wanavyokimbizana, pili ni wasikivu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa iliyopo hapa ni upatikanaji wa fedha. Tuiombe Serikali ipeleke fedha kwenye miradi hii ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwona hapa Mkurugenzi wa Mfuko ule wa Maji, tukaongeze nguvu kwenye mfuko huu. Niwaombe Wizara ya Fedha tuongeze nguvu kwenye Mfuko wa Maji, tukaongeze hata shilingi 50 tu. Mfuko huu utakwenda kutusaidia, kwa sababu moja ya kazi za mfuko huu pia unasaidia

kutatua ile miradi chechefu, ile ambayo imekwama. Mfano mzuri ni ule Mradi wa Same - Mwanga - Korogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule umeenda kukamilishwa kupitia fedha hizi za Mfuko huu wa Maji. Niwaombe wenzetu wa Wizara ya Fedha tujaribu kuangalia mfuko huu na kuuongezea fedha hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe pia Wizara kujaribu kuongea na mamlaka nyingine za maji huku kwenye mikoa na huku kwenye halmashauri, waende wakajifunze Tanga kwenye ile *green bond,* maana lazima tutafute sasa vyanzo vingi vya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii ni mingi, hatuwezi kumaliza tu hivi kwa kusubiria hizi fedha bila sisi wenyewe kuanza kubuni vyanzo vingine. Kwa ile *green bond,* sisi Tanga tumefanikiwa. Uzuri hata gawio sasa hivi linaenda vizuri. Wameshagawiwa takribani mara nne. Kwa hiyo, tutangaze zile, watu wawekeze, tumalize miradi, halafu watu watapata gawio. Kwa hiyo, sasa na wengine waende wakajifunze pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimshauri kaka yangu, Mheshimiwa Waziri Aweso, tumeona pia hapa Waheshimiwa Wabunge wengi wameongea kuhusu kubambikiwa bili za maji na utatuzi mkubwa wa kuondoa kubambikiwa bili za maji, ni hizi mita za kulipia kabla ya matumizi *(prepaid meters)*. Mita hizi ni nzuri, lakini kuna baadhi ya maeneo tutakwenda kukwama kwa sababu ya mitandao. Kwa hiyo, ninaiomba Wizara ya Maji wakae na Wizara ya Mawasiliano kuhakikisha tunapata mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi tu pale Tanga nilikuwa na hii mita ya *prepaid*, *Engineer* Hill mwenyewe ni shahidi, na mimi niko kilometa sita kutoka pale mjini kabisa katikati ya mji na hakuna mtandao. Kwa hiyo, nikawa nashindwa kuweka, lakini pia Mheshimiwa *Engineer* Ulenge naye pia hivyo hivyo alikuwa na hii mita, imebidi waje wazifungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasa tuombe Wizara ya Maji wakae na Wizara ya Mawasiliano kuhakikisha mawasiliano yanakuwa sawasawa ili tusije tukakwama kwenye hizi mita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba kaka yangu Mheshimiwa Waziri, ule mradi wa Mkinga - Horohoro sasa hivi uko hatua nzuri na wakati ule Mheshimiwa Rais anapita kwenye zile siku 100 aliahidi tabasamu kwa wananchi wale. Ninawapongeza pia kuna kijiji kimoja pale cha Mtimbwani tayari wameanza kupata maji kama Mheshimiwa Rais alivyoelekeza, ninawashukuru wametekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninawashukuru kwa jitihada walizochukua kwa sababu sasa hivi wamenunua mabomba yote ya mradi mzima shilingi bilioni saba. Kwa hiyo, ninawaomba Wizara twende tukakamilishe ule mradi tuweke nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zodo. Nilimwita Mheshimiwa Adonis Alfred Bitegeko, Mheshimiwa Sumry atafuatia.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Maji. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ambayo kwa dhahiri ameonesha kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona dhamira yake ya dhati kabisa kuwezesha wananchi wengi kupata huduma ya maji mpaka sasa hivi imefikia 85.2% kutoka 70.1% mwaka 2021 wakati anaingia madarakani. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa sisi wakazi wa vijijini kuona kwamba huduma hiyo imeimarika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri wake na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Mimi kama Mbunge wa

Muleba Kaskazini nimekuwa nikipata ushirikano mkubwa sana kutoka kwao hasa pale ninapofuatilia miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru sana, kwa kuwa katika miaka mitano iliyopita Jimbo la Muleba Kaskazini lilipata miradi mitano ya maji ambayo yamesaidia sana kuimarisha huduma za maji na kuongeza asilimia ya upatikanaji wa maji mpaka kufikia 81% kutoka 74%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na mafanikio haya, sisi katika Jimbo la Muleba Kaskazini bado tuna miradi miwili mikubwa ya maji ambayo tunaisubiri. Tuliahidiwa katika mwaka huu wa fedha miradi hiyo itakuwa imetekelezwa (mradi wa maji wa Iroba na mradi wa maji wa Makongora).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miradi ambayo wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini wamenituma niiombe Serikali iweze kuitekeza miradi hii, kwani itasaidia sana kuleta huduma za maji katika wakazi takribani 9,000 katika maeneo hayo na maeneo ya jirani ya vijiji hivyo. Pia tunatarajia kwamba katika mwaka ujao wa fedha tutapata visima vitatu ambavyo vitasaidia sana katika kuboresha huduma ya maji katika Jimbo la Muleba Kaskazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi ambalo ninaomba niliseme hapa leo ni kwamba katika miradi mitano ambayo imetekelezwa katika Jimbo la Muleba Kaskazini, tuna mradi mmoja wa Kagoma ambao utekelezaji wake umefikia 96% bado asilimia nne kukamilika, lakini bado mkandarasi anadai fedha shilingi milioni 119 ili kukamilisha mradi huo. Tunaomba sana Serikali isimamie ili mkandarasi huyu aweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali ya kuleta maombi hayo ya Jimbo la Muleba Kaskazini, ninapenda pia kushauri Serikali kwamba ukiangalia dira yetu ya 2050 imetoa kipaumbele sana katika sekta ya binafsi kuweza kuchangia katika kuleta mafanikio ya maendeleo. Ninaamini kwamba maji pia ni uchumi. Ninaamini kwamba ni wakati mwafaka sasa hivi Serikali ikafungua milango kuruhusu sekta binafsi iweze kushiriki katika kutoa huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni suala la msingi sana, tumeona mafanikio kule Tanga kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge aliyetangulia kwamba imesaidia sana uuzaji wa hatifungani. Ninashauri kwamba sisi tufungue pia fursa zaidi kwa wawekezaji waingie kuwekeza katika sekta ya maji ili kusaidia sana katika kuongeza zaidi miradi mingine ya maji, lakini pia kufadhili miradi ya maji. Tumeona pia katika upande wa barabara, *Samia Infrastructure Bond* imesaidia sana katika kuongeza uwezo wa Serikali katika ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaamini kabisa sekta binafsi ikishirikishwa, basi tutaweza kufika mbali katika kufanikisha mipango yetu ambayo kimsingi itasaidia sana maendeleo yetu ya sekta ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia hili pengine ni jambo la jumla la Kitaifa, nimeona kwamba katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2025/2026 kwamba ilipangwa miradi 1,318 vijijini, lakini mpaka tunafikia mwezi wa nne ni miradi 54 tu imeshatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba Serikali iongeze nguvu zaidi katika kukamilisha miradi mingine 992 ili tuweze kupata huduma zaidi ya maji na kufikia yale malengo kusudiwa ya kuona kwamba kila kijiji kinapata huduma ya maji ifikapo mwaka 2030. Ninaamini kabisa kwamba kwa mpango kabambe wa Serikali ambayo imeuandaa, tutaweza kufikia yale malengo tarajiwa ya kutoa huduma za maji kwa kila kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninapenda kutumia fursa hii kwa kuwa ninahitimisha pia mchango wangu, ni kwamba ninawashukuru wananchi wa Jimbo la Muleba Kaskazini kwa jinsi wanavyoniamini. Nami ninapenda kuwahakikishia kwamba chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mimi pamoja na madiwani tutapambania kuona kwamba wanapata maji ya uhakika na usalama katika vijiji vyote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bitegeko, ahsante sana.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana. Nilimwita Mheshimiwa Haidary Hemed Sumry, atafuatiwa na Mheshimiwa Isack Joseph Copriano, Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau ajiandae.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya na uhai. Niendelee kumpongeza na kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kwenye eneo hili la sekta ya maji kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama nisipomshukuru Mheshimiwa Waziri wa Maji na Mheshimiwa Naibu wake na wataalamu wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kwenye eneo hili la kuwahudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mpanda uko miongoni mwa miji ambayo ina miradi ya miji 28. Mradi huu ukikamilika utakwenda kupunguza kabisa changamoto ya maji tuliyonayo kwa sababu Mji wa Mpanda kwa sasa unapata lita milioni sita, lakini mradi huu ukikamilika, utatuongezea upatikanaji wa maji kutoka lita milioni sita mpaka lita milioni 18.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaona kabisa mradi huu utaenda kuwa mkombozi kwa wananchi wa Jimbo la Mpanda mjini. Ombi langu kwa Wizara ni kwamba itusaidie kusukuma huu mradi kwa sababu mradi huu ulikuwa ukamilike Oktoba, 2025 lakini kuna ahadi ya Wizara kwamba mradi huu utakamilika mwezi wa Saba mwaka 2025, lakini kinachoendelea kule *site* kinatutia mashaka kwamba mradi huu utaenda kukamilika huu mwezi wa Saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana ndugu yangu Mheshimiwa Aweso, kaka yangu, twende atusaidie ku-*push* hawa wakandarasi ili mwezi wa Saba kweli maji yatiririke Mpanda na changamoto ya maji iondoke kwenye Mji wetu wa Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu ya pili, tuna kata za pembezoni ambazo zilikuwa zinahudumiwa na *RUWASA*, lakini kwa kuwa mji wetu ni Manispaa, miji yote ile ya pembezoni imerudishwa kuhudumiwa na Mamlaka ya Maji Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi mfano kwenye Kata ya Mwamkulu, Kata ya Kakese, Kata ya Misunkumilo na Kata ya Magamba; kwenye kata hizi za pembezoni kuna miradi ambayo ilikuwa inafanywa na *RUWASA*, lakini sasa hivi imekuwa kama imesimama kwa sababu ukienda Mamlaka ya Maji hamna bajeti yake. Ukienda *RUWASA*, wameshaikabidhi Mamlaka ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba ndugu yangu, kaka yangu Mheshimiwa Aweso aende akaiamshe hii miradi. Wananchi wa Kakese na Mwamkulu wanasubiria hii miradi ikamilike ili waweze kupata maji kama yeye alivyosema, maji hayana mbadala, na ni ukweli usiyopingika kwamba maji hayana mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba hii miradi iende ikakamilike ili iweze kuwahudumia wananchi wangu wa Jimbo la Mpanda Mjini. Ninaamini huko waliko wananisikia, ninaongea Mheshimiwa Mbunge wao hapa, *message* imefika na ninaomba kama kuna uwezekano, kama ni Waziri au Naibu Waziri, basi waende wakatembelee kwenye hizi kata ili wakaone adha ambazo wananchi wanazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninamshukuru Mheshimiwa Waziri. Kipindi cha kampeni, yeye na Mheshimiwa Mgombea wa Urais walikuja kwenye jimbo langu, na mimi kama mgombea kipindi kile nilimwomba sana aende akaitembelee Kata ya Magamba, lakini akaniambia ndugu yangu Sumry, mimi sasa hivi siyo Waziri, hapa nimemsindikiza tu Mheshimiwa Rais kuja kuhakikisha kwamba tunapata kura za kutosha, lakini ninakuahidi baada ya Mheshimiwa Rais kuchaguliwa, na Mungu akijalia nikawa Waziri wa Maji, nitahakikisha hiyo Kata ya Magamba tunakwenda kupeleka maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri kwenye jimbo langu, hii Kata ya Magamba na ilikuwa *commitment* yangu kwa wananchi kwamba nitapambana usiku na mchana, nitashawishi kuhakikisha kwamba wanapelekewa maji. Ziko dalili, nimeongea na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Mpanda ameniambia ziko dalili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dalili peke yake hazitoshi. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwenye bajeti hii awapelekee maji wananchi wa Kata ya Magamba na watamwandika kwenye historia kwa sababu kata hii ni kata kubwa, lakini kuna kisima kimoja na wananchi wote wanaenda kuteka hapo maji kwenye kisima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri akienda kukitembelea hiki kisima anaweza akakuta ndoo zaidi ya 2,000 zinasubiria huduma ya maji. Kwa hiyo, ninaomba sana chondechonde Mheshimiwa Aweso anisaidie, aniokoe kwenye hili eneo, wananchi wa Kata ya Magamba nao waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri amekuja kwenye Mkoa wa Katavi mimi nikiwa Meya na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Katavi tukamsukuma kuhakikisha kwamba...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia kwa kuunga mkono hoja.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naongelea mradi ule wa gridi ya Taifa, nafikiri Mheshimiwa Waziri amenielewa, tumeona na tunaomba a-*push* ili mradi huu uanze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Isack Jeseph Copriano, atafuatiwa na Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, na Mheshimiwa Martha Festo Mariki ajiandae.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na mimi kwa kupatia nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miradi ambayo ametupa Wilaya ya Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tu niseme, kwa sababu dakika tano hizi ni chache, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Watumishi wote wa Wizara ya Maji, ninajua wananisikia walioko kule Monduli, Arusha kwa sababu wote wanahudumu kwenye Wilaya ya Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na ushauri tu kidogo. Mheshimiwa Waziri ningetamani sana kwenye wilaya yangu pasianzishwe miradi mipya. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri akasimamie miradi hii niliyopewa na Mheshimiwa Rais, miradi ya vijiji 13. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, wameweka mguu chini, wametengeneza *MoU* kati ya Wizara na *pipe industry* kwa ajili ya ku-*produce* mabomba yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika sana na nilipata fursa ya kutembelea, na nimeona mabomba yanaendelea kutengenezwa. Ombi langu ni kwamba, ninajua mara nyingi ninakutana na Mheshimiwa Waziri, na aliniambia, "jambo moja ambalo nitakufanyia ni kuhakikisha vijiji 13 vilivyokuwepo Monduli vinapata maji."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, vipaumbele visitolewe kwenye miradi mipya, vitolewe kwenye miradi ambayo imeanza kutekelezwa. Itatusaidia sana kuondoa changamoto ya maji kwenye wilaya zetu. Kuna mradi Makuyuni wa vijiji saba ambao unagharimu karibu shilingi bilioni saba. Mradi

ule umeanza na tayari ulishapelekewa karibu shilingi milioni 800 pale inaendelea. Ninaomba mradi ule ukamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hilo tu, kuna mradi kule kata ya Mfereji - Donyonaado wa shilingi bilioni 1.5 umeshapelekewa shilingi milioni 250. Ninaomba mradi ule upelekewe fedha ili ukamilike. Siyo hilo tu, kuna mradi mwingine wa Bwawa la Somweinen, Mheshimiwa Naibu Waziri atakumbuka, alikuja nikiwa Mwenyekiti wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi pale alikuwa anasuasua tukamwondoa na mradi ule sasa unafanyika kwa *force account*. Ninaomba basi angalau ziongezwe fedha wananchi wale wapate huduma ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua Wilaya ya Monduli ni wilaya ya kame. Kipindi hiki cha ukame, sisi tulivyopata matatizo mengi ya maji, ninajua kabisa jinsi Mheshimiwa Waziri alivyojitoa, na mimi ninashukuru sana Wizara yake. Juzi tumetukarabatiwa Bwawa la Nanja. Leo tunavyozungumza maji yale wameshayazuia na wananchi wangu wanapata maji. Sasa Bwawa la kule Somweinen likikamilika itanisaidia kupunguza tatizo la maji hususan kwa mifugo na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, apeleke fedha kwenye mradi ule unaotekelezwa na *USA*. Mradi ule umekwama pale msituni kwa zaidi ya miaka mitatu sasa na mradi ule unafanyika kwa *force account*. Mheshimiwa Naibu Waziri anakumbuka, jana niliuliza swali dogo na akaniahidi kwamba watapeleka fedha. Miradi viporo iliyoko Monduli ikikamilika itaniondolea kesi kubwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesimama kumwomba Mheshimiwa Waziri kwa dhati kabisa, na ninajua anatosha kwenye kiti hicho na chenchi inabaki, kwa dhati kabisa ninaomba anipelekee fedha Monduli, wananchi wangu waondokane na tatizo la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwezekana, wakati tunaendelea kutekeleza miradi hii, na kwa kuwa Mheshimiwa Waziri anajua Monduli ina shida ya maji, basi aninunulie hata boza wananchi wangu wachote maji kutoka Arusha kipindi tunatekeleza miradi hii. Itanisaidia sana kupunguza tatizo hili wakati tunatekeleza miradi mikubwa ambayo tumeletewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimwomba Mheshimiwa Waziri tangu muda mrefu, na boza halitazidi hata milioni 300 au 250. Ukininunua boza, wananchi wataweka mafuta, watachangia, na maji yatakuwa yanapelekwa wakati tunatekeleza hii miradi mizuri ambayo kimsingi unaona ni jinsi gani Mheshimiwa Rais amewakumbuka wananchi wa Monduli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nimesimama kuomba sana kwa dhati nisianzishiwe miradi mipya Monduli, tukamilishiwe miradi hii viporo. Nitakuwa na amani na jimbo lile litatawalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo sina mengi, ninakushukuru na kuipongeza na Wizara hii, na niseme tu kazi inayofanyika kwenye wilaya yangu hususan ma-*engineer* wanafanya kazi nzuri, *RUWASA* wanafanya kazi nzuri, na *AUWSA* wanafanya kazi nzuri, ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mheshimiwa Waziri amesimama kidete kusema anawatua ndoo kichwani akina mama wa Monduli. Ninaomba sana kwa dhati aende kukakamilisha miradi hii ili wananchi wangu wakapate huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa 300%, wananchi wangu wapate maji, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Martha Nehemia Gwau, Mheshimiwa Martha Festo Mariki na Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, wajiandae.

**MHE. MARTHA N. GWAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninaomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ushindi mkubwa wa kishindo. Pia, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Makamu wa Rais, na pia ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri Mkuu wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani kubwa kwa Chama changu cha Mapinduzi, na shukrani kubwa zaidi kwa akina mama wa Mkoa wa Singida kwa kunipa kura nyingi za kishindo na kufanya nije hapa Bungeni kwa awamu nyingine ya pili kuwawakilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kupongeza Wizara ya Maji chini ya Mheshimiwa Waziri Aweso kwa kazi kubwa anayoifanya, na chini ya Katibu Mkuu mwanadada mahiri *Engineer* Mwajuma. Kwa kweli wanafanya kazi nzuri na wanahitaji kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa fadhila, niwapongeze Mameneja wa Mkoa wa Singida wanaohudumia suala zima la maji. Meneja wa *RUWASA, SUWASA,* bonde na wale wa Mamlaka ya Miji Midogo, wanafanya kazi nzuri na wanatushirikisha Waheshimiwa Wabunge vizuri katika kuwatatulia wananchi wa Mkoa wa Singida changamoto zao katika suala zima la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, maji ni uchumi. Dira ya Taifa ya 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi na dhamira ya dhati ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kumtua mama ndoo kichwani. Tunakiri tulipo sasa siyo sawa na tulipotoka miaka 10 iliyopita. Kwa hiyo, jitihada kubwa imefanyika, mikakati mingi imefanyika kwa weledi mkubwa kututoa hapa tulipo. Tunashukuru na tusiwe wachoyo wa fadhila, tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri au maombi machache kwenye Wizara ya Maji. Ombi la kwanza mikoa inatofautiana. Tuna mikoa ambayo ina changamoto ya vyanzo vya maji, na tuna mikoa ambayo ni kame kama Mkoa wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wetu wa Singida una changamoto kubwa ya upatikanaji wa maji ya chini ya ardhi. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali na tunaomba Wizara ya Maji wawekeze kithabiti kuhakikisha kwamba tunapata vifaa vya kisasa ambavyo vitaenda kuchimba chini zaidi ya ardhi ili waweze kupata maji kirahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto hii inasababisha zoezi la miradi kurudiwa, kutokufanikisha miradi kwa wakati, lakini hata ongezeko la fedha. Kwa hiyo, tunaomba mikoa yetu kame isaidiwe kuwa na mkakati mbadala wa kuhakikisha tunapata vifaa vya kisasa ili tunapofanya mradi tusirudie mara ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Waziri Aweso, pamoja na kazi kubwa anayofanya ila atuangalie mikoa kame isiyokuwa na vyanzo vya maji iweze kuwa na njia mbadala au vifaa vya kisasa vya kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni ombi. Tuna vijiji 59 Mkoa wa Singida ambavyo havijawahi kuona maji kabisa, wanatumia maji ya visima vya kienyeji, lakini maji yao siyo salama. Vijiji hivyo ni Mkalama, kuna vijiji sita; Manyoni, vijiji 21; Singida *DC* ina vijiji vitano; Iramba, vijiji nane, na Ikungi, vijiji 19. Tunaomba Wizara iwekeze sasa kwa wasiyonacho kabisa. Walionacho wasubiri wasiyonacho kabisa ili tuweze kufaidi keki ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Aweso alisema, wote tunatoka vijijini. Kama wote tunatoka vijijini, kuna wanaoongelea maji yanatoka mara mbili kwa wiki, kuna wanaoongelea maji yanatoka mara moja kwa wiki, na kuna yule Mtanzania ambaye hajawahi kuona maji kabisa. Kwa hiyo, tunaomba bajeti hii ya mwaka huu wa fedha iwafikirie wasiyonacho kabisa ili tuweze

kuongea lugha moja, hata kama tukiwa na mgao, basi Watanzania wote tuwe nacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mheshimiwa Aweso ni msikivu, nina hakika kabisa anaenda kutatua vijiji vyote visivyo nacho kabisa ili wote tupate keki ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Singida tuna mradi wa miji 28 unatekelezwa katika Mji wa Manyoni, Mji wa Singida, Manispaa ya Singida, na Mji wa Kiomboi. Tunaiomba Serikali, imefika hatua nzuri, tunashukuru. Tunaomba mradi huu umaliziwe kwa haraka ili usaidie kutatua changamoto ya maji katika hiyo miji midogo niliyoitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mradi wa Ziwa Victoria, nilieleza changamoto ya vyanzo vya maji. Tunaomba na wenyewe ukamaliziwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Martha Festo Mariki, atafuatiwa na Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, na, Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, ajiandae.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema aliyetujalia uzima na afya njema. Pia ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kwa kuonyesha nia ya dhati ya kumtua mwanamama ndoo kichwani kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu Waziri wa Maji, Katibu Mkuu, dada yangu Mwajuma pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Maji kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niendelee sana kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Waziri wa Maji kwa kuona umuhimu wa kutenga shilingi bilioni sita kwa ajili ya upembuzi yakinifu ya kutoa maji katika Ziwa Tanganyika na kuyaleta katika Mji wa Mpanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mji wa Mpanda ni mji ambao unakua sana na Mkoa wa Katavi ni mkoa pekee ambao umeonyesha katika sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 kwamba ni mkoa ambao una ongezeko kubwa sana la watu wanaokuja kutafuta fursa mbalimbali za kibiashara ndani ya Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Mkoa wetu wa Katavi ni dhahiri kwamba sasa unahitaji maji ya uhakika na maji ya uhakika ni kutoa Ziwa Tanganyika na kuyaleta katika Mji wa Mpanda kwa ajili ya wananchi waweze kupata maji ya uhakika muda wote na wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutamani jambo zuri siyo mbaya kwa sababu, kama imewezekana kwa kutoa maji Ziwa Victoria na kuyaleta katika Mikoa ya Tabora mpaka Dodoma hapa tunaambiwa wanakuja, tunaamini na sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi, Rukwa pamoja na Kigoma, mradi huu wa kutoa maji Ziwa Tanganyika unawezekana katika eneo letu na sisi tuweze kupata maji ya uhakika na maji salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee sana kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Maji katika Kata ya Maji Moto Halmashauri ya Mpimbwe tunao mradi wa maji ambao kwa kweli unahitaji tuweze kupata chujio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kabisa kipindi cha masika ambapo mvua zinanyesha, wananchi wale hususan akina mama, wamekuwa wakipata taabu sana kutokana na kwamba tu hatuna chujio. Wamepata maji yenye tope kutokana na ukosefu wa chujio, na kipindi cha masika kutokana na mvurugiko mkubwa wamepata maji ambayo siyo majisafi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aweze kututengea fedha, atuletee, ili wananchi wa Kata ile ya Mamba waweze kupata maji ya uhakika. Pia ninaomba usambazaji wa maji kutoka Mamba kwenda Mbede na maeneo ya Kasansa mpaka Ikuba. Hili likifanyika, itawasaidia sana akina mama wale wa Mkoa wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wale wamenituma, wanaomba sana Mheshimiwa Waziri aweze kuwapatia fedha kwa ajili ya usambazaji. Hata hivyo, kikubwa zaidi ni chujio ili akina mama wale na wenyewe waweze kupata maji ya uhakika. Tunatambua panapokuwa na changamoto ya maji wanaopata changamoto kubwa sana ni akina mama. Kwani wamekuwa wakihangaika mpaka usiku kwenda kuhakikisha kwamba wanatafuta maji safi na salama kwa ajili ya familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri anatambua maji hayana mbadala. Ni wakati sasa wa Taifa letu kutupia sana jicho katika Wizara ya Maji. Tunatambua kwamba, kwa kuwa maji hayana mbadala, mtu anaweza akawa hana umeme, lakini akaishi. Hauwezi ukaishi kama majisafi na salama hayapatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaiomba sana Serikali yangu, ni muda sasa na wakati wa kuweza kuwaongezea fedha Wizara ya Maji kwa kuwa maji hayana mbadala ili sasa tuweze kutatua changamoto ya maji. Kwani tunatambua ni zaidi ya vijiji vingi sana ambavyo havina kabisa maji, hawajawahi kupata historia ya maji wala hawajawahi kuona maji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri pamoja na watendaji wako, lakini tunaiomba sana Serikali hususan Wizara ya Fedha, ni muda sasa na wakati wa kuhakikisha kwamba Wizara hii inakuwa ya kipaumbele. Sote tunajua maji ndiyo yenye umuhimu. Hata mtu anapopoteza maisha, tunatambua kwamba huwezi ukapelekwa kupumzishwa katika makazi yako ya milele bila kuoshwa. Hapa pote tunaona tunatumia maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa kuwa wote tunajua umuhimu wa maji, mama akijifungua yanahitajika maji. Kwa hiyo, tunaona maji ni kitu muhimu sana na hakina mbadala wowote. Ni muda sasa wa Wizara hii iweze kuongezewa fedha kwa ajili ya kutatua changamoto za maji na miradi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana, ninaunga mkono hoja, na ahsante sana. Maji hayana mbadala. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala.

**MHE. FARAJI B. NANDALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili nami niwe miongoni mwa wachangiaji kwenye Hotuba hii ya Wizara ya Maji iliyowasilishwa na Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Aweso na Naibu wake Mheshimiwa Kundo Mathew.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kuchangia, nichukue nafasi hii kuanza kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa moyo wake wa dhati na wa upendo wa kuona namna gani anataka kumtua mama ndoo kichwani. Dhamira yake hii imeonekana mapema kabisa wakati anaingia madarakani mwaka 2021 wakati bajeti yake ya kwanza kabisa aliyoanzisha ya shilingi bilioni 756 na leo hii tunazungumzia zaidi ya shilingi trilioni 1.12 zaidi ya ongezeko la 68%. Hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia kwa dhamira yako hii ya dhati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na muda, nitakwenda mbio mbio ili nijaribu kuwasilisha yale ambayo wananchi wa Ndanda wameniagiza. Kwanza kabisa nilete shukrani zangu kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia fedha shilingi milioni 360 kwa ajili ya ujenzi wa chujio ambapo kesho kutwa siku ya tarehe tisa tunakwenda kuzindua na Mwenge wa Uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nichukue nafasi hii kumpongeza pia Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutafutia *alternative* ya fedha zaidi ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi

wa chujio kwenye chanzo cha maji cha Mbwinji ambapo chanzo hiki ni kikubwa na tegemezi sana kwa zaidi ya majimbo manne yaliyopo kwenye Jimbo la Ndanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Ndanda wanashukuru sana kwa hizi fedha ambazo zimetolewa na Serikali. Pia Jimbo la Ndanda ndiyo *hub* ya maji kwa zaidi ya majimbo manne au matano yaliyopo Mkoa wa Mtwara. Maji mengi yanatokea kwenye Jimbo la Ndanda, na hii inathibitika kupitia mradi wa *MANAWASA* ambao unazalisha zaidi ya lita za maji 8,100,000; lakini uzalishaji wa maji haya umekuwa hauwanufaishi hasa wananchi wa Jimbo la Ndanda na kuwanufaisha zaidi majimbo mengine kwa mfano Nachingwea, Masasi Mji na Ruangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Ndanda ndio walinzi wa mradi huu mkubwa wa *MANAWASA* kupitia chanzo cha Mbwinji, lakini mpaka leo hii ni kata nne tu ambazo zinanufaika kupitia mradi huu wa *MANAWASA*. Hivyo, wananchi wa Jimbo la Ndanda wamenituma nije nikuombe na wao wanahitaji wanufaike kupitia mradi huu wa *MANAWASA* kwa sababu mradi huu wa *MANAWASA* ndiyo mradi ambao unatoa maji ya baridi, na mazuri ukilinganisha na kata nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwepo huo kuna mambo ambayo wananchi wa Jimbo la Ndanda wanataka kuyoana. Kwanza kabisa uzalishaji kwenye vyanzo vingi vya maji kwenye Jimbo la Ndanda umeendelea kupungua kutokana na shughuli za kibinadamu kuongeza na uchimbaji wa madini na kilimo. Hii husababisha uzalishaji wa maji kwenye Jimbo la Ndanda kupungua na kusababisha mgawanyo mkubwa wa maji kwenye Jimbo la Ndanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, wananchi wa Jimbo la Ndanda wanaomba Serikali ikiwezekana, basi iwekeze fedha kwenye ujenzi wa Bwawa Mkumba Shamba lililoko kwenye Jimbo la Nachingwea, Bwawa lile ambalo lina uwezo wa kuzalisha lita bilioni 24 kwa mwaka na lita milioni 66 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi kuanzishwa kwa mradi huo kutasababisha watu wa Nachingwea waweze kuwa na maji yao pekee badala ya kutegemea maji kutoka kwenye Jimbo la Ndanda, na yale maji ambayo yanatoka kwenye Jimbo la Ndanda yaende kuhudumia wananchi wa Jimbo la Ndanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wananchi wa Jimbo la Ndanda wanaomba kama Serikali itawapendeza wawekeze kwenye mradi wa maji wa Mahiwa Nyangao mradi ambao utakuwa na uwezo wa kuzalisha zaidi ya lita milioni tisa na kutatua changamoto ya maji kabisa kwenye Jimbo la Ndanda na Wilaya ya Masasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Jimbo la Ndanda ndiyo Jimbo ambalo linaongoza kwa uzalishaji wa maji, zipo changamoto. Kwa mfano, leo hii kwenye Jimbo la Ndanda kuna zile *DP (Domestic Point)* 219 kwa ajili ya uuzaji wa maji, lakini mpaka kufikia jana ni *DP* 70 tu ndizo ambazo zinafanya kazi wakati *DP* 219 hazifanyi kazi na kusababisha wananchi wengi wa Jimbo la Ndanda kukosa huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya hizi *DP* kutokufanya kazi, kwanza kabisa wanalalamika wale watoa huduma kwamba wanabambikiwa fedha za ukusanyaji wa mapato kutokana na hizi *DP*. Leo hii wanakusanya fedha, wakienda kwenye hizi mamlaka kupeleka zile fedha, wanasema fedha mliyokusanya ni ndogo na bili iliyosoma ni kubwa. Wale watendakazi wanaacha kazi kwa sababu mishahara yao na posho zao zinatumika kwenda kufidia madeni zinazotokana na hizi *DP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, kwanza wale watu ni watendakazi, siyo waajiriwa wa moja kwa moja. Ni watu tu ambao wanachukuliwa. Ninaomba mamlaka zitoe ajira kwa wale wafanyakazi, waajiriwe; wapate ajira za kudumu ili mzigo wa hili deni linalotokana na kuongezeka kwa bili usiende kuelemea kwa wale watendakazi, uwe wa mamlaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ushauri wangu mwingine, mamlaka za upimaji (wakala wa upimaji) wawe na utaratibu wa

kuzipima hizi mita mara kwa mara kuangalia ufanisi wake na ili kuondoa huu mzigo mkubwa ambao wananchi wanalipa bili ambayo ni tofauti na kile ambacho wametumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ushauri mwingine kwa hizi mamlaka, zichukue hatua ya haraka kabisa katika kutoa ajira ili hizi *DP* 219 ziweze kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo na kutokana na muda haya mambo mengine, nitachangia kwa kutumia njia ya mtandao. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tuna wageni wengine 27 wa Mheshimiwa Jesca Yuda Mbogo, hawa ni Madiwani wa Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana kwenye Bunge letu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Nilimwita Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, na Mheshimiwa Daniel Awack, ajiandae.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Ninaomba nimtangulize Mwenyezi Mungu katika mchango wangu. Pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya na kuhakikisha wanawake wanatuliwa ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimpe pongezi nyingi sana Mheshimiwa Waziri Jumaa Aweso, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, dada yetu *Eng.* Mwajuma kwa kazi nzuri ambayo wameendelea kuifanya katika Wizara hii ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze pia Meneja wa Mkoa wa Iringa wa *RUWASA* pamoja na *IRUWASA,* kwani wamekuwa msaada sana katika mkoa wetu katika hii miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kilolo wanaendelea pia kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, tumepata miradi 40 ambayo imeweza kusaidia vijiji 46 katika Wilaya yetu ya Kilolo. Hata hivyo, wananchi zaidi ya 246 wameweza kufaidika na miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kilolo bado vijiji 20 havijapata maji. Kwa hiyo, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri, hivi vijiji 20 viweze kufikiwa na miradi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao ujenzi wa miradi ya maji inayoendelea kutekelezwa. Mradi wa Maji wa Kihesa Mgagao, Masege na Masalali, huu mradi umeshafika zaidi ya 80%, lakini mkandarasi anadai shilingi bilioni 1.2. Kwa hiyo, tunaomba Mkandarasi alipwe ili huu mradi uweze kusaidia wananchi kwa vijiji vilivyobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, upo mradi ule wa Ng'ang'ange ambao Naibu Waziri alikuja pamoja na Makamu Mwenyekiti wakati huo Mheshimiwa Anna Lupembe, wakasaini huu mradi. Sasa mwaka mzima bado wananchi hawajapa maji. Kwa hiyo, tunaomba huu mradi pia ukamilike ili wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mradi wa Kisima, ule tumeuita Injinia Mwajuma kwa sababu ni mradi ambao tulipewa wakati wa Siku ya Wanawake, bado tu usambazaji. Tunaomba Injinia Mwajuma aje sasa kwenye ule mradi ili maji yaweze kusambazwa, wananchi waweze kupata maji. Tunao mradi mwingine wa Ikula. Hii ni *tank* tu, shilingi milioni 200 tu wakipewa wananchi wa Ikula watapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao pia mradi wa kuboresha maji katika Mji Mdogo wa Kilolo, gharama yake ni shilingi milioni 800, na huu mradi umeshafikia 95%. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali, tunaomba tu waweze kutupatia fedha ili mradi uweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunao mradi wa kuboresha maji Mji Mdogo wa Ilula. Huu ni mradi wa shilingi bilioni 1.3, na 70% tayari. Kwa hiyo, tunaipongeza Serikali kwa kazi nzuri, lakini tunaomba miradi hii sasa ikamilike kwa wakati ili wananchi sasa waweze kufaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, kwa kuwa miradi hii imesimama kutokana na wakandarasi kutolipwa vyema, tunaomba sasa Serikali ifanye utaratibu, Wizara ya Maji iongezewe fedha ya kutosha na pia tuangalie na vyanzo vingine ili wananchi wote waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Martha hapa amesema maji ni kila kitu. Kila kitu kinahitaji maji. Kwa hiyo, tunaomba Serikali iangalie Wizara ya Maji, fedha zote zinazotengwa zipelekwe kwa wakati ili miradi iweze kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti hata hivyo, tunaomba tuongeze nguvu kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji, kwa sababu vimeharibiwa sana. Hivi vyanzo tusipovitunza, basi hatutapata maji ya uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilolo *IRUWASA* gari ni shida, barabara hazipitiki, wananchi hawafikiwi, miradi haikaguliwi kwa sababu hawana maji. Tunaomba gari katika Wilaya ya Kilolo, *IRUWASA* waweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeweza kushika shilingi, lakini ninawapenda sana wake wa Mheshimiwa Waziri, tena wote ni rafiki zangu, siwezi kuchukua mshahara wake, kwa sababu kwanza anafanya kazi nzuri sana. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa...

**MBUNGE FULANI:** Unawapenda wake zake? *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Ndiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitachukua mshahara, ila ninakuomba miradi ambayo tayari wakandarasi wpo, walipwe ili miradi iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na Mwenyezi Mungu awabariki, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kabati ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, atafuatiwa na Mheshimiwa Aysharose Mattembe, na Mheshimiwa Charles Mhando Njama ajiandae.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi ya kuweza kuchangia Wizara hii ya Maji, na pia ninatoa shukrani kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miradi mikubwa ambayo anatupatia sisi watu wa Jimbo la Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, watumishi wote wa Wizara ya Maji na pia watumishi wote ngazi ya Mkoa wetu wa Arusha na pia katika Jimbo langu la Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametembelea Jimbo la Karatu mara nyingi na Naibu Waziri na changamoto kubwa katika Mji wa Karatu katika eneo la Mjini, Mamlaka ya Mji wa Karatu, Mheshimiwa Waziri anajua. Kuna bwawa pale linasumbua na kwenye lile bwawa kuna visima vitatu, ikifika kipindi cha masika tunapata changamoto kubwa sana ya wananchi wa Jimbo la Karatu katika Mji wa Karatu kukosa maji. Hilo Waziri na Naibu Waziri ni mashahidi, na pia Katibu Mkuu ni shahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa visima vitatu vilivyopo katika eneo la bwawa lile la mjini, limepata changamoto tena kubwa. Sasa ombi langu ni nini kwenu ninyi Waziri na Naibu Waziri?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuja kuchimba visima vitatu, na kutokana na jiografia ya hali halisi ya Jimbo lile katika

eneo la mjini, visima vile vitatu vimeonyesha vina maji lita 200,000 kwa saa na inaweza kupeleka kupunguza changamoto ya maji kutoka 52% kwenda 89%, mkitupatia fedha shilingi bilioni 2.7% na hilo mkifanikisha kwa maji, tunapanda kutoka 52% katika Mji wa Karatu kwenda 89% katika eneo la Mji wa Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo ni ombi kubwa la wananchi wa Jimbo la Karatu, na Waziri ni shahidi, na Wizara imetusaidia kuchimba mitaro ili kuokoa bwawa lile lisiendelee kuathiri wananchi wa eneo la mjini, na pia kuathiri nyumba za watu katika katika Mji wa Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwa kupitia wananchi wa Jimbo la Karatu, mtupatie shilingi bilioni 2.7. Mheshimiwa Waziri ni shahidi, mwaka 2022 tuliweza kukaa vikao katika Jimbo la Karatu, alisema atatoa shilingi bilioni 4.5, hakufanikisha lile zoezi la shilingi bilioni 4.5. Akitoa shilingi bilioni 2.7 itakuwa imefikia azma ya wananchi wa Jimbo la Karatu kupata maji kwa 89% na atakuwa ametimiza ahadi yake ya mwaka 2022 kwa wananchi wa Jimbo la Karatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya upande wa vijijini *RUWASA,* upatikanaji wa maji katika Jimbo la Karatu ni 82%, tunaishukuru Serikali lakini tuna ombi. Kuna wakandarasi ambao tayari wako kazini, wameomba fedha na wameandika *certificate*. Kwa mfano, kuna Kijiji kimoja kinaitwa Qorong'aida ambacho mkandarasi ameomba shilingi milioni 176. Pia, kuna Kijiji kinaitwa Mangisa - Jobaj ambacho mkandarasi ameomba shilingi milioni 255; kuna Kijiji cha Mang'ola Juu, mkandarasi ameomba shilingi milioni 85; na Kijiji cha Matala Endanyawet mkandarasi ameomba shilingi milioni 510. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna changamoto katika Tarafa ya Mbulumbulu vijiji vinne na *RUWASA* imejaribu kuchimba maji katika Kijiji cha Slahhamo imeshindwa kupata maji. Imechimba maji katika Kijiji cha *Upper Kitete* imeshindwa kupata maji katika vijiji vile; na kuna Kijiji kingine hiki cha Kitete, na Kijiji kingine cha Lositete. Ukanda huu ni mwambao ambao unaendana na ukanda wa Mto wa Mbu ambao uko juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wizara ione namna ipi nzuri sasa ya wananchi wale wa vijiji vinne ambavyo viko kwenye Tarafa ya Mbulumbulu Kata ya Mbulumbulu ambavyo vina changamoto kubwa, na Wizara imechimba mara kadhaa na maji yamekosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na niseme kwamba, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Karatu tunaomba, haya ni maombi yao ambayo nimeyawasilisha mbele yako Seriksli iyazingatie kupitia Wizara, itupe ridhaa ya kutangaza sasa, miradi hii ya shilingi bilioni 2.7, Wizara itoe kibali cha kutangaza katika mji wa Karatu ili wananchi wa Mji wa Karatu waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninashukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa kututunzia muda. Ninamwita sasa Mheshimiwa Aysharose Ndogholi Mattembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Charles Mhando Njama, Mheshimiwa Godfrey Mbuga, ajiandae.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii muhimu ya Bajeti ya Maji. Nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kibali cha kusimama katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, Naibu wake, Mheshimiwa *Eng.* Kundo na Katibu Mkuu kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuhakikisha wananchi wanapata majisafi na salama. Ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitumie nafasi hii kuwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Singida kwa kunichagua kwa kura nyingi na kuniwezesha kurudi tena Bungeni. Ninaomba niwahakikishie wanawake wa Mkoa wa Singida, nitawatumikia

kwa nguvu zangu zote na moyo wangu wote, kuhakikisha Singida inapaa kwa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye ni kinara namba moja wa kumtua ndoo mwanamke kichwani na kwa mageuzi makubwa aliyoyafanya katika Wizara hii ya kuhakikisha wananchi wanapata majisafi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, ninaomba sasa nijielekeze moja kwa moja kwenye mchango wangu. Nianze na gridi ya Maji ya Taifa. Ninaipongeza sana Serikali kwa kuja na mpango mkakati huu wa kumtua ndoo mwanamke kichwani kwa kutumia vyanzo vya maji vya maziwa na mito kuhakikisha changamoto ya maji inamalizika kabisa nchini. Ninaipongeza sana Serikali. Ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wangu wa Singida, Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria umeshafika katika Mji wa Shelui. Ninaiomba sana Serikali, usanifu unaoendelea katika mradi huu wa Ziwa Victoria, uzingatie mahitaji yote kwa wananchi wa Mkoa wa Singida, kwa kuwa endapo mradi huu utakamilika, nina hakika kabisa wananchi wa Mkoa wa Singida watapata majisafi na salama kwa uhakika. Kwa hiyo, ninaomba hilo lichukuliwe kwa jicho la tatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni suala la Mradi wa Maji wa Miji 28. Katika Mkoa wangu wa Singida, Mradi huu unatekelezwa Kiomboi, unatekelezwa Singida, na unatekelezwa pia Manyoni. Ninashukuru sana kwa Manyoni mradi huu umefikia 80%, lakini kwa Mradi wa Mji wa Singida na Mji wa Kiomboi, kwa kweli bado kuna changamoto. Ninaomba sana, Mheshimiwa Waziri ni msikivu, mradi huu sasa uweze kukamilika, kwa kuwa miji hii ya Kiomboi, Singida na Manyoni inakua kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ningependa kulichangia ni uhaba wa vitendea kazi. Jiografia ya Singida ni

kubwa sana. Ninaomba sasa watendaji wetu wa *RUWASA* waweze kupata magari. Wanatembea na pikipiki, umbali ni mrefu kutoka kijiji kimoja kwenda kijiji kingine, ili sasa miradi hii iweze kukaguliwa kwa kina na iweze kufanyika kwa uhakika, ni lazima magari yawepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya kama Ikungi, Wilaya ya Singida Vijijini, pamoja na Manyoni hawana kabisa magari. Ninaomba katika bajeti hii tuliyotengewa, magari yaweze kupatikana ili kazi hizi ziweze kufanyika kwa uhakika kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia ni kuishukuru sana Serikali kwa miradi ambayo tumeipata, na miradi hii imetumia zaidi ya shilingi bilioni 10. Mradi wa Maji Tulya, Mwangeza, Msingi, Makuro, Mpambaa, Kinangali na miradi wa maji wa vijiji 11 wa Kintinku, Lusilile lakini ipo miradi ambayo imekamilika, na miradi mingine haijakamilika na ukiuliza ni kwa nini miradi hii haijakamilika? Unaambiwa wakandarasi hawajalipwa madeni yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na Waheshimiwa Wabunge wote kwamba Wizara hii iongezewe bajeti ili sasa wakandarasi wetu waweze kulipwa madeni yao na miradi hii iweze kukamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwapongeza sana watendaji wa *RUWASA* wa Mkoa wa Singida wakiongozwa na kaka yangu Said kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya katika Mkoa wangu wa Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Ninamwita Mheshimiwa Charles Mhando Njama, atafuata Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga, na Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela ajiandae

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kulipa nafasi. Awali ya yote nianze kwa kuipongeze sana Serikali chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo imeendelea kukamilisha adhima yake ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sisi watu wa Korogwe Mjini tunayo miradi miwili mikubwa ya maji. Tunao Mradi wa Miji 28, ambapo mradi huu ni tegemeo kubwa na tumaini lililojaa kwa wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini kwamba sasa tunakwenda kusahau changamoto ya maji Korogwe Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tunao mradi wa Ndemaha. Mradi huu nao utakwenda kutusaidia kuongeza wingi wa maji katika Jimbo letu. Pamoja na miradi hii miwili, tunafahamu kumekuwa na changamoto kwa kiasi, hasa katika mradi wetu wa Miji 28 kwa kuwa tulitazamia kupata maji katika Jimbo letu la Korogwe na kuanza kuyapokea mwezi wa Nne, lakini katika ufuatiliaji inaonekana tutayapata mwezi wa Saba. Bado tuna matumaini makubwa, kwamba mradi huu utakamilika na tutapata maji haya kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wetu wa Mto Ndemaha, bado unasuasua sana. Ninamwomba kaka yangu Waziri Aweso atusaidie, twende tukaukamilishe mradi huu ili kuhakikisha kwamba maeneo yote ya Jimbo la Korogwe Mjini, katika kata zetu zote 11, tuna uhakika wa kupata maji yanayotosha, ambayo ni safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Jimbo la Korogwe Mjini tuna wasiwasi. Pamoja na miradi hii mikubwa, ambayo tuna uhakika ikikamilika tutapata maji takribani *cubic meter* za ujazo milioni 16 ambapo ukilinganisha na uhitaji wetu wa sasa wa milioni saba, tutakuwa na ziada ya takribani lita milioni tisa ambazo tunaamini hatutakuwa na changamoto ya maji ndani ya miaka 25 hadi 30 ijayo katika Jimbo letu la Korogwe Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, changamoto ambayo tunaiona mbele yetu ni wasiwasi wa kuwepo kwa upotevu wa

maji baada ya maji haya kukamilika kufika katika Jimbo letu la Korogwe Mjini. Hii ni kwa sababu, miundombinu ya maji tuliyokuwa nayo katika Jimbo la Korogwe Mjini, mingi ni chakavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu Wizara inao mpango wa kwenda kurekebisha miundombinu ile ili kuhakikisha kwamba upotevu wa maji tunaukabili iwezekanavyo. Ninamsihi Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake, tukaweke kipaumbele katika kukarabati miundombinu hii, ili maji yatakapofika hasa haya ya miji 28, tusiwe na upotevu wa maji katika eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ile nia ya maji kufika kwa wananchi iweze kukamilika. Tusije tukawa tuna maji mengi lakini wananchi wanashindwa kupata maji kwa sababu ya miundombinu ambayo imekuwa chakavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongelea upotevu wa maji katika ujumla wake kama nchi, ninaona kama tunayo fursa kubwa ya kwenda kuimarisha huduma ya maji katika jamii. Takwimu zinaonesha kwamba takribani 35% ya maji yanapotea, ukiya-*quantify* katika fedha, ni takribani shilingi bilioni 240. Ukiangalia bajeti yetu ya mwaka huu, ambayo ni shilingi trilioni 1.12, kiasi hiki kinachopotea, ni karibia 22% ya bajeti ambayo tunaenda kuipitisha mwaka huu. Maana yake ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hatuwezi kurudisha gharama za uzalishaji wa maji ambazo tunazitumia. Ukiangalia kwa hii 35% inayoongelewa ya upotevu, kama ni sahihi, maana yake ni kwamba katika kila shilingi 100 ambayo unaitumia kuzalishia maji, shilingi 35 zinapotea njiani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiweza kwenda kukabiliana vizuri na changamoto ya upotevu wa maji, tunao uwezo wa kuipunguzia Serikali mzigo wa kuendelea kuingiza fedha katika bajeti hii, na Wizara hii ikawa na vyanzo vya kuweza kuisaidia ku-*fund* bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, na nimeona namna ambavyo amekuwa mkali katika eneo hili la upotevu wa maji, na ameleta *transformation* nyingi katika Wizara hii ya maji, ninaamini na hili tunao uwezo wa kwenda kulikabili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja, na ninakushukuru tena kwa nafasi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ninamwita Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga, atafuata Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela, Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, ajiandae.

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi hii. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema zake na rehema zake. Baada ya kumshukuru Mungu, niipongeze na kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa fedha nyingi ambazo zimekuja kwenye Jimbo la Kisesa na kwa miradi yote ambayo inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisesa tumepata shilingi bilioni 6.9, ambayo ni kwa ajili ya miradi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Mradi wa Inonelwa ambao una shilingi bilioni tano, na Mradi wa Mwashata ambao una shilingi bilioni moja, na Mradi wa Mbalagane, Semu ambao una shilingi milioni 592. Miradi hii yote, mingine inaendelea na mingine imeshakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninashukuru sana kwa juhudi za Serikali, na ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Aweso pamoja na Mheshimiwa *Eng.* Kundo na Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, dada yetu Mwajuma, lakini pia ninawapongeza *RM* wa Simiyu Lufwetula pamoja na *DM* wa Meatu, ndugu yangu David Kaijage kwa kazi nzuri na kubwa ambayo wanaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninapitia hii bajeti, nimevutiwa sana na jinsi ambavyo wameiweka kwamba asilimia saba inaenda kwenye matumizi ya kawaida na 93% inaenda

kwenye maendeleo. Maana yake 93% inaenda kumtua mama ndoo kichwani, Wizara ya Maji hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nimepata wasiwasi sehemu moja. Ukiangalia kwenye fedha za maendeleo shilingi 1,039,000,000, *financing structure* yake ni 38.5% tu ndiyo ambayo inatoka kwenye fedha za ndani. Inanipa mashaka kidogo, na 61.4% ni fedha za nje. Ukiangalia Kamati wameelezea pia hiki kitu. Ninapata wasiwasi namna ambavyo hii miradi mikubwa ambayo tunategemea itekelezwe, kama kweli itaenda kutekelezwa kwa kiwango hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, atakapokuja kwenye majumuisho, atoe ufafanuzi vizuri. Je, 38.5% ya mapato ya ndani peke yake ndiyo yanayoenda kwenye utekelezaji wa miradi. Kweli tutatoboa? Kama anavyosema kwamba wali wa kushiba unaonekana kwenye sahani, kwa wali huu, mimi ninaona hatushibi. Kwa hiyo, kuna haja ya kutazama vizuri kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia imeonesha kwamba upatikanaji wa fedha hizi ni 74.3%. Sasa ninajiuliza kama 38% kwa 61% na bado upatikanaji ni 74.3%, kwa hiyo, kuna maeneo ambayo yanatupa mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Wizara ya Fedha, kwanza ninaunga mkono hii bajeti. Pamoja na kuunga mkono, nishauri kwamba, ni vizuri wakandarasi wapewe kipaumbele, madeni ya wakandarasi yapewe kipaumbele ili waweze kurudi *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo miradi Kisesa ambayo imesimama kwa sababu wakandarasi wanadai. Upo mradi wa Mwashata, mkandarasi anadai shilingi milioni 234. Upo mradi wa Mwasengela, Lingeka pamoja na Mwakasumbi, mkandarasi anadai shilingi milioni 114. Ninaomba, baada ya hii bajeti kuwa tumeipitisha, kipaumbele cha kwanza tunaomba wakandarasi wakalipwe madeni yao ili hii miradi iweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Mheshimiwa Rais amenunua mitambo kwa kila mkoa kwa ajili ya kuchimba visima, lakini ninaona *speed* haiendani na shauku ya Mheshimiwa Rais. Kwa mfano, kwenye Jimbo langu la Kisesa, tangu hii mitambo imekuja, ni visima vitano tu ndivyo ambavyo vimechimbwa, kati ya hivyo vitano, ni vitatu tu ndivyo ambavyo vinatoa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara iunde Kamati, au iunde Kitengo cha *Evaluation*, ili kuweza kufanya tathmini, lakini mwisho nimalizie kwa kusema, Mradi wa Ziwa Victoria ndiyo ambao utatusaidia kwa Meatu na Kisesa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Khalid Mussa Nsekela; Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, na Mheshimiwa Patrick Mwalunenge wajiandae

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii niweze kuchangia hoja ambayo iko Mezani. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Rais na kumpongeza kwa kazi kubwa na juhudi za makusudi za kumtua ndoo mama kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitoe pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri na timu nzima ya Wizara ya Maji kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya, lakini kwa wasilisho zuri sana la bajeti ambayo siyo tu kwamba inaonesha namba kwenye jedwali, lakini ni bajeti ambayo inaakisi maono ya Mheshimiwa Rais na Dira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri na kuisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri. Ukiangalia hii bajeti ya Wizara ya Maji ni bajeti ambayo inamgusa kabisa mwanamama ambaye anatembea kilometa zaidi ya tano kufuata maji saa 11 asubuhi. Pia ni bajeti ambayo inamhusu kabisa mwanafunzi ambaye anakosa masomo akiwa kwenye harakati za kwenda kuchota maji. Vilevile, ni bajeti ambayo inamhusu mkulima na mfugaji

ambaye anategemea majisafi na salama na wingi wa maji katika uzalishaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti ukiangalia takwimu za Tanzania kutoka *World Bank,* ni kwamba tume-*improve* sana katika suala la kupata majisafi na salama. Ni 30% mpaka 40% ya wananchi wana majisafi na salama, 70% mpaka 85% wana maji ya msingi, lakini kwenye takwimu hizi kwa mimi ambaye ninatokea Kyerwa, bado ninakuwa na ugomvi nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru kwa kazi kubwa inayofanyika. Kuna miradi ambayo inagusa vijiji 21 na nimeona kwenye bajeti fedha zimetengwa, ambazo zitaenda kukamilisha miradi hii. Ukiangalia idadi kubwa ya Vijiji vya Kyerwa bado tunategemea maji ya visima, maji ya chemchem na maji ya mvua ambayo hayana uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninaomba nitoe rai kwamba, bajeti tumeiona, lakini tunaomba fedha hizi zitoke mapema. Nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba, mafanikio ambayo anataka ayaone, na nimeona jitihada zake zilivyo, ni mafanikio ambayo yatakuwa na maana pale yatakapokuwa yamemgusa mwananchi wa kawaida, hasa mwananchi wa kijijini, vikiwemo Vijiji vya Kyerwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili ninaomba nitoe rai kwamba, vile vyombo vya watumia maji vya vijijini vijengewe uwezo, vipewe nguvu na viwajibishwe katika kukusanya mapato na kusimamia miradi. Hapa ninaomba kidogo Mheshimiwa Waziri aniazime masikio yake kwa sababu, kuna siku niliuliza swali la Mradiwa Kigorogoro, Rulamana Kashandana Mheshimiwa Naibu Waziri akanipa majibu kidogo, ambayo sikuridhika nayo, lakini nikaona nifanye kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetembelea mradi ambao uko Kigorogoro, Kata ya Kibale, ule mradi umejengwa 2009. Ule mradi uko kilometa tano kutoka makazi ya watu, uko msituni, lakini tenki la maji limejengwa kilometa 12 kutoka kisima kilipochimbwa. Sasa unaweza ukaona kwamba, tayari usalama wa mradi ni shida kwa

sababu, uko msituni, lakini una gharama kubwa ambayo inatumika ku-*pump* maji kilometa 12 kutoka kwenye kisima kuja kwenye tenki la maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kibale, Kigorogoro, Rulama na Kashanda wameji-*commit*. Nimeongea nao wanasema wao hawakushiriki kuharibu mradi, kama ilivyojulikana toka mwanzo, na mimi kwa niaba yao ninaomba, sasa wameahidi kwamba, wako tayari, wanaomba Serikali sikivu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iwapelekee mradi wa maji kwa sababu, miaka mingi hawana majisafi wala hata maji ya msingi hakuna. Kwa hiyo, wanaomba, na wako tayari kutoa ushirikiano wa kutosha wakipata kisima cha maji pale kwenye Kata ya Kibale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba nitoe rai kwamba, ni muda mwafaka sasa, wakati Wizara ya Maji inafanya kazi kubwa kusambaza majisafi na salama kwa wananchi, na kuna haja ya ushirikiano mkubwa sana na Wizara ya Nishati, nikimaanisha *TANESCO,* kwamba, wasambaze umeme pale pote kwenye miradi ambapo inapelekwa kwa sababu, ukienda Jimbo la Kyerwa, miradi mingi ipo sehemu, hakuna umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Serikali inaingia gharama kubwa sana kwenda kuvuta yale maji kwa kutumia sola. Kama hakuna mvua, maji hakuna, kwa sababu, changamoto nyingi ambazo zinatokea kwenye shida ya maji ni uhakika wa maji. Miradi ipo, lakini uhakika hamna, umeme hamna, sola ina shida, mvua imenyesha, watu hawana huduma ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mwisho kabisa, kuna Mradi wa Kuvuta Maji kutoka Mto Kagera ambao unakwenda kugusa Kata ya Nyaruzumbura, Kyerwa, Nyakatuntu, Businde, Bugarana Kamuli, ambao utahudumia vijiji 21. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri, hili suala la wanakijiji wa Kyerwa au Kyerwa kwa ujumla watashukuru watakapoona kuna jitihada za msingi zinafanyika ili mradi huu uweze kukamilika. Ninashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila, Mheshimiwa Patrick Mwalunenge na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, ajiandae.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwanafasihii. Kwanza kabisa, ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mawaziri wa Wizara ya Maji kwa miradi ambayo imetekelezwa katika Jimbo la Msalala, yenye thamani ya shilingi bilioni 32.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli wananchi wa Msalala wanampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa fedha hizi nyingi ambazo ametuletea jimboni kwetu. Mheshimiwa Waziri amekuja na Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni, tukawaambia tunayo miradi yetu ambayo bado haijakamilika. Mradi wa Nduku, Busangi, ambao unatakiwa utoke Nduku, Busangi, ufike Ntobo, makao makuu ya halmashauri. Tunaomba mradi huu uweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mradi wa Mangwi, Ilogi, ambao unatakiwa utoke Mangwi, Ilogi, ufike Lunguya. Wananchi wa Lunguya wanausubiria sana mradi huu uweze kukamilika. Tunao mradi wa Mwamboku, Magongwa, ambao haujawahi hata kuanza, lakini wananchi wanausubiria kwa hamu sana, ili uweze kutatua kero ya maji katika Kata ya Kashishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mradi wa Vijiji 21, ambao huu unakwenda kugusa kata tisa. Kata tano ni ambazo zina vyanzo vya maji ya visima virefu, ambapo tayari visima virefu vipo. Kwa hiyo, ni ukamilishaji tu wa usambazaji wa maji katika visima hivyo. Unazungumzia Kata ya Ikinda, Kata ya Shilela, Segese, Mega na Chela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi ambao, pamoja na kimya cha Mheshimiwa Waziri cha kukamilisha mradi ule ambao ulianza, sisi katika Jimbo la Msalala bomba la Ziwa Victoria limepita kwenye jimbo letu. Tunavyo vijiji tisa ambavyo vinapitiwa na bomba la Ziwa Victoria, ambapo mradi huu unagusa kata nne; Kata ya Mwalugulu katika Kijiji cha Sungamile, Kata ya

Mwakata, Kata ya Isakajano, Vijiji vya Matinje na pia, unagusa Mradi ambao unatakiwa ukamilike wa vijiji viwili ambavyo viko kwenye Kata ya Isakajana, ambavyo ni Jana yenyewe pamoja na Butondolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Msalala, Serikali ikikamilisha Mradi huu wa Vijiji 21 unakwenda kuwa na vijiji 75 kati ya vijiji 92 vya Jimbo la Msalala. Kwa kweli, atakuwa ametusaidia sana katika jitihada za kumtua ndoo mama kichwani. Miradi yetu hii mingi ni ya kufikisha maji kijijini. Gharama za kuvuta maji kufikisha majumbani bado ni gharama kubwa sana. *CBWSOs* zetu tayari zinafanya vizuri sana kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi baada ya kutufikishia maji haya kwa kiwango hiki, kuanzia mwezi wa Saba mpaka leo hii, kaya 428 zimeshaunganishwa maji, lakini bado gharama ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuombe *CBWSOs* zetu ziendelee kutekeleza miradi midogo midogo ya kusogeza maji kwa wananchi, ili gharama ya kuvuta maji kutoka kwenye bomba kufikisha kwenye kaya za wananchi wetu ipungue na hiyo ndiyo maana halisi ya kumtua ndoo mama kichwani. Badala ya kwenda kuchota maji kwenye *DP* na kuleta nyumbani, tunataka wananchi wetu wachote maji majumbabi mwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao Mradi wa gridi ya Maji ambao tunasema, tutatoa maji Ziwa Victoria, lakini tunayo mikoa ambayo hata ukichimba maji chini unakutana na chumvi. Upi mpango wa Wizara wa kuvuna maji ya mvua ya kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunao Mradi wa Lita za Ujazo Milioni Nane ambao ni wa Bwawa la Maji ya Mvua ulioachwa na Buzwagi, pale Kahama. Tunapeleka maji yale kwenye tenki letu la maji, pale shule.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana na ninaomba kuunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru. Nilimwita Mheshimiwa Patrick Adkin Mwalunenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza, na Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, ajiandae.

**MHE. PATRICK A. MWALUNENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia Bajeti yetu pendwa ya Wizara ya Maji. Kwanza, kabisa ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya dhati ya kumtua mama ndoo kichwani na amejipambanua wazi kwa kutenga bajeti kubwa, kuiwezesha Wizara ya Maji, shilingi trilioni moja na kitu, dhamira yake ni njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niko Jimbo la Mbeya Mjini. Mheshimiwa Waziri anafahamu Jimbo la Mbeya Mjini, kwa maana ya Jiji la Mbeya. Tuna changamoto ya maji, lakini tunaamini ule Mradi wa Kiwira utakuwa ndiyo *solution,* kwa sababu, una uwezo wa kutoa lita zaidi ya milioni 117. Zaidi ya watu milioni 1.5 wataweza kunufaika na ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwahiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, apelike *speed* ule mradi ukamilike ili watu wa Mbeya Mjini na wilaya nyingine waweze kunufaika. Tumezungumza mara nyingi changamoto za pale na amenihakikishia kwamba, ataziondoa ili ule mradi aweze kuendelea, na watu wetu wapate maji. Kwahiyo, ninamwomba sana ndugu yangu Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema wazi, katika biashara rahisi kuifanya duniani ni biashara ya maji. Sasa sielewi tunakwama wapi? Hata tuki-*involve private sectors*. Ninashukuru, kwenye hotuba wamesema kwamba, sasa tutazi-*involve private sectors* na *financial institutions* ku-facilitate hii miradi ya maji. Hilo ni jambo bora, nina uhakika tunaenda kufanya mapinduzi makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalia kampuni ngapi zinazalisha maji ya kunywa? Ni lita na lita zinapita kwa malori na malori. Hawawezi kushindwa wale watu. Kama tutawawekea mazingira mazuri ya kufanya miradi mikubwa ya maji, tutaipunguzia Serikali kazi nzito ya kutafuta fedha na hasa kwenye miji mikubwa, ibaki kuhangaika kutafuta pesa kwa ajili ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri na majiji ambayo yana uwezo wa mapato, tuangalie namna nyingine ya kuhakikisha kwamba hawa watu wanakuwa *financed* na *private sectors* na benki, ili tuweze kutatua miradi ya maji. Kuanzia jana wachangiaji wote wanaona kwamba, maji yana umuhimu, kila Mbunge, lakini ninaona shida mnayoipata ni upatikanaji wa fedha na dhamira ya Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu wake na watendaji wote, nikiwaangalia usoni na mioyo yao ni kuhakikisha kwamba, wanamtua mama ndoo kichwani. Tatizo liko kwenye upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni kwamba, kwanza waanze kubana matumizi. Nimeona kwenye bajeti yao, sehemu kubwa ya fedha inaenda kwenye miradi, waendelee hivyo hivyo. Pia, waendelee kubana zaidi matumizi ili fedha iende kwenye miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua Waziri wa Fedha yuko hapa, Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuwa Waziri wa Fedha, anafahamu ni kiasi gani cha fedha kinatumika kwenye kununua magari kwa watumishi wa umma. Hebu tujibane kama Serikali, angalau kwa miaka miwili. Hakuna mtumishi wa umma atakayeugua kwa kukosa gari jipya, lakini watu wataumwa kwa kukosa maji. Tuangalie ni kiasi gani cha fedha kinatumika kununua magari mapya kila mwaka, ile fedha tuipeleke kwenye miradi ya maji, tuisaidie Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako wawekezaji mbalimbali wanakuja kuwekeza kwenye nchi yetu, wanakuja kuwekeza kwenye migodi na biashara kubwa. Tuwabane wale iwe kama sehemu ya *condition,* wanapokuja kuwekeza hapa, basi wawekeze pia kwenye miradi ya maji, iwe kama, sehemu ya

kutoa *CSR* kwenye jamii yetu. Nina uhakika tutaisaidia Wizara yetu na maeneo mengi yatapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mji wa Chunya unazalisha dhahabu pale, lakini maji hakuna. Ni jambo la kusikitisha sana. Kwa hiyo, tuangalie *mechanism* nzima, kama Serikali, kuangalia ni jinsi gani tunaisaidia Wizara ya Maji iweze kupata fedha na kuweza kuhudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na miamala ya simu. Ni kweli kabisa inatusaidia na kila mtu hapa akiamka asubuhi, akinawa uso, amepiga mswaki na maji, anakwenda kwenye simu, kununua vocha ya shilingi 500 au shilingi 1,000, na kwenyewe tuangalie ni shilingi ngapi miamala, inaweza ikachangia kuleta fedha kwenye Mfuko wetu wa Maji ili Wizara ya Maji iweze kupata fedha na kutekeleza miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri hapa amesoma hotuba, ni nzuri na ina matumaini makubwa sana kwa wananchi, lakini bila fedha hawezi kutekeleza ile miradi. Ninatamani kuona Bajeti ijayo mwakani, asiyongee tena habari ya miradi ambayo haijakamilika; Bwawa la Kidunda, Bwawa la Kiwira, kutoa maji kwenye gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Ninaunga mkono hoja, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Juliana Daniel Shonza. Mheshimiwa Lucy Mayenga atafuatia na Mheshimiwa Flatern Mdaku, ajiandae.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi, ili niweze kutoa mchango wangu kwenye Wizara ya Maji. Ninampongeza sana Mheshimiwa Aweso kwa kazi nzuri ambayo anaifanya. Ninaamini ameona kila Mbunge alivyosimama hapa ametambua namna ambavyo amekuwa kijana mchapakazi na msikivu. Kwa hiyo, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Waziri anafungua hotuba yake, amegusia Mradi wa Maji wa Mto Momba na ninajua, hata nilivyosimama hapa, Mheshimiwa Waziri anajua kabisa kwamba, ninazungumzia Mradi wa Mto Momba. Yapo mambo mengi sana ambayo Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Sita, Mama yetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameyafanya ndani ya Mkoa wa Songwe na ametuandikia historia kubwa, ambayo kwa kweli, haitakaa ije ifutike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo kubwa mojawapo ambalo Mheshimiwa Rais ametufanyia ni kutuletea Mradi wa Maji wa Mto Momba. Mradi huo ni mkubwa sana na ni mradi wa kimkakati. Mkoa wa Songwe tumekuwa tunaiomba sana Serikali kuweza kupata mradi wa kimkakati. Mradi huo una thamani ya shilingi bilioni 119 na sisi kama Wabunge wa Mkoa wa Songwe tuna imani kwamba, mradi huo utakapokamilika, kwa kiasi kikubwa sana utasaidia kuweza kumaliza changamoto kubwa ya maji inayowakumba wanawake wenzangu wa Mji wa Tunduma, inayowakumba wanawake wenzangu wa Mji wa Vwawa na inayowakumba wanawake wenzangu wa Mji wa Mlowo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu umesainiwa mwezi wa Tatu mwaka 2025. Ninakiri kwamba, huu mradi umetusaidia sana hata kwenye kutafuta kura za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na hata ushindi mkubwa ambao ameupata ndani ya Mkoa wa Songwe ni kutokana na ahadi ya umaliziaji wa mradi huu wa Mto Momba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miezi 13 sasa imepita tangu mradi huo uweze kusainiwa. Kwa bahati nzuri siku ya kusaini Mheshimiwa Aweso ulikuja na Waziri wa Fedha, ambaye sasa hivi ndiye Mtendaji Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kwamba, Mheshimiwa Waziri ameona namna ambavyo wanawake wamehamasika na ambavyo wameufurahia huu mradi. Imepita miezi 13 sasa na hivi ninavyoongea imebaki miezi 15 tu mradi unatakiwa uweze kukamilika, lakini mpaka sasa hali ya kule *site* kwa kweli, bado hairidhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua Mheshimiwa Aweso ni mfuatiliaji, na anajua kinachoendelea kule Songwe. Mpaka sasa hivi, kwenye yale makubaliano, mkandarasi alipaswa apewe malipo ya awali, shilingi bilioni 15, lakini mpaka sasa amepokea shilingi bilioni 5.9 pekee yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwa *nature* ya mradi jinsi ulivyo mkubwa ni wazi kwamba, shilingi bilioni 5.9 zitaishia tu kwenye kufanya yale maandalizi ya awali. Bado mradi hautaweza kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Mheshimiwa Aweso, amefanya mambo makubwa na sisi wananchi wa Mkoa wa Songwe tumesikia miradi mbalimbali ambayo imetekelezwa. Mradi wa Kidunda wa kutoa maji kwenye Ziwa Victoria na Mbunge mwenzangu hapo amesimama, amesema sasa hivi mradi umefika Singida na sisi wananchi wa Mkoa wa Songwe tunakuomba sana, tunaiomba sana Serikali iweze kutilia mkazo kwenye kuhakikisha kwamba, mradi wa kutoa maji Mto Momba unakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa changamoto ni fedha, mimi ninaiomba Serikali, kwanza, iongeze *speed* ya kutoa fedha kwenye mradi ili mkandarasi asisimame na wananchi waone kwamba, mradi unaanza kutekelezwa. La pili, tunafahamu dhamira ya Serikali ni kutekeleza mradi huu kwa kutumia mapato ya ndani, siyo jambo baya, lakini pia, tumeona miradi mingi ya kimkakati, ambayo Serikali imeitekeleza kwa kutafuta mikopo yenye masharti nafuu. Kama inawezekana, Serikali iangalie uwezekano wa kutafuta mkopo nafuu kwa sababu, kwa miezi 15 iliyobaki siyoni uwezekano wa huu mradi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo zuri sana ambalo Mheshimiwa Waziri ameliongelea kwenye hotuba yake, amesema kwamba, wana mpango sasa hivi wa kuanzisha *water body*. Hili ni jambo jema na linaonesha namna gani ambavyo Wizara hii imekaliwa na Waziri, ambaye ni mbunifu. Kila siku anaumiza kichwa kuhakikisha kwamba, tunamaliza changamoto za maji. Kwa hiyo, ninaomba Mheshimiwa Waziri atakapoanzisha huo

mkakati wa *water body,* kwa sababu amesema ni mpango ambao lengo lake ni kumaliza ile miradi ya kimkakati, kipaumbele namba moja ninaomba sana asiusahau mradi wa kutoa maji kwenye Mto Momba.

*(Hapa, kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho…

**MWENYEKITI:** Hakuna la mwisho Mheshimiwa, malizia.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo miradi 24 ndani ya Mkoa wa Songwe. Tunaomba iweze kukamilika kabla hamjatuletea miradi mingine, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa ninamwita Mheshimiwa Lucy Thomas Mayenga, atafuatiwa na Mecktridis Fratern Mdaku. Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete ajiandae.

*(Hapa microphone iligoma kuwaka)*

**MWENYEKITI:** Hamia kwa Mheshimiwa Sitta hapo.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kutoa mchango wangu. Kwanza kabisa, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kusimama leo hapa kuweza kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuweza kunipitisha kugombea kwa mara nyingine na hatimaye kufanikiwa kubaki hapa Bungeni kwa kipindi cha tano. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwasahau wananchi wangu wa Jimbo la Kishapu, ni wananchi ambao kwa kweli wamenipa

heshima kubwa kuanzia kwenye kura za maoni mpaka leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kusimama kuchangia na kutoa mawazo kwenye Wizara kama hii kusema kweli Mbunge yeyote unapata faraja kubwa kwa sababu unajua unachangia kwenye Wizara ya watu makini ambao ni wasikivu, ambao ni wanyenyekevu na ambao wanajali maslahi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawapongeza sana Waziri wetu Aweso, Mheshimiwa Naibu Waziri, Kaka yangu Kundo na bila kumsahau dada yetu kipenzi Katibu Mkuu, Mwajuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu huyu ni mdogo sana, wakati anateuliwa nafasi hii ya Katibu Mkuu watu wengi walikuwa wanasema huyu dada mbona kama mdogo mdogo, lakini kwa kweli ameonesha kwamba umri haijalishi, kazi ndiyo kila kitu. Ninampongeza sana na atafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kweli kwa kuinua sekta ya maji hapa nchini kwetu, ametubeba sana. Maji ni changamoto kubwa na katika maeneo mengi ninafahamu kwamba bado kuna changamoto katika maeneo mbalimbali, lakini kwa kweli kujitoa kwake mama yetu huyu, kuweka fedha nyingi kwenye sekta ya maji, wananchi wengi vijijini na maeneo hata ya mjini wanamkubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza wasimamizi wa sekta hii ya maji, *CEO* wa *RUWASA* ambaye ni kaka yangu, *Eng*. Walter, *CEO* wa *DAWASA, Eng*. Bwire, ninawapongeza kwa sababu moja kati ya jambo kubwa ambalo nimekuwa nikipingana nalo miaka yote nikiwa Bungeni ni ubadhirifu na wizi. Wameweza kupambana na haya mambo kwa kusimama kidete, hawa-*compromise* kwenye *quality,* ninawapongeza sana. Ninaona kabisa sekta hizi zimepata watu makini, ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa uteuzi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mambo yafuatayo: mpaka sasa hivi jumla ya miradi 3,302 imekwenda vijijini. Hii ni miradi mingi sana, lakini nilikuwa ninaomba Waziri atupe jicho la kipekee kwenye Jimbo langu la Kishapu. Mheshimiwa Waziri mwenyewe anafahamu, alikuja na Mheshimiwa Rais wakati wa kuomba kura na alisimama akasema kwamba kwenye Jimbo hili atafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vyote, Kata zote ambazo zina changamoto ya maji nimeshamwelezea, Kata kama ya Mwataga wanayo changamoto ya maji kubwa, Kata ya Sekebugoro, Shagihilu, Masanga, Kiloleli, Ngofiram, Mwaweja, maeneo haya yote yana changamoto kubwa sana ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimwambie Mheshimiwa Waziri kwenye Jimbo langu la Kishapu kuna Kata moja ambayo haina maji ya bomba kabisa. Wamehangaika sana, chini hakuna maji, kama ambavyo Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba katika eneo letu la Jimbo la Kishapu chini ni pakame. Kwa hiyo, wananchi wanalalamika sana na wanahangaika sana kuhusu changamoto ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya miradi kwa mfano kama Kata ya Igaga, kuna miradi imeshafanyiwa usanifu, Kata ya Mwataga kuna miradi imefanyiwa usanifu na maeneo mengine. Hii miradi ambayo tayari imeshafanyiwa usanifu ninaomba sana, tusaidiwe tuweze kupata fedha kwa ajili ya kupeleka maji katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kwenye Kata zile nyingine ambazo zina mradi wa Ziwa Victoria unapita, Kata kama Sekebugoro, Kata kama Busangwa, Kata ya Mondo, Kata ya Bubiki, wananchi wanalalamika sana, hawana maji. *Imagine* mradi wa Ziwa Victoria unapita kwenye maeneo yao, lakini maji wao hawana, kwa kweli inasikitisha na inauma sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo tunajua kwamba maji ni uhai, ninakuomba uweze kutusaidia. Uwe na mkakati maalum wa kuangalia maeneo ambayo hayana kabisa maji, na

yale mengine ambayo yana unafuu unaweza ukawaangalia kwa *second hand*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo, pia ninaomba sana baadhi ya miradi mikubwa katika Jiji la Dar es Salaam pale *DAWASA,* ninaomba *DAWASA* pale iwekewe mkakati maalum iweze kupata fedh. Kingine, madeni ya *DAWASA* yachukuliwe na Serikali ili uboreshaji wa maji katika Jiji la Dar es Salaam uende kwa kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Mecktridis Fratern Mdaku, atafuata Mheshimiwa Ghati Chomete na Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola ajiandae.

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji ya mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka na neema zake. Pia, kwa nafasi ya kipekee ninamshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi nzuri anayoifanya katika Taifa letu, lakini pia kuendelea kuwa Rais wa maono kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri anayoifanya, anatuwakilisha vyema upande wa Serikali, pia na kazi nzuri anayoifanya ya ziara anayozunguka katika Mikoa yote Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya kipekee, ninapenda kumpongeza sana Waziri wa Maji, kaka yangu, Mheshimiwa Jumaa Aweso, Naibu wake, Mheshimiwa Kundo Mathew pamoja na Dada yangu Mwajuma Waziri na timu nzima ya watendaji wa

Wizara ya Maji kwa kazi kubwa wanayofanya kuhakikisha sekta ya maji iko vizuri na kumtua ndoo mwanamke kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza Kaka Kirita, *Engineer* wa *RUWASA,* kwa kutusaidia watu wa Malinyi kwa kushirikiana na Mhandisi wa Mkoa, *Eng*. Lutonja wa *RUWASA* Mkoa wa Morogoro. Pia na mhandisi wangu wa *RUWASA* Wilaya ya Malinyi, kaka yangu Marco Chogelo. Kwa kweli ninawashukuru sana kwa sababu Jimbo la Malinyi ni Jimbo lenye changamoto ya maji, lakini wamejitahidi kadiri walivyoweza kuhakikisha Malinyi inakaa vizuri na watu wanapata majisafi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Maji, na mchango wangu mkubwa nimeutoa kwa njia ya maandishi, lakini hapa leo ninapenda kuongelea tu kuhusu Jimbo langu la Malinyi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Maji kwa kutupa miradi katika Wilaya yetu ya Malinyi. Zaidi ya shilingi 1,100,000,000 zinakwenda kutekeleza katika maeneo ya Malinyi, Ihowanja, Biro, Misegesi, Mbalinyi pamoja na Kilosa Mpepo. Kwa kweli ninasema ahsanteni sana, ninashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa Malinyi tumekumbwa na changamoto nyingi kubwa ukiacha ya mafuriko ambayo pia na yale mabwawa yetu yanaharibika, lakini Serikali imetuangalia kwa jicho la huruma na inakwenda kutekeleza miradi hii. Hii miradi ilikuwa imekwama lakini sasa Serikali nadhani inatoa fedha kuhakikisha miradi hii inakwenda kukamilika na inakwenda kutekelezeka *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Aweso na timu yake, na nitawapa ushirikiano mkubwa kuhakikisha hii miradi inakwenda kukamilika ili adha ya maji katika Wilaya ya Malinyi iweze kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya miradi hii iliyotajwa katika bajeti ya Wizara ya Maji ya mwaka huu, bado Malinyi tuna

changamoto ya miradi miwili ambayo ni chakavu sana ikiwa ni mradi wa maji tiririka wa Mtimbira, ulijengwa miaka ya 1980 iliyopita na ilijengwa wakati huo ilikuwa inahudumia watu 12,000, lakini sasa hivi inahudumia wananchi 72,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa ninaomba Serikali iangalie uwezekano wa kwenda kukarabati mradi huu, itoe fedha ili mradi huu nao uende ukakamilike ufanyiwe ukarabati wa upanuzi wa miundombinu yake, matenki pamoja na mabomba. Pia, mradi wa Itete nao pia ni mradi wa maji ya mserereko lakini pia ni chakavu kama ulivyokuwa mradi wa Mtimbira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna uhaba wa maji katika vitongoji vya pembezoni mwa maeneo ya Madega, Njasa, Lumbanga, Mkanga, Butu pamoja na Shinyanga. Ninaomba maeneo haya pia ikiwezekana yaweze kupatiwa maji ya visima virefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malinyi hatuna changamoto ya vyanzo vya maji, tunavyo vyanzo vya maji vya kutosha vya mito pamoja na mabwawa, lakini tumekuwa hatupati yale majisafi na salama. Licha ya Wizara kujitahidi na *RUWASA* kujitahidi, dada yangu Mwajuma aliniambia siku moja: "Mheshimiwa Mbunge tena kwenu Malinyi mbona mnapata majisafi na salama mazuri kabisa! Katika Wilaya zote Mkoa wa Morogoro Malinyi tumejitahidi kuleta huduma hii." Ni kweli kabisa ninamshukuru sana, lakini bado hayatoshelezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Wizara iangalie kwa jicho la huruma hii miradi ya visima pamoja na hii miradi michakavu ikienda kukamilika itahudumia watu wengi sana wa Wilaya ya Malinyi na wao pia wataishukuru Serikali yao kwa kuwajali na kuwapa majisafi na salama. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nimwite sasa Mheshimiwa Ghati Zephania Chomete atafuatia Mheshimiwa Kangi Lugola na Mheshimiwa Santiel Kirumba ajiandae.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia. Nami pia nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika nchi yetu na hasa kwa kuhakikisha anaendelea kumtua mwanamke wa Kitanzania ndoo kichwani kama dhamira yake inavyojieleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, kwa kazi nzuri anayoifanya katika kumsaidia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Wizara hii ya Maji yeye pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu wetu wa Maji, dada yetu mahiri sana, mchapa kazi *Eng*. Mwajuma na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia sitaacha kuwapongeza sana Watendaji wa Wizara hii katika Mkoa wangu wa Mara kwa namna wanavyopambana kuhakikisha wanamtua ndoo mwanamke wa Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, bado kuna changamoto katika Mkoa wetu wa Mara. Tunashukuru sana kwa miradi ambayo imeletwa katika Mkoa wetu wa Mara, tumepata miradi 77 ya maji lakini miradi hiyo ina thamani ya shilingi bilioni 265 ambayo itaenda kuwanufaisha wananchi 985 katika Mkoa wetu wa Mara. Pia, tumepata miradi sita mipya ya maji yenye thamani ya shilingi bilioni 1.6. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi tunapokea, tatizo kubwa tulilonalo katika Mkoa wetu wa Mara ni kutokukamilika kwa miradi. Mimi ninaomba Waziri utakapokuja kuhitimisha hoja yake atuambie miradi hii ambayo ametupatia Mkoa wa Mara itakamilika lini? Hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024 tulisaini mradi wa maji wa miji 28 wa shilingi bilioni 134. Fedha hizo mpaka sasa mradi wa maji wa miji 28 haujakamilika, uko 15%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ambao tulisaini nao mradi huu, wao wako 80% na wengine 70%, lakini sisi 15%. Hii ni aibu kubwa sana. Tumezunguka kwa wananchi wa Mkoa wa Mara, akinamama wa Mkoa wa Mara tumewaambia dhamira njema ya Rais ya kuwatua ndoo kichwani, lakini mpaka sasa mradi ule mkandarasi hayupo *site,* mradi haujakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Wana-Mara tutaondoka na shilingi ya Mheshimiwa Waziri ili kusudi aje atuambie ule mradi utakamilika lini? Mkandarasi atalipwa lini? Mradi ule ukikamilika utaenda kuwasaidia mama zangu wa Wilaya ya Rorya, wa Wilaya ya Tarime Mjini na Jimbo la Tarime Vijijini baadaye na Serengeti. Hizi ni Wilaya ambazo zinateseka sana suala la upatikanaji wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijiji vingi havina maji. Mheshimiwa Waziri, ametembelea Mkoa wa Mara, amejionea namna gani akina mama wanateseka, lakini kuna sehemu tunashukuru amezigusa, ninaomba atakapokuja hapa atuambie ni lini mkandarasi wa mradi ule atapewa fedha ili aweze kukamilisha ule mradi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuipongeza Wizara hii. Tuliwahi kupata shilingi bilioni 70 kwa ajili ya kutekeleza mradi wa Mgango - Kiabakari na sasa ule mradi unaendelea kufanya vizuri, ila kuna kata moja ambayo ndiyo ule mradi umepita, Kata ya Tegeruka. Jamani changamoto ya pale ni mabomba. Ninaomba mradi ule mabomba yapelekwe ili Kata na vijiji vile ambavyo viko pale viweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, atafuatiwa na Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, na Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, ajiandae.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa, nina dakika tano tu, nianze na maneno haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2023/2024 tulianzisha mradi wa vijiji 24 Jimbo la Mwibara na tukatenga *token* ya shilingi 741,800,243. Mradi huo unahusu vijiji 24 vya Kisorya, Nambubi, Nampangala, Masahunga, Bwanza, Nansimo, Makwa, Busambu, Sunsi, Mwitende, Nambaza, Bunere, Busambara, Igundu, Bulendabufwe, Namalebe, Mchigondo, Namalama, Kitengule, Kibara A, Kibara B, Kibara Stoo, Mwibara na Nakatuba, lakini kwa bahati mbaya fedha hazikupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukaja mwaka wa fedha 2024/2025 tukatenga fedha shilingi bilioni moja kama *token,* lakini fedha hazikupatikana, mwaka wa fedha 2023/2024 tukatenga fedha, lakini fedha hazikupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso anafanya kazi kubwa sana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Watanzania tunapata maji, lakini kinachomwangusha ni tatizo la fedha. Tutapiga kelele, tutaomba miradi, lakini hakuna fedha. Sasa tukiendelea kutegemea fedha hizi za ndani, ninaamini vijiji hivi 24 vya Mwibara havitapata maji. Ninaomba, tutafute kwenye *alternative financing* ili tupate fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka wa fedha tunatenga fedha, tunasema mradi utatekelezwa na hautekelezwi. Tutafika mahali hatutaaminika. Wana Mwibara wasipomwamini Mbunge kwa yale anayoyasemea wataenda mbali zaidi, watailaumu Serikali. Sasa kama shida ni upatikanaji wa fedha, na kwa nguvu zake zote imeshindikana, labda nishauri kama kanuni zinaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua wakati mwingine tukimtegemea Mungu anaweza akajibu. Kama Kanuni zinaruhusu

nije hapo mbele ashike bajeti yake nimwombee kwa Mungu ili Mungu aweze kujibu, kwa sababu haiwezekani miaka yote hii ya fedha tunatenga fedha hazipatikani! Tunatenga fedha hazipatikani! Tunatenga fedha hazipatikani, lakini kwenye maombi kila siku tukicha wenzetu Makanisani na Misikitini aah, maombi hujibiwa na matokeo tunayaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mambo mawili ya muhimu sana. Jimbo la Mwibara tumezungukwa na maji na kijiji cha mwisho ni kilometa mbili kutoka kwenye chanzo cha maji ya Ziwa Victoria. Kijiji ambacho kipo mbali na maji, kiko kilometa mbili, inakuwaje badala ya kusubiri tupate fedha hizi nyingi, tunaweza…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa malizia, muda wako umeisha, malizia kengele ni moja tu.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Haya, ninakushukuru sana. Nilimwita Mheshimiwa Amina Mussa Mkumba, Mheshimiwa George Natany Malima atafuatiwaa na Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma ajiandae.

**MHE. AMINA M. MKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika Hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Maji 2026/2027. Awali ya yote, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza, nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, karimu kwa kuniwezesha kusimama hapa kuchangia katika hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana pia Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na chama changu, Chama Cha Mapinduzi kwa kuniwezesha kuwa Mbunge katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninaomba pia kuwashukuru sana wananchi wa Kibiti kwa imani kubwa waliyonipa, ninawaahidi imani hiyo nitailinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa michakato mbalimbali, kwa hatua nyingi ambazo amezifanya katika kuhakikisha kwamba anamtua mama ndoo kichwani; na sisi Kibiti tumeshuhudia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akimtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa Maji, kaka yangu Jumaa Aweso, Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Meneja wa Maji Kibiti, Mabula, Meneja wa Maji Mkoa, kiukweli wanatupa ushirikiano sana, ninawapongeza sana. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri na timu yake. Tumeona juhudi mbalimbali za kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata maji; na mwenyewe ametumia neno hapa la kutangatanga na ninawatia moyo katika juhudi zao na Mwenyezi Mungu atawajalia na Tanzania itapata maji. Nipongeze pia hali ya upatikanaji wa maji Tanzania. Upatikanaji wa maji vijijini umefikia 85.2% mwishoni mwa mwaka 2025; hiyo ni hatua kubwa, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zote hizo, sisi katika Wilaya yetu ya Kibiti bado tuna changamoto nyingi katika maji. Katika eneo la Kibiti kuna eneo la visiwani ambapo kwa sasa hatuna miradi yoyote ya maji; na katika eneo hilo kuna Kata tano za Mbuchi, Kiongoloni, Msala na Makaloni. Niiombe sana Wizara, kwa sababu katika kata hizo kuna wananchi wengi na wanahitaji huduma ya maji, wahakikishe kwamba wanatenga bajeti kwa ajili ya kwenda kuweka miradi ya maji katika kata hizo. I(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi ambayo imeshakamilika, lakini inatoa maji ya chumvi. Tuna Mradi Mchungu ambao unatoa maji, lakini unatoa maji ya chumvi. Niiombe Wizara ihakikishe kwamba inafanya *process* za kusafisha maji ili watu waweze kunywa maji mazuri, masafi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna madeni ya wakandarasi. Kuna Mradi wa Nyanjati, mkandarasi anadai shilingi milioni 200; Mradi

wa Jaribu Mpakani, mkandarasi anadai shilingi milioni 100; Mtunda shilingi milioni 150. Sasa labda niulize Wizara, ni lini wakandarasi hawa watalipwa madeni yao ili watu waanze kupata maji safi na salama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nipongeze sana wizara kwa mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kwamba Taifa letu linapata maji kwa miradi mikubwa kwa ajili ya Gridi ya Taifa ambayo inaunganisha Ziwa Victoria na maeneo mengine ambayo yana uhaba wa maji. vilevile Bwawa la Kidunda ambalo litahakikisha kwamba maeneo ya Dar es Salaam na Mikoa ya Pwani tunapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, niendelee kuwapongeza Wizara na pia nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwapambania wanawake wa Tanzania na kuhakikisha kwamba mama anapata unafuu katika utafutaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja Wizara hii kwa asilimia mia moja. Ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Namwita sasa Mheshimiwa George Natany Malima, Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma, Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mheshimiwa Sheila Lukuba na Mheshimiwa Jafari Chege wajiandae.

Mheshimiwa George Malima hayupo; tuendelee na anayefuata, Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma; Mheshimiwa Kinyoma hayupo; Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba hii ya Wizara ya Maji. Nianze kwa kusema kuwa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Wizara hii ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutuletea bajeti hii ya shilingi trilioni moja na *point*. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri

Jumaa Aweso, nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri Kundo, niwapongeze wafanyakazi wote wa Wizara ya Maji wakiongozwa na *Engineer* Mwajuma Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kuhusu Mkoa wangu wa Kilimajaro. Katika Mkoa wa Kilimanjaro tumepata mradi mkubwa wa shilingi bilioni 406 na *point*. Mradi ule umekwenda vizuri sana katika awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani, tunaishukuru sana Serikali ya Awamu Sita kwa kupitia Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. Waswahili wanasema 'Kushukuru ni kuomba tena'. Tunaamini kwamba awamu ya kwanza iliyotekelezeka imefanya kazi vizuri, imewatua akina mama ndoo kichwani kwa kiasi fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali iendelee kutoa fedha kwa ajili ya kuendeleza mradi huu katika awamu nyingine ya pili ambayo itachochea sana maji kwa matumizi ya nyumbani, na zoezi la kumtua mama ndoo kichwani litakuwa linaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongelea Mradi huo wa Kilimanjaro, nitaongelea *RUWASA*, Wakala wa Maji Vijijini. *RUWASA* ni chombo ambacho kinafanya kazi katika vijiji vyetu vyote vya Tanzania. *RUWASA* wanafanya kazi nzito na ngumu kwa mazingira yao. Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote tunafahamu kwamba asilimia kubwa ya wananchi wetu wanaishi vijijini na vijijini kule ndipo hapo palipo na ile kauli ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kazi aliyoifanya Mheshimiwa Rais katika kuchimba maji chini kwa kupitia magari. Maeneo ambayo hakuna maji kabisa tumewaona akina mama, hii ni kazi ya *RUWASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RUWASA* hii hii, ukiangalia bajeti yake ni ndogo sana. Ili ifanye kazi vizuri inahitaji kuongezewa bajeti. Kwa kuwa bajeti yao ni ndogo na watumishi wao ni

wachache, ili wafanye kazi vizuri tunaiomba sana Serikali iongeze bajeti *RUWASA*. Isitoshe kwenye kuongeza bajeti tu na watumishi hawatoshi. Pia iende mbali, ihakikishe kwamba inaweka mipango mizuri ya kuwapanga watumishi hawa kikanda ili kusudi lililokusudiwa likapate kutekelezeka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni suala la mabonde. Tunayo mabonde tisa nchini. Watu wote tumesimama hapa tunaongelea kuhusu vyanzo vya maji, tunaongelea kuhusu uchafuzi wa maji, tunaongelea kuhusu matumizi mabaya ya maji; lakini wanaohusika na haya ni hawa watu wa mabonde. Watu wa mabonde ndiyo wanaosimamia vyanzo vya maji. Tumeona, wote ni mashahidi; tumesimama hapa tumeongea katika Bunge lako Tukufu, yako maeneo ambayo ukipita, sisi wenyewe tukipita kurudi majimboni kwetu tunaona jinsi wananchi wanavyofanya shughuli za maendeleo za kilimo kwenye mifereji. Tunaona jinsi ambavyo wananchi wanafanya shughuli zao za maendeleo kwenye nishati kinyume na utaratibu wa matumizi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali, hawa watu wa Bonde la Maji waweze kuangaliwa kwa jicho la tatu. Maana ya jicho la tatu ni nini; kwanza waongezewe bajeti ili waweze kufika katika vyanzo vya maji ambavyo wanavyo ambavyo vinaharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niseme kwamba ninaunga mkono hoja. Niishukuru sana Serikali ya Awamu ya Sita, iendelee kutoa fedha ili kazi ya maji inayoendelea nchini ikapate kukamilika vizuri. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Sheila Lukuba, hayupo, Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara yetu hii ya Maji. Kwa sababu ya muda nianze kwa kuazima maneno ya Mheshimiwa Waziri wa Maji mwenyewe ambayo amekuwa akiyatumia sana; kwamba ‘Moyo usiyokuwa na shukrani hukausha mema yote’.

Kwa kweli kwa mtu ambaye hatakuwa na moyo wa shukrani kwa kazi kubwa nzuri ambayo Mheshimiwa Waziri ameifanya kwa muda wote ambao amekuwa kwenye wizara hii, basi atakuwa anakausha mema yote ambayo kimsingi halitakuwa jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua dhamira nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambayo inakwenda kutafsiriwa na Waziri wa Maji kwa namna ya utendaji wake wa kazi, yeye pamoja na wasaidizi wake, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara. Sisi tunawaombea kila la kheri Mheshimiwa Waziri, tunajua kuwa atafika kule ambako kunakusudiwa kwa namna ambavyo anaendelea kutafsiri maono na dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia ya kumtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, pamoja na dhamira nzuri aliyonayo Mheshimiwa Waziri nimwombe autazame sana Mkoa wa Mara. Katika tafiti ambazo zipo za ukiangalia hata tafiti zake katika mikoa yote 26 atatambua kwamba Mkoa wa Mara ndiyo mkoa ambao kama si wa mwisho, basi ni wa pili kutoka mwisho kwa changamoto kubwa sana ya maji. Wakati tunakumbana na changamoto hii, ni mkoa ambao unazungukwa na maji kwa isiyopungua 60% kwenda mpaka 70%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano Wilayani kwangu Rorya; mimi peke yangu ninazungukwa na maji; kwa maana ya Ziwa hili Victoria ambalo linatoa maji kwenda mahali parefu, yanakwenda Nzega, yanakwenda Dodoma na maeneo mengine; ninazungukwa na maji 77%. Yaani eneo la nchi kavu ambalo tunaishi sisi na kufanya shughuli zetu za kiuchumi ni 23% pekee yake, 77% ni maji pekee yake; lakini unaweza ukaona katika wilaya zote za Mkoa wa Mara, wilaya ambayo ina changamoto kubwa ya maji ni Wilaya ya Rorya. Ninatambua juhudi zake na kazi kubwa nzuri alizofanya katika awamu iliyopita kwa miaka iliyopita, amenisimikia miradi kadhaa pale, lakini miradi ile imesimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri, pamoja na majibu mazuri atakayoyatoa hapa leo sina sababu ya

kumshikia shilingi, lakini apange namna ya kufanya ziara; twende tukatembelee miradi ile ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia ametupa fedha lakini miradi mingi imesimama na haitoi maji. Ninamtegemea sana Mheshimiwa Waziri, kwa sababu kwa kufanya hivyo ninaamini kuwa tutaondoa manung'uniko ya wananchi kwenye maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo Mradi wa Miji 28, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri; ninajua ni juhudi zake yeye. Bila yeye Wana-Rorya wasingepata ule mradi pamoja na Tarime. Alikwenda akamshawishi Mheshimiwa Rais, akaridhia mradi ule uingizwe kwenye bajeti na sasa unatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ule unakwenda kwa kusuasua sana, tuombe fedha. Nichukue nafasi hii kuomba sana Wizara ya Fedha wautazame mradi ule. Mradi ule ndilo suluhisho la changamoto ya maji kwenye wilaya zaidi ya tatu zenye *population* zaidi ya watu 200,000 wanakwenda kutatuliwa na changamoto ya maji kwa kukamilika kwa mradi ule. Niombe sana Wizara ya Fedha watoe fedha ili mradi ule uweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kutambua na changamoto zilizopo, mimi nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba wakati tunaingia 2021 changamoto ya maji kimkoa tulikuwa kwenye 54% peke yake, sasa hivi tupo kwenye 81%. Tumwombe aweke nguvu chini, akazane kadiri anavyoweza ili na sisi tuondokane na changamoto ya maji kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri mambo mahususi kama matatu. Kwanza, upo mradi wa Kata ya Kang'ombe, mradi ule ndiyo wanaouita Mradi wa Nyihara. Mheshimiwa Dkt. Samia ametupa zaidi ya milioni 600. Mheshimiwa Waziri autazame mradi ule. Leo wananchi wa kata ile zaidi ya 20,000 hawapati maji safi na salama pamoja na kupewa shilingi 600,000,000 kwa sababu ya upungufu wa shilingi 20,000,000 peke yake ya kukamilisha kuwalipa watu wa *TANESCO* waweze kuunganisha maji kwa kutumia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 20,000,000 hii ninaamini Mheshimiwa Waziri akitamka leo haina sababu ya kusubiri bajeti ya mwakani. Mradi wa shilingi 600,000,000 tayari tumeshakamilisha, shilingi 20,000,000 ya kuwalipa *TANESCO* ili waweze kuweka transfoma pale wananchi wanufaike. Mradi umesimama; na nimeona kwenye bajeti humu tunaambiwa hadi 2027. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atakaposimama jioni ya leo, aweze kusema neno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ningetamani nimshauri Mheshimiwa Waziri ni kwenye hizi jumuiya za maji; zinahangaika sana. Tumepewa sana miradi kule vijijini, unakuta mtu ameishiwa LUKU ya shilingi 20,000, mlolongo wa maombi ya kununua luku anaanza yeye, inakwenda inapitishwa na wilaya, inakwenda mkoani, inakuja *HQ,* inakwenda Hazina; shilingi 20,000 peke yake wananchi wamekaa wanamsubiri. Niombe utaratibu huu ufumuliwe; ikiwezekana kama inawezekana iishie ngazi ya mkoa ili angalau tupunguze manunguniko kwa sababu miradi ipo, lakini inakaa muda mrefu haiwezi kutoa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri jambo la pili; tumepewa mitambo ya kuchimba visima gharama za kukodisha mitambo ile ni kubwa sana. Kuna wakati Mheshimiwa Mbunge anatamani atoe fedha hata ya Mfuko wa Jimbo kusaidia kuchimba visima, lakini gharama za kukodisha mitambo ambayo tumepewa sisi wenyewe ni gharama kubwa sana. Niombe wazipitie gharama hizi ili ziweze kuwanufaisha wananchi. Tupo tayari sisi kuwasaidia wananchi kwa kuunga juhudi kama wadau lakini gharama za kukodisha mitambo zimekuwa ni kubwa wakati mwingine tunashindwa kufikia malengo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe lingine ambalo ninafikiri Mheshimiwa Waziri anaweza akalifanyia kazi; ni kuhakikisha kwamba; kama nilivyosema; miradi yote ambayo tayari Mheshimiwa Dkt. Samia alitoa fedha, ipo kwenye maeneo mbalimbali, tuhakikishe miradi ile inakamilika na inatoa maji. Ikibidi na ikimpendeza Mheshimiwa Waziri ahakikishe kuwa ile miradi ya zamani inakamilika kwanza kabla hatujaanzisha miradi mipya.

Kwa sababu miradi ya zamani tayari ipo, Mheshimiwa Dkt. ameweka fedha, lakini wananchi hawanufaiki na miradi ile. Ikianzishwa mradi mpya na ilihali mradi wa zamani bado haujanufaisha wananchi; tunakuwa hatujafanya jambo sawa; kwa sababu tunakwenda na tunarudi nyuma. Matokeo yake ndiyo maana ukisema asilimia za upatikanaji wa maji bado tunaonekana tuna changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtakie Mheshimiwa Waziri kila la kheri, ninajua yeye ni msikivu na ninajua anakwenda kuyatatua haya Waheshimiwa Wabunge tunayoyasema. Ninaamini kabisa kwa uwezo wake na uchapakazi wake sina shaka juu ya hili. Hata hivyo, ningetamani atamke neno juu ya mradi wenye upungufu wa shilingi 20,000,000 ili wananchi wa Kata ya Kyang'ombe waweze kunufaika na maji ya shilingi 600,000,000 ya Mama Samia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. Nimwite Mheshimiwa Sheila Lukuba.

**MHE. SHEILA E. LUKUBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Maji. Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia kuweza kusimama kwenye Bunge lako Tukufu. Pia ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Morogoro, kwa jinsi anavyopambana kuhakikisha anamtua mama ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri Aweso pamoja na menejimenti yake yote kwa hotuba yake nzuri iliyoshiba yenye matumaini kwa wananchi wa Tanzania. Ninatoka Mkoa wa Morogoro, tuna majembe kule Mkoa wa Morogoro, Ndugu yangu Kejo na ndugu yangu Lusajo. Watu hawa wamekuwa ni wapambanaji, ukipiga simu moja tu wanapokea. Ninadhani kuna mafunzo ambayo wamepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitakwenda na mstari unasema Mathayo 10:42 Yesu anasema: "Na yeyote atakayemnywesha mmoja wa wadogo hawa kikombe cha maji baridi kwa jina la mwanafunzi, amini nawaambia hatopoteza thawabu yake".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa tendo la Mheshimiwa Rais wetu Samia Suluhu Hassan kuanzisha Gridi ya Taifa, sisi wanawake wa Mkoa wa Morogoro tunampongeza. Watu wote sasa wanakwenda kuoga, tunakwenda kumwagilizia, lakini wote tunakwenda nchi nzima kunufaika na maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Morogoro pia tunamshukuru Mheshimiwa Rais, hadi Disemba, 2025, ameweza kutupa kiasi cha shilingi 456,000,000,000 ambapo miradi ya shilingi 58,000,000,000 imeshakamilika na miradi ya kiasi cha shilingi 397,000,000,000 wakandarsi bado wanadai. Niwaombe Wizara ya Fedha kupitia Wizara ya Maji, waweze kutoa fedha hizo ili miradi iweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumpongeze pia Mheshimiwa Rais, Mkoa wa Morogoro wakati anaingia tulikuwa na 53% tu ya upatikanaji wa maji safi na salama, lakini mpaka Desemba, 2025 Mkoa wa Morogoro upatikanaji wa maji kwa sasa ni 72%. Ahsante sana mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maji hayo kumekuwa na uchafuzi wa maji katika vyanzo mbalimbali. Niwaombe Wizara ya Maji kwa kushirikiana na TAMISEMI waweze kuvilinda vyanzo hivyo hata kwa kutumia mgambo wa halmashauri ili watu waweze kupata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Waziri, TAMISEMI na Ofisi ya Rais na Mazingira kwamba Mkoa wa Morogoro urudishiwe misitu ya zamani ya Milima ya Uluguru, Udzungwa, Lumuma, Kipate, Lubeho, Turiani, Lumbiji na milima mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, milima hiyo ni vyanzo vikuu vya maji kwenye Mkoa wa Morogoro. Mabwawa yote haya tunayoyajenga yanategemea maji kutoka kwenye vyanzo hivyo. Hivyo niwaombe turudishe ule uoto wa zamani wa milima hii. Pamoja na kwamba sisi Mkoa wa Morogoro tuna mabwawa, (Bwawa la Mwalimu Nyerere na Bwawa la Kidunda) lakini tuna upungufu wa maji kwenye vijiji 65. Vijiji hivi havina maji kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa Mkoa ningeweza kutaja kijiji kimoja kimoja, lakini nitataja kwa ujumla. Wilaya ya Mvomero, vijiji 19; Morogoro Vijijini; vijiji 27; Kilosa; vijiji 14; na Gairo; vijiji vitano. Nitamwomba Waziri atakapokuwa anakuja kumalizia; je, Serikali haioni kuna umuhimu sasa wa kuweka mkakati wa muda mfupi ili vijiji hivi viweze kupata maji safi na salama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimwombe Waziri Aweso ndugu yangu ana watendaji wazuri sana kwenye Mkoa wa Morogoro, lakini *RUWASA* – Kilosa, Ulanga, Malinyi hawana magari. Nimwombe ndugu yangu awapatie magari ili wakishindwa kufanya kazi aweze kuwawajibisha ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, ninaomba niunge mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Edibily Kazala Kinyoma aweze kuchangia.

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia. Kwanza ninaomba niipongeze Wizara kwa kazi kubwa ya kizalendo kazi ya kiwito kabisa ya kuwatumikia Watanzania. Pia, nimshukuru Mheshimiwa Rais, lakini pia nimpongeze kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya kazi ya utu ya kuhakikisha anamtua ndoo kichwani mama zetu na dada zetu wanaohangaika usiku na mchana kuhakikisha wanatunza familia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Wizara nimeona kwenye bajeti yao pale wamenitengea shilingi bilioni 1.5 kuhakikisha Kijiji cha Chekenya, Kabulanzwili, Muzye, Nyakitonto, Malalo, Kazage, Makere, Nyangwa, Kalimungoma na Rusesa wanapata maji safi na salama bila kusahau Titye na kisima kinachokwenda kuchimbwa Kijiji cha Mvugwe. Kwa kweli ninawashukuru sana Wizara kwa moyo huu mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe fedha hizi wasichelewe watuletee kwa haraka, wananchi wanayo hamu kubwa ya kupata huduma hii ya maji. Wakati ninamaliza ninaomba nishauri kitu kimoja tu kwenye Wizara pamoja na kazi kubwa wanayoifanya; bado kuna shida kubwa kwenye upotevu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Waziri alivyozungumza mwenyewe wakati anawasilisha, tuna upotevu wa maji zaidi ya 30% kwenye Taifa letu. Tunapozungumza zaidi ya 30%, ripoti ya mwisho inaonesha zaidi ya 35% tunapoteza maji kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake hii 35%, kama tuna 100% kwamba 35% tunapoteza, maana yake maji hayawafikii wananchi. Tunaweza tukasema kwamba labda tumetoa milioni kadhaa za lita za maji zinawafikia wananchi, lakini ukienda maana yake *field* haya maji hayapo. Kwa hiyo, iko haja ya Serikali na Wizara kuongeza mbinu mbadala za kuhakikisha wanadhibiti maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri, ikiwezekana watumie teknolojia ya kisasa ikiwemo zile *sensors* za kujua wapi kuna *leakage* za maji. Ukienda mijini utakuta maji yanatiririka hovyo na vijijini mpaka pengine unaona huruma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine niwashauri waongeze uwajibikaji hasa wale watumishi wa chini, maana kuna eneo unaweza ukapita unakuta *leakage* ni ndogo tu, lakini maji yanatiririka zaidi ya wiki mbili na watumishi wako pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri watu wa *RUWASA* kwa kwetu kule vijijini wajitahidi unakuta changamoto ni ndogo tu hata ukifunga mpira tu, lile eneo linakuwa limezibika. Kwa hiyo, nishauri kwenye upotevu wa maji wajitahidi watumie *sensors,* lakini pia watumishi wawe *active* kupambana na hizi changamoto ndogo ndogo zinazowezekana kutibika kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa utafiti tunapoteza zaidi ya shilingi 185,000,000,000 kwenye upotevu wa maji. Kwa hiyo, unaweza ukaona ni fedha nyingi na mapato mengi yanapotea ambazo ni fedha za Watanzania ambazo zingeweza kusaidia kuchimba visima vya kutosha, vingeweza kusaidia kuwapelekea maji kwenye vijiji vingine ambavyo tunasema…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. EDIBILY K. KINYOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Masache Kasaka.

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kupata nafasi kuweza kuchangia kwenye hii Wizara muhimu sana, Wizara ambayo haina mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na timu yake yote ya Wizara kwa kazi kubwa ambayo wanaendelea kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kilio cha Watanzania wote ni maji na wao wamejizatiti kuhakikisha kwamba hakika hawalali kuhakikisha kwamba wanafikisha maji kwa kila Mtanzania, hongera sana kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa *champion* kuhakikisha kwamba anaendelea kuwatua akina mama ndoo

kichwani. Hili kwetu sisi tunampongeza yeye na tutaendelea kumwombea ili azma yake ile iweze kwenda kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia *RUWASA* kuanzia *DG* wake na viongozi wake kwa Mkoa mpaka Wilayani kote wanafanya kazi kubwa nzuri na tumeona miradi mingi ambayo tumeenda kuitembelea. Hata kule Wilayani kwangu Chunya fedha nyingi ambazo zimekwenda kwenye upande wa *RUWASA* kule vijijini zimeweza kwenda kufanya kazi na matokeo yanaonekana na *DM* wangu *Engineer* Oleneno Sanga kwa kweli anafanya kazi kubwa sana. Tusipowasifu wakiwa hai hatuwezi tukawasifu wakiwa hawapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi kubwa ambayo inaendelea kufanyika tumeona hapa karibu Wabunge wote ambao wamesimama hapa jambo kubwa wanaipongeza Serikali kupeleka miradi kwenye maeneo yao. Hata hivyo, jambo kubwa ambalo wameenda kuwa kilio chao ni kutokamilika miradi hii kwa wakati na fedha kwenda kwa kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinapokwenda kwa kusuasua maana yake miradi hii yale malengo ambayo yamewekwa kwenda kuwafikia kwenda kumtua mama ndoo kichwani hayawezi kufikikiwa kwa wakati. Sasa, ushauri wangu ni nini? Ushauri wangu kama Serikali, kama nchi twende na mkakati wa pamoja kwenda kutafuta fedha ili miradi hii yote chechefu twende tukaitatue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona mfano kupitia hatifungani kwenye Mkoa wa Tanga imeweza kufanya vizuri. Hii tuchukue kama *sample* kwenye nchi nzima twende na *model* hiyo twende tukauze hatifungani hizi tupate fedha ili miradi kwenye kila Jimbo kila mahali iweze kukamilika ndiyo tutakuwa tumeenda kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye lazima wajue wananchi wetu kwamba maji ni huduma, lakini maji ni biashara. Tunapofungua bombani maji yanapotoka wao watalipa. Kwa hiyo maana yake tukienda kwenye hatifungani tutapata fedha,

ile fedha ambayo ataendelea kutumia ndiyo ambavyo itaenda kurudi na kurudisha ile fedha ambayo imetumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo lakini wananchi wangu wa Chunya Mjini wamenituma maji. Leo ninapozungumza haya na Mwenyekiti wangu wa Bodi yuko hapa juu kwenye Jukwaa la Spika pamoja na wapiga kura wangu wengine, akina mama wameniambia usipozungumza habari ya maji Chunya Mjini hatutakuelewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chunya Mjini tupo kwenye Mradi wa Maji wa Miji 28. Miji 28 kwa kweli kwa Chunya bado haijaanza hata kidogo na tunafahamu juhudi ambazo zinaendelea kufanyika. Pamoja na yote hayo, tuone namna nzuri na bora kuhakikisha kwamba mradi huu unaanza na wananchi hawa wanaenda kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa zaidi wakati juhudi hizo zinaendelea twende tukatatue changamoto hii kwenda kuchimba visima japo vichache kwa muda mfupi ili changamoto ya maji pale Chunya Mjini iweze kupungua au iweze kwisha ili wananchi wangu wa Chunya na wao waweze kuona Wizara ya Maji na yenyewe inasikia kilio chao na inakwenda kuwatatulia hili. Bila kufanya hivyo *DM* wangu wa pale Chunya *Engineer* Chamsa ataendelea kulalamika na wananchi wataendelea kumlalamikia anafanya kazi lakini watu wa Chunya Mjini wanataka maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja kwamba pale Chunya Mjini kuna changamoto ya maji, bado kuna miradi michache chechefu ya kule upande wa *RUWASA,* kuna Mradi mkubwa wa Matwiga *phase two*. Mradi huu uli-*design*-iwa kwa vijiji nane, lakini sasa hivi unatoa maji kwa vijiji viwili. Kwa hiyo ile *pressure* ambayo imetoka kwenye chanzo kwenda kwenye tenki mpaka kwenye usambazaji huo imekuwa kubwa kwa sababu *design* yake imekuwa ni vijiji nane na sasa hivi inakwenda vijiji viwili hivyo inapelekea changamoto ya mabomba kupasuka mara kwa mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mitambo ambayo imefungwa pale na kile ambacho kinaenda kuzalishwa hivyo wananchi hawa wanalipa kidogo kuliko umeme ambao unatumika pale. Matokeo yake mradi uendeshaji wake ni mkubwa kuliko kile ambacho kinakusanywa. Niombe twende tukaumalizie mradi huu ili uweze kwenda kutekeleza na vijiji vingine kwa maana ya Kijiji cha Mazimbo kiweze kwenda kukamilika. Fedha zimeombwa na zikipatikana zaidi ya shilingi milioni 300 *at least* pale zitaweza kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vingine vya Mtanila na maeneo ya jirani kwenye ule mradi vikiweza kukamilika ndivyo ambavyo tutaweza kwenda kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kupata nafasi hii na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge tumemaliza idadi ya wachangiaji waliokuwepo katika *list* yetu ya sasa ya muda huu.

Matangazo machache; la kwanza wageni waliopo mchana huu ndani ya ukumbi wa Bunge. Hawa ni wageni wa Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Waziri wa Maji ambao ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Pangani. *(Makofi)*

Tunao pia, wataalamu kutoka Wizara ya Maji na taasisi zake, Wataalamu mbalimbali, Wadau wa Sekta ya Maji, Wakandarasi Washauri na Wadau wa Maendeleo. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo pia, Viongozi wa Vyombo vya Utoaji Huduma ya Maji Ngazi ya Jamii. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kwa ujumla wake Mheshimiwa Waziri alikuwa na makundi mbalimbali ya watu wakiwepo Madiwani 10, Watendaji wa Kata 10, Kampeni Meneja wawili, Makatibu wa Mbunge wawili na vilevile ana ndugu na marafiki mbalimbali ambao wamo ndani ya Ukumbi huu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Wageni wa Mheshimiwa Mhandisi Kundo Andrea Mathew, Naibu Waziri wa Maji; hawa ni ndugu Nkeyenge Nkeyenge, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, karibu sana yuko pale, Ndugu Judith Ringia yeye ni Kaimu Mkurugenzi, Halmashauri ya Mji wa Bariadi. *(Makofi)*

Tuna Madiwani wa Halmashauri ya Mji wa Bariadi, Watendaji wa Kata wa Mji wa Bariadi, Makatibu wa Mbunge Jimbo la Bariadi na Makampeni Meneja wote kwa ujumla wenu mnaweza kusimama. Karibuni sana ndani ya ukumbi wetu huu wa Bunge. *(Makofi)*

Tuna Mgeni aliyetembelea kwa ajili ya Mafunzo, Ndugu Godliving Monyo kutoka Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *(DIT)*. Karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na uchangiaji jioni. Tutakaporudi tutaanza na wafuatao: Mheshimiwa Yohana Msita, Mheshimiwa Dkt. Neema Majule, Mheshimiwa Luboja Silvery, Mheshimiwa Neema Mwandabila na Mheshimiwa Abubakari Asenga.

Baada ya matangazo hayo, ninasitisha kikao cha Bunge mpaka saa kumi na moja jioni. *(Makofi)*

*(Saa 6.54 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mheshimiwa Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Yohana Msita, Mheshimiwa Dkt. Neema Majule na Mheshimiwa Silvery Luboja ajiandae.

**MHE. YOHANA S. MSITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuwa mchangiaji wa kwanza jioni hii. Ninaomba nichukue nafasi hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima, lakini kuwashukuru sana wananchi wangu wa Jimbo la Itigi kwa kuendelea kuniombea, ninawaahidi kuitenda kazi kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya katika Sekta ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia kijana mahiri kabisa Mheshimiwa Jumaa Aweso pamoja na Naibu wake na Katibu Mkuu. Kwa kweli Wizara hii ya Maji wanaitendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona ari na nguvu na moyo walionao wa kufanya kazi. Changamoto ambayo ninaiona ni upatikanaji wa fedha. Tunakubaliana sote hapa kwamba maji ni uhai; pasipo maji hakuna maisha. Sasa, kama ndivyo Wizara hii ya Maji lazima tuipe kipaumbele sana, tuhakikishe fedha zote ambazo zinatakiwa kufika ndani ya Wizara hii zinafika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mkoa wa Singida bajeti iliyopita ilitengewa jumla ya shilingi 10,000,000,000 kwa ajili ya maji. Mpaka kufikia mwezi Machi ilishapokea jumla ya shilingi bilioni 1.6 tu pekee. Hii maana yake nini? Maana yake ni kwamba, miradi mingi ya maji haijatekelezeka. Katika Jimbo la Itigi viko vijiji havijawahi kuonja ladha ya safi na salama, kwa maana ya maji ya bomba. Vijiji kama Ipangamasasi Kata ya Idodyandole, Mnazi Mmoja, Tulieni, Kalangali, Chabutwa, Ipalalyu na Mgandu, vijiji hivi havina miundombinu kabisa ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaomba Serikali, tunapoipitisha bajeti tujitahidi kutafuta vyanzo vya fedha ili miradi hii ya maji iweze kukamilika na miundombinu iweze kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Itigi lina changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji chini ya ardhi. Mitambo imekuja na ninawashukuru watu wa Wizara. Mitambo imekuja imechimbwa; vijiji ambavyo maji hayajapatikana, Vijiji kama vya Mtakuja, Makale, Kayui, Chagutwa, Kintanula, Itagata, Mwamagembe, vijiji hivi lazima tuje na njia mbadala tuone namna gani tunaweza kuwasaidia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vimechimbwa visima vingi, lakini maji hakuna. Sasa, inawezekana labda mitambo yetu uwezo wake ni mdogo, aidha, tunachimba mita ni chache zaidi. Tuje na mkakati mahsusi tuhakikishe kwamba vijiji hivi vinapatiwa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Jimbo la Itigi upatikanaji wa maji safi na salama ni 66% bado tuko chini. Ninaomba watu wa Wizara watuangalie kwa macho mawili, tuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji katika Jimbo langu la Itigi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tunayo mito, tunayo mabonde na kadhalika. Huu mpango wa kuchimba mabwawa, ninadhani kwenye Jimbo la Itigi uelekezwe kwa kasi kubwa sana, kwa sababu chini ya ardhi sehemu nyingi hatupati maji. Maeneo

kama ya Mbugani, Doroto, Kitaraka, Itagata, Makale, maeneo ambayo maji hayapatikani, tuchimbe mabwawa yaweze kupunguza adha ya upatikanaji wa maji. Maji ya binadamu, lakini sisi Jimbo la Itigi pia ni wafugaji wazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawaomba sana, suala la uchimbaji wa mbwawa katika Jimbo la Itigi lipewe kipaumbele ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu pamoja na mifugo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala la vitendea kazi; Jimbo la Itigi hivi ninavyozungumza watu wa Maji pale Itigi Mjini wanayo pikipiki moja. Ile ni halmashauri, angalau basi tuongezewe pikipiki angalu zifike hata nne, lakini tupatiwe na gari ili watendaji wetu waweze kufanya kazi zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, ninaiomba sana Wizara watuangalie watu wa Jimbo la Itigi kwa macho mawili ili tuweze kufika zile asilimia ambazo kwa mujibu wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi inatutaka tufike, hasa kwenye majimbo ya vijijini katika ile 85%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yohana Msita. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Neema Majula, atafuata Mheshimiwa Silvery Luboja; na Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba ajiandae.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi hii ya kuchangia jioni. Nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu ambaye amefanya mambo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka kwa *issue* hii ya maji ni ajenda kabisa ya Rais wetu. Toka alipokuwa Makamu wa Rais, ajenda ya kila mwanamke ni ajenda ya Rais. Akiwa Makamu wa Rais amehakikisha alipambana na kupunguza vifo vya mwanamke na mtoto, akijipambanua kabisa kwamba yeye ni

mwanamke. Pia amebeba ajenda hii ya maji kumtua ndoo mwanamke kichwani, lakini amebeba ajenda nyingine sasa hivi ya kumtua mwanamke kuni kichwani. Moja kwa moja ajenda yote ya mwanamke inakuwa ajenda ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kongole nyingi sana ninampatia Rais wetu kwa kazi kubwa na kutuangalia sisi wanawake kwa jicho la tofauti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana pia Mheshimiwa Jumaa Aweso. Nami ninasema ni Waziri wangu, akiwa Waziri hivi hivi aliniteua kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya *DUWASA*. Kwa hiyo, nimefanya naye kazi kwa karibu sana. Ninafahamu uwezo wake mkubwa wa kuchapa kazi. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, ninampongeza Naibu Waziri, ninampongeza Katibu Mkuu, sasa hivi mwanamke Mwajuma, anafanya kazi nzuri sana katika Wizara hii ya Maji. Tuna imani kubwa sisi wanawake wa Tanzania nzima ambao ndiyo tunatuliwa huu mzigo wa maji kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo niseme tu kwamba, Jiji letu la Dodoma linakuwa kwa kasi sana. Asilimia tano ya ukuaji wa miji hii mikubwa ambayo ndiyo inafanya hata kama *production* inaongezeka, hatuwezi kuona kwa kasi hivyo kutokana na ukuaji wa miji hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamtia moyo mwanangu Mheshimiwa Jumaa Aweso. Aendelee kukazana tu kutafuta vyanzo mbalimbali vya maji. *Dodoma water table* ipo karibu sana. Hivyo wataalam waendelee kufanya *geological survey* waone kila maji yalipo yaweze kutoka kwa ajili ya manufaa ya wananchi wa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, niseme kwamba, Hayati Julius Kambarage Nyerere toka mwanzo alikuwa na nia ya kutoa maji kutoka Ziwa Victoria kuleta Dodoma. Alisema atachimba mfereji mrefu kutoka Ziwa Victoria hadi Dodoma. Azma hiyo amekuja kuitimiza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anataka kutimiza kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wetu, maji ya Ziwa Victoria Dodoma tunayatarajia kwa matarajio yote na ambaye utatekeleza haya ni wewe. Kwa hiyo, sisi tunaona kwamba uandike historia kwenye uongozi wako wa Uwaziri; sasa maji haya yasiwepo kwenye makaratasi tena, yaje Dodoma. Kwa hiyo, kwenye kipindi hiki bajeti hii itakayopitishwa, anza moja kwa moja mkakati wa kuyaleta maji Dodoma. Nina imani kubwa ya kwamba utafanya hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie mambo machache tu kwa ajili ya Wizara yetu ya Maji. Kwanza kabisa tufanye huo utafiti. Kitengo cha utafiti kiwe kikubwa kwa ajili ya kutafiti tunatafiti miamba yetu tunaangalia maji yalipo. Katika utafiti huu wataalam wetu waangalie pia mabadiliko ya tabianchi. Tunasema tunatoa maji kwenye maziwa yetu na mito yetu, lakini wafanye ulinganifu na mabadiliko ya tabianchi. Tusijekuwa tunachukua maji, tunapata maji, lakini tunaharibu pia mazingira yetu ambayo sisi wanadamu tunapaswa kuishi hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo ushauri wangu uelekee kwenye *maintenance*, yaani kwa ajili ya kutengeneza miundombinu iliyochakaa. Upotevu wa maji bado upo 30% mpaka 35%, lakini tukijitahidi tukafika kile kiwango cha Kimataifa cha 25% kwa kufanya ukarabati wa miundombinu. Ninataka niseme pia kwamba, siyo ukarabati peke yake. Sisi hapa Dodoma tuna SAWA *Group*. Hawa ni vijana ambao kila siku wanaangalia maji yanavuja wapi na kutoa taarifa na tunafanya *maintenance*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninampongeza sana Mkurugenzi wangu pia Aron Joseph, anafanya kazi nzuri ya kuzuia upotevu wa maji. Ninaiomba Wizara itenge *emergence funds* na pia itenge *maintenance funds*. Huku tunaongeza *production* huku tunafanya *maintenance,* lakini pia tunazuia upotevu wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ambalo ninapenda kushauri Mheshimiwa Waziri, ninaomba kushauri kuhusu *prepaid meters*; kwa kweli *prepaid meters* peke yake ndiyo suluhisho la jambo hili. Samahani ninamalizia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *prepaid meters* tungekuwa kama *TANESCO,* kwa hiyo hatutapata mambo ya ubambikizaji wa *bills* na vilevile *the same time* tutaweza ku-*maximize profit* ya mauzo yetu ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Silvery Luboja, ajiandae Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba.

**MHE. SILVERY L. SALVATORY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai. Pia ninawashukuru watendaji wa Wizara ya Maji wakiongozwa na Mheshimiwa Waziri Aweso, pia nisimsahau Meneja wangu wa *RUWASA,* ndugu yangu Mapengo kwa kazi nzuri ambazo amekuwa akizifanya kwenye Jimbo la Misungwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa faida ya muda, ninaomba nitambue juhudi kubwa za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na niseme tu kwamba zimeainishwa kwenye ukurasa…

*(Hapa haikusikika kutokana na hitilafu ya kipaza sauti)*

**MHE. SILVERY L. SALVATORY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sasa barabara zifuatazo, Wizara ya Maji ikashirikiane na Wizara ya Ujenzi na mamlaka nyingine za Serikali ili waone na zenyewe zinafanyiwa usanifu wa kina ili ziweze kufanya *operation* nzuri kwenye mradi wa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Barabara ya kutoka Buhingo Nyamainza – Ihelele ina urefu wa kilometa 30, ambayo inatoka Mwanangwa inakuja kuunga kwenye hiyo *junction*. Tunayo Barabara ya Manawa – Kasololo – Mbarika, ina urefu wa kilometa 38.5 ambayo wakati wa masika ziwa huwa linajaa linaziba njia. Kwa hiyo, ninaomba kama tuna nia ya dhati ya hiyo Gridi ya Taifa, tukaweze kuizingatia hiyo barabara na kuihudumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo Barabara ya kutoka Mbarika – Ilujamate – Nhundulu yenye urefu wa kilometa 46.6. Ninaomba hayo yazingatiwe na ninarudia kuishukuru Wizara ya Maji na watendaji wake wote kwa hotuba nzuri na kwa kuainisha miradi yote kama ambavyo imeonekana kwenye ukurasa wa 266 – 268 kwenye Jimbo langu la Misungwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Santiel Eric Kirumba, Mheshimiwa Neema Mwandabila na Mheshimiwa Kafiti Kafiti ajiandae.

**MHE. SANTIEL E. KIRUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninapenda kuipongeza Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Mkoa wa Shinyanga kwa awamu iliyopita, iliweza kutuletea takribani shilingi bilioni 145 za mradi wa maji. Hii inaonyesha kabisa ajenda ya Mheshimiwa Rais kwa Mkoa wa Shinyanga ni kumtua mwanamke ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameweza hii kuitekeleza; Mkoa wa Shinyanga una vijiji 506, mpaka sasa hivi tunavyoongea vijiji 46 tu ndiyo havijafikiwa na mtandao wa maji. Kwa hiyo, nina imani Waziri Mheshimiwa Aweso, tutakapoipitisha bajeti hii, ataweza kutukamilishia mradi huu wa maji katika vijiji vilivyobaki 46. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ninapenda kuipongeza Menejimenti Nzima ya Wizara ya Maji, ukianzia Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *Engineer* Mwajuma, *RM* wetu wa mkoa pamoja na Meneja *KUWASA* Mkoa. Wote wamekuwa ni watu wa kufikia kirahisi tunapopata changamoto yoyote ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea pia kuipongeza Serikali. Kwa Wilaya yetu ya Kahama tulikuwa na changamoto kubwa sana ya maji, hasa hasa kwenye maeneo mengi, lakini Mheshimiwa Rais akaidhinisha fedha. Wakishirikiana na *Barrick* wameweza kujenga chujio la kisasa katika Kata ya Mwendakulima na hii imepunguza adha ambayo ilikuwa

inatokea. Chujio lile la *KASHWASA* likipata shida, wananchi wa Kahama wanakosa maji, ambapo kwa Mkoa wa Shinyanga wananchi wa Kahama ni wengi, walikuwa wanakosa maji pamoja na vijiji vya jirani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana Mheshimiwa Waziri amesema, yeye nyumbani kwake anapata utulivu, lakini sisi wanawake wa Mkoa wa Shinyanga baadhi ya vijiji hatupati utulivu kwa sababu hatupati maji safi na salama kwenye baadhi ya maeneo. Hii huwafanya wanawake wengi kutoka asubuhi kwenda kutafuta maji na maji hayo wanayafuata kwa umbali mrefu sana na hata kulazimika pia kununua maji yale kwa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii imewapelekea wanawake wale hata kushindwa kujishughulisha na shughuli nyingine za kiuchumi kwa sababu wanakwenda kufuata maji umbali mrefu na hii imewafanya wanawake wengi wa Shinyanga pato lao kushuka. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, anapoongelea utulivu na sisi kwetu kwenye ndoa zetu Shinyanga bado utulivu haupo vizuri, tunahitaji maji safi na salama ili tuweze kujihusisha na shughuli nyingine za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakandarasi wengi kwetu wamefanya kazi na Serikali kweli imejitahidi inalipa, lakini, kama kuna miradi mingine haina ulazima kuifanya kwa haraka tusubiri ile ambayo ipo kwa mapema iweze kulipwa. Wakandarasi hawa wanapitia shida sana tunapokuwa tunawaomba watufanyie miradi halafu tukawacheleweshea malipo. Wakandarasi hawa wengine wanakuwa wameshachukua pesa benki, kwa hivyo tunakuwa tumewaletea usumbufu mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakuomba kama Serikali turudi tena tujipange, ile miradi ambayo tuna ulazima na pesa tumeshaitenga ninaomba tuifanye kwa haraka na tuwalipe wakandarasi hawa kwa haraka. Maana hawa wakandarasi ni wananchi wetu, kwa hiyo wanapokuwa wanapitia hii adha ya malipo na kwengine wanaondoka kwenye baadhi ya miradi, inakuwa ni changamoto kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi katika maeneo yale wanaona huu mradi upo, lakini mkandarasi hayupo na wanakuwa na kiu ya kutumia maji na hawana mbadala wa sehemu nyingine wanayoweza kupata maji isipokuwa Serikali yetu inatakiwa iwatimizie kwamba waweze kupata maji safi na salama. Kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa mwaka huu wa fedha akawe na bajeti yake, awalipe hawa wakandarasi wa nyuma kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kusisitiza pia Waziri anafanya kazi nzuri sana na Serikali ya Mheshimiwa Rais imekuwa ikikuunga mkono kwa kiasi kikubwa sana kuhakikisha maji safi na salama yanafika kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Neema Mwandabila; Mheshimiwa Kafiti Kafiti na Mheshimiwa Patali Shida Patali wajiandae.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara yetu hii nzuri ya Maji ambayo kimsingi ni Wizara ambayo ina dhamana kubwa sana kwa maisha ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuungana na wenzangu kuendelea kuwapongeza kwa namna wanavyofanya kazi na kutusaidia kusogeza huduma za maji majumbani kwetu. Kwa kuwa dakika ni chache ninaomba nijielekeze kwenye haya mambo machache: kwanza, ninatamani nimwombe Mheshimiwa Aweso kipekee kabisa kutupatia gari la *RUWASA* kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli katika Wilaya yangu ya Ileje. Hili ninamwomba kwa heshima na kama ningekuwa na uwezo wa kupiga magoti hapa ningempigia, kwa hiyo, ninamwomba sana Mheshimiwa Aweso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ninataka nimpatie taarifa Mheshimiwa Aweso kwamba, tunashukuru kwa fedha shilingi bilioni 5.9 ambazo wamezitoa kwa ajili ya Mradi wa

Momba, Tunduma na Vwawa. Kati ya shilingi 17,000,000,000 ambazo walitakiwa watoe kama fedha za awali tunawashukuru kwa hizo fedha, lakini ninatamani Waziri ajue kwamba pamoja na kwamba amesema mradi unatekelezeka, mkandarasi hajaanza kazi bado mpaka saa hizi pamoja na kwamba wamempa hizo fedha. Kwa hiyo, kipekee pia nimwombe sana Mheshimiwa Aweso, atusaidie huyu mkandarasi kwa hizo fedha alizompatia aanze kazi angalau sisi kama wananchi tupate matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe pia kaka yangu Aweso kwamba, pamoja na kwamba anafanya kazi nzito ya kuhakikisha miradi mipya inaanza, atusaidie tu kulipa madeni ya wakandarasi wetu ambao wameondoka *site,* kazi hazipo. Tuna shilingi 821,000,000 ambayo wakandarasi wameondoka *site* kazi haziendelei. Sasa hii miradi ingetusaidia kusogea kutoka 55% ya maji tuliyonayo kwenye Mji wetu wa Vwawa Mlowo, ingetusogeza tufike angalau 84%. Kwa hiyo, hili nalo pia nimwombe Mheshimiwa Aweso atusaidie. Ninajua, anakuwa na fedha nyingi sana kiasi kwamba shilingi 821,000,000 kwake siyo changamoto kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niendelee kusisitiza kwamba Wizara hii ni ya muhimu, lazima ije na mkakati maalum wa ku-*strategize* yaani ni kama wafanye *reform* au watafute namna bora nzuri yaku-*operate* kutekeleza kazi zao. Hivi tunavyoongea pamoja na hayo maombi niliyomwomba kuna miradi mingi ambayo imesimama kwenye maeneo yetu: unakuta mipira imeenda *site,* lakini hakuna kinachokuwa kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajitahidi kujipanga wanapotoa fedha watoe kwa kulingana kwamba hizi fedha zitahakikisha huu mradi unakwisha. Hiyo ninadhani sisi kama Taifa itatusaidia kuliko hapa saa hizi, sasa huyu anavuta, huyu anavuta, hakuna kinachoendelea. Kwa hiyo, hilo pia ninatamani wakae chini waangalie namna nzuri zaidi, wajipange vizuri zaidi ili kuhakikisha utoaji wa fedha wanavyokuwa wanaupeleka kwenye maeneo yetu uzingatie vigezo vya kuhakikisha miradi iwe *on time*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hilo, niendelee kuomba suala la *cost.* Wanapokuwa wanajenga ile miradi ya maji kuna miradi ya vijijini na miradi ya mijini, kuwe angalau na uwiano wa *pricing*. Siyo kwingine wana-*charge* 300, kwingine wana-*charge* 500, kwingine wana-*charge* 700 na kwingine wana-*charge* 2000. Kwa hiyo, kama wanasema ni miji na kwenye miji tuta-*charge* kiasi Fulani, basi iwe *flat rate* kwenye miji yote. Kama ni vijijini wanasema vijijini tuta-*charge* 500, tujue basi hii ni *flat rate* kwa maeneo yote ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia hata wao kuwa na mpango mzuri wa namna ya kupata mapato. Kuna wakati nilikuwa ninasoma taarifa yao, hii Wizara ndiyo ninaona kama ni Wizara inayopokea fedha nyingi lakini hatuoni wao wanaingiza kitu gani. Kwa hiyo, ifikie hatua wanapokuwa wanapewa fedha wawe wanaoanisha na kiwango wanachokuja kuipatia Serikali yetu fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nisiseme mengi, niendelee kumsihi kaka yangu Mheshimiwa Aweso kwamba suala la Wizara hii anaiweza na anaimudu pamoja na timu yake nzima waangalie tu namna bora nzuri ya kufanya vizuri. Kuna kitu niliwahi ku-*share* naye, suala la Mto Rukwa. Yeye ndiye Waziri wa Maji, ndiye mmiliki wa maji ya Taifa lote hili kama maji yanatusumbua, basi na yeye anatakiwa awajibike kuhakikisha maji hayatusumbui. Sina maana ya kutusumbua kwa maana hayapatikani, lakini pia yanapokuwa yamezidi kwenye maeneo yetu waliangalie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ziwa Rukwa linazidi kutanuka, waangalie namna ya ku-*control* maji ya Ziwa Rukwa, wananchi wanaendelea kupoteza maeneo yao na nini, wakati haya maji yanaweza yakatumika kwa namna iliyo bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga hoja mkono na ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Neema Mwandabila. Nilimtaja Mheshimiwa Kafiti Kafiti; Mheshimiwa Patali Shida Patali na Mheshimiwa Abubakari Asenga Wajiandae.

**MHE. KAFITI W. KAFITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia bajeti hii kutoka kwa Wizara hii ya muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Ilemela, kwanza kabisa nitoe pongezi sana kwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mchango wake mkubwa kwa kuhakikisha anamtua mama ndoo. Ninadhani wote ni mashahidi, Mheshimiwa Rais wakati anaingia alisema moja ya ahadi yake kubwa ni kuhakikisha anamtua mama ndoo na hili limedhihirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Ilemela kiukweli tulikuwa kwenye wakati mgumu, ukiona mtu anaulizia maji ya Ziwa Victoria na wewe upo hapo hapo, lakini hupati maji ilikuwa ni changamoto kubwa. Leo nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu sasa Ilemela inakwenda kung'ara, Ilemela inakwenda kuwa na maji ya uhakika. Kwa hiyo, nimpongeze sana Ndugu yangu, Mheshimiwa Aweso amefanya kazi nzuri sana yeye na wasaidizi wake; Mheshimiwa Kundo na Wizara nzima kwa kweli wanajituma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kutoa pongezi kwa dada yangu Nelly wa *MWAUWASA* anafanya kazi kubwa sana. Kwa hiyo, ninaomba sana kwa nafasi hii niliyopata nitoe pongezi kubwa kwa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu maji ni uhai lakini bila maji binadamu yeyote hawezi kuwa hai na ndiyo maana tunaamini kwamba suala la uwepo wa maji ni suala la muhimu sana katika jamii yetu. Kwa hiyo, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, chanzo chetu cha *Capri Point* amekwenda kukipanua

kutoka lita milioni 90 mpaka lita milioni 144, pongezi sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukaona Ilemela tulikuwa tuna shida kubwa sana ya maji, lakini kutokana na upanuzi huu wanaokwenda kuufanya katika chanzo chetu cha *Capri Point*, Wilaya sasa ya Ilemela tunakwenda kuondokana na tatizo la maji. Ninampongeza, mkandarasi aliniambia zaidi ya shilingi bilioni 4.5 tayari zipo Ilemela mkandarasi anaendelea na utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo bado ameendelea kusambaza mabomba. Tunafahamu kipindi cha nyuma Ilemela iliendelea kuwa na changamoto kubwa ya maji, lakini ninaamini kwa uwepo wako kwa bajeti na pesa ambazo tunakwenda kumuidhinishia Ilemela sasa tunakwenda kuwa salama katika eneo zima la maji. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri, bajeti hii ni bajeti kubwa, lakini tumeweza kuangalia hapa bajeti hii kwa mapato ya ndani ni ya zaidi 30%. Sasa nimwombe kama hatutaongeza bajeti hii kwa kutumia vyanzo vya ndani nina mashaka utekelezaji wa bajeti hii. Kwa hiyo, niombe sana Mwenyezi Mungu aendelee kumtia nguvu atafute pesa nyingi zaidi kuweza kutekeleza hii miradi ambayo Watanzania wanaitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, sisi watu wa Ilemela tunashukuru ametuletea ule mpango wa maji taka kwa wakazi wale wa mlimani, ametupa zaidi ya shilingi 22,000,000,000 kwa ajili ya wakazi wa Lumala, Kiseke pamoja na Pasiansi. Hilo nimpongeze sana kwa sababu tulikuwa tunapata shida, wakati wa mvua tunasema tunafungulia koki watu wa mlimani, sasa Waziri amekwenda kuboresha maisha ya wakazi wa Jimbo la Ilemela, hilo nimpongeze sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba vilevile nimwambie tu na niendelee kumtia moyo, tunafahamu Idara hii wengi tulikuwa tunalia na kubambikizwa bili za maji lakini sasa unakuja kwako na mpango wa *smart meter*. Maana yake ni kwamba tatizo la

kubambikwa bili za maji linakwenda kuwa historia. Kwenye hilo ninampongeza sana Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaona wenzetu wa *TANESCO* sasa hatulalamiki kubambikiwa bili, kwa sababu sasa wameturahisishia. Kwa hiyo, katika eneo la maji, nimwombe sana Waziri aendelee kuweka mkazo huu wananchi waweze kufurahia huduma ya maji wanayoyapata bila kuwa na ubambikiwaji bili. Umbambikaji wa bili umeleta chuki kwa Serikali, umeleta chuki kwa wananchi, umeleta chuki kwa viongozi, kwa hiyo kupitia usimamizi wake tunaamini suala hili linakwenda kwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kuelezea suala lingine la upotevu wa maji. Tumekuwa tunapambana kwa kiwango kikubwa sana kuhakikisha kwamba tunaongeza *speed* ya usambazaji wa maji, lakini sijaona mikakati ya kudhibiti upotevu wa maji. Tumeona taasisi kama *DAWASA* inapoteza maji mengi sana, taasisi kama *MWAUWASA* inapoteza idadi kubwa ya maji. Kwa hiyo, hii ni hasara kwa Serikali, ni hasara kwa wananchi na inaongeza gharama kwa Serikali, kwa hiyo niendelee kumwomba Mheshimiwa Waziri katika eneo hili tuendelee kulipa mkazo mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ni lazima tuwe sasa na mpango, tunasema tuwe na *water budget* kwa kumalizia. Ni lazima tujue mahitaji yetu ya maji ni kiasi gani, matumizi yetu ni kiasi gani. Kwa historia tunaambiwa kwamba Ziwa Victoria lilishawahi kukauka miaka 400,000 iliyopita. Sasa sisi tumejipangaje katika hili? Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri niendelee kumpongeza Waziri, tupo tayari kuhakikisha tunapitisha bajeti yako ili kuleta ustawi wa maisha bora ya watu wa Ilemela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hiyo na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kafiti. Nilimtaja Mheshimiwa Patali; Mheshimiwa Abubakari Asenga na Mheshimiwa Florent Kyombo wajiandae.

**MHE. PATALI S. PATALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kupata fursa hii ya kuchangia hotuba muhimu ya Wizara hii nyeti ya Maji. Awali ya yote, niungane na Wabunge wote waliotoa pongezi kwa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuongeza bajeti ya Wizara ya Maji kutoka shilingi 898,000,000,000 mpaka shilingi trilioni 1.1, hili ni jambo kubwa, ni jambo la kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue fursa hii adhimu niwashukuru na kuwapongeza timu nzima ya Wizara ya Maji ikiongozwa na Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, lakini pia Naibu Waziri wake, kaka yangu Mheshimiwa Mathew Kundo, Katibu Mkuu *Engineer* Mwajuma, *CEOs* na *MDs* wote wa taasisi zilizo chini ya Wizara ya Maji. Kipekee salamu zangu za pongezi ziwaendee maafisa wanaosimamia huduma za maji Mkoa wa Mbeya. Mimi jimbo langu linahudumiwa na taasisi mbili: Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Mbeya *CPA*. Gilbert Kayange pamoja na *Engineer* Hancy Patrick kwa upande wa *RUWASA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijielekeze kwa kusema mambo mawili; hatuwapongezi kwa sababu wapo Wizara ya Maji, tunawapongeza kwa sababu ya kupandisha utoaji wa huduma ya maji kufikia zaidi ya 92.5% mijini na 85.2% vijijini. Pia, tunawapongeza kwa sababu ya kupunguza malalamiko ya wateja kwenye sekta ya maji, jambo ambalo lilikuwa limekithiri miaka ya nyuma. Tunawapongeza kwa sababu ya kuja na mpango mkakati wa Gridi ya Taifa kutatua changamoto ya maji nchi nzima na tunaamini suala hili likikamilika linaenda kuwa mwarobaini wa changamoto za maji nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza kwa sababu wanatupa uthabiti na matumaini ya Watanzania wote kwa kuwa na uhakika wa huduma ya maji kwa sababu maji ndiyo huduma pekee ambayo haina mbadala. Tunawapongeza kwa sababu wanatii maandiko. Ukisoma Kitabu cha Waebrania 13:17 kinasema; "Watiini viongozi wenu, na kushika amri zao, wao huchunga roho zenu usiku na mchana na watatoa ripoti ya utumishi wao mbele ya Mungu, kama mkiwatii watafanya kazi zao

kwa furaha la sivyo watazifanya kwa huzuni." Wao ndiyo wanampa furaha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu hana *stress,* wanaisimamia vyema Wizara ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa pamoja na salamu zangu niseme mambo machache: Mbeya Vijijini, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imetuletea fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Hata hivyo, ninaomba nimwombe Waziri, Mheshimiwa Aweso tuna miradi saba inayoendelea, hii miradi inasuasua tunaomba fedha ili wakandarasi warudi *site* kwa ajili ya kutekeleza mradi. Mathalani Mradi wa Izyra ambao upo 55%; Mbagala Iyunga, Mwakasita upo 50%; Mradi wa Masoko upo 40%; Ilea - Ihango upo 80%; Iwalanje-Tembela 75%; na Isuto kisima pale kipo 95%, tunaomba fedha ili miradi hii ikatekelezeke. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, ninaomba nijikite na nijielekeze kwenye ushauri. Wizara ya Maji kwa mwaka wa fedha uliopita ilikuwa inadai taasisi za Serikali shilingi bilioni 61. Mkoa wa Mbeya tuna Mradi wa Maji wa Mto Kiwira una takribani zaidi ya shilingi bilioni 119. Mradi huu unaendelea vyema lakini tunaamini hizi fedha ambazo tunadai kwenye taasisi zingepatikana leo hii Wanambeya wote na huu mradi unaenda Mbeya Vijijini kwenye kata tano: unapita Swaya, Utengule Usongwe, Nsalala, Kata ya Bonde la Songwe, Iwindi na baadhi ya maeneo ya karibu ya Mshewe. Zikilipwa hizi fedha miradi kama hii ingemalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tukubaliane kuiunga mkono Wizara ya Maji na sisi tumwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu kama Mtendaji Mkuu wa Serikali aziandikie taasisi hizi ziweze kulipa madeni haya ili miradi mingine iendelee kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, kuna utaratibu lazima tukubaliane, umewasilisha na saa hizi tunaelekea kuweka ushirikiano mkubwa na sekta binafsi. Sekta binafsi haijalishi ni mtu mmoja au watu sita, kuna utaratibu kupitia Sheria ya Maji

inayosimamia rasilimali za maji Namba 11 ya Mwaka 2009, kwa wateja kuchimba visima. Utaratibu huu umekuwa na malalamiko kidogo na muda mwingine taasisi kukinzana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mteja anatakiwa aombe kibali cha kuchimba kisima kwenye Bodi za Mabonde, lakini waliokasimiwa kisheria ya kutoa huduma hasa mijini ni Mamlaka za Maji. Sasa Sheria ile inaeleza, mteja apewe kibali mahali ambapo mtandao haujapita. Mheshimiwa Waziri, ninaomba sana uliangalie hili, watekelezaji wa kutoa kibali cha uchimbaji wa kisima wapewe Mamlaka za Maji. Wao ndiyo wanajua wapi hakuna maji, wapi tutapeleka maji na lini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie. Hii itaondoa migongano, lakini pia itaondoa migongano ya taasisi kwa taasisi lakini pamoja pia na wateja kupata huduma kwa haraka kwa kuondoa *bureaucracy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kwa heshima sana kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Abubakari Asenga; Mheshimiwa Florent Kyombo na Mheshimiwa Lazaro Komba wajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara yetu ya Maji. Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Waziri na Watumishi wa Wizara wasihuzunike, sisi tunasema ni mambo makubwa ya kuomba miradi, kuomba maji, kuomba fedha na madhali wanafanya kazi kwa bidii, Mwenyezi Mungu atawasaidia. Sisi tunawaombea Mwenyezi Mungu awasaidie wapate fedha, watusaidie kwenye miradi hii mikubwa ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa, kama kawaida yangu, kusema mambo mawili; kwanza kushukuru na kuomba tena, kama wananchi wa Kilombero walivyonituma. Leo nimepokea simu ya Mwalimu wangu wa Kiswahili, anaitwa Joram Mkumbi, Mzee wa Ulumbi, ameniambia nimeona *video TikTok*,

Ifakara inafumuliwa mitaro. Wanataka kufanya nini Ifakara? Nikamwambia Mwalimu Joram Mkumbi, ile si mitaro. Yale ni mabomba makubwa ya Mradi wa Maji wa Kiburubutu wa shilingi bilioni 45 ambazo Halmashauri ya Mji wa Ifakara imepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoingia kwenye uchaguzi Mwaka 2020, tuliahidi jambo hili. Nina mambo makubwa ya lami na mradi huu wa maji, Wakati tunasema Chama Cha Mapinduzi tunaomba kura, wananchi waliona kama hadithi, pengine tunadanganya; leo matenki kule yamefika karibu 70% na Ifakara Mjini pale, kata zote tisa za Tarafa ya Ifakara, watu wanaona mji unafukuliwa mabomba ambamo binadamu anaweza akatembea, yanapita Ifakara Mjini kwenda kusambaza maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais Samia kwa mradi huo mkubwa. Sasa Mwalimu wangu wa Kiswahili akasema, maneno ya Kiswahili yapo haba kwenye kushukuru, akasema ukienda pale, simama kwa turuhani na urua, mshukuru Waziri, mshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Maji, Injinia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwambia Mheshimiwa Waziri, miezi miwili iliyopita Injinia aliniazimia eskaveta tukaenda kuboresha tuta pale Ifakara. Kama si Katibu Mkuu wa Maji kunipa lile eskaveta, basi leo athari ya mafuriko ingekuwa kubwa sana katika Mji wa Ifakara. Ninamshukuru kwa kiasi kikubwa sana kwa hiyo, nimesimama hapa kutoa shukrani belebele, shukrani teletele na shukrani *jazira* kwa kazi kubwa, ambayo Mheshimiwa Waziri ameifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amekuja jimboni kwangu, nimemwambia kuhusu ule mto, amefika ametembea. Sijawahi kuona Waziri anatembea kwa mguu porini kwenye vichaka, karibu kilometa nzima, anaenda kuona sehemu ambako mto umezibwa. Waziri mwingine angebaki kwenye gari tu, lakini ametembea kwa mguu, amefika mtoni, ameona namna mto ule ulivyoziba. Nisimkushukuru kwa kweli, nitakuwa mchoyo wa fadhila. Sasa ninaomba nini Mheshimiwa Waziri, kwa sababu, dakika ni tano?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni hilo la ule mto aliouona. Wizara ya Kilimo wanataka kujenga mabwawa na skimu za umwagiliaji. Ule mto, Wizara ya Nishati wanautaka kwa sababu, unamwaga maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere. Sisi tuna kilometa takribani tatu au nne kutoka Kibaoni mpaka Lipangalala. Mheshimiwa Waziri, ninavyozungumza naye kuna wananchi zaidi ya 100 wako Shule ya Msingi Lipangalala baada ya nyumba zao kujaa maji kwa sababu, mto ule umejaa uchafu, umejaa takataka. Maji kidogo tu, mvua kidogo, maji yanamwagwa kwa wananchi na lile tuta la zamani limeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea na Mamlaka ya Bonde, nimeongea na Katibu Mkuu ameniambia atanisaidia na wewe nisaidie vifaa ama pesa kidogo zikakae pale zifukue mto ule, zirejeshe yale matuta, yale maji yakamwagwe Mto Kilombero yaende Bwawa la Mwalimu Nyerere. Ni maji muhimu sana kwa nchi yetu. Ninazungumza katika hali ambayo Waziri mwenyewe amefika na ameona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hilo ni jambo la msingi sana. Sitamani kwenda kushika shilingi yako Mheshimiwa Waziri kuhusu jambo hili. Wananchi wa Ifakara leo, wa Jimbo la Kilombero, wanaangalia Mbunge atasema nini kuhusu mafuriko tuliyoyapata au kazi yake ni kutuletea unga tu? Sasa haiwezi Wizara nzima, Mheshimiwa Waziri Juma Aweso na Mwenyekiti wa Mkoa, Msisimbi, wakakosa eskaveta na ma-*tipper* mawili kukaa pale kufukua mto ule? Mwenyezi Mungu ambariki atusaidie jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, ninaomba shilingi 60,000,000 tu, maji ya Kidatu *Solar Station* ni machache. Nimeongea na Meneja mzuri wa *RUWASA,* anaitwa *Engineer* Mlelwa, Kilombero akasema tukipata shilingi 60,000,000 tu pale Kata ya Kidatu, Msolwa *Station* wataongezewa maji. Ameniambia wamefanya upembuzi yakinifu kwa Mradi wa Iyanga na Lumemwe yote kupata maji, shilingi 680,000,000 zinatakiwa na tenki pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna matenki pale Mradi wa Barabara; wale Waisraeli wameacha matenki makubwa. Yale matenki yanataka mnara ili tuyatumie kuleta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, siyo kwa umuhimu, ninaomba shilingi 67,000,000 za ukarabati wa Mradi wa Maji wa Mwaya, katika Kata ya Mwaya yenye watu wengi pia. Mwaya kuna watu 40,000 wanahudumiwa na mradi huo. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri anisaidie mambo hayo. Mungu ambariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Abubakari Asenga. Nilimtaja Mheshimiwa Florent Kyombo na Mheshimiwa Dkt. Lazaro Komba. Mheshimiwa Emmanuel Khambay, ajiandae.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia Wizara ya Maji. Ninasema leo sikutaka kuchangia Wizara hii, lakini imebidi nisimame kutoa ushuhuda wa kazi nzuri ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ushuhuda wa ndugu yangu Waziri Aweso, ambaye amekuwa kwenye Wizara hii akihudumu vizuri pamoja na wasaidizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo matatu. Kwa ufupi nitatoa ushuhuda, nitaomba, lakini mwisho nitashauri. Pongezi za kwanza za dhati ziende kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tunaona nia yake ya dhati ya kubadilisha wananchi wake ndani ya Tanzania kwa kuhakikisha kwamba, kila mmoja anapata maji. Hii inakuwa *reflected* kwenye bajeti, kutoka bajeti iliyopita ya shilingi 898,000,000,000 na leo tunaenda kwenye shilingi *1.12 trillion,* kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji. Ni pongezi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza viongozi waandamizi wanaomsaidia Mheshimiwa Rais; Mheshimiwa Dkt. Balozi Emmanuel Nchimbi pamoja na Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba kwa kuendelea kumshauri Mheshimiwa Rais vizuri.

Pongezi za dhati ziende kwa askari wake wa mwanvuli, ambaye ni Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Ndugu yangu Mheshimiwa *Engineer* Kundo, pamoja na wasaidizi wao, wakiwa na Mtendaji Mkuu, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, lakini na viongozi wa Taasisi ya *RUWASA,* bila kumsahau Ndugu yangu *Engineer* Krita na Wakurugenzi wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mikoa yetu tunaona tunao wasaidizi wao, wanafanya kazi kubwa na kwa ueledi. Kwa Mkoa wa Kagera tunaye ndugu yangu Warioba Sanya, lakini kwenye wilaya yangu tunaye *Engineer* Robert, ambao wanaendelea kufanya kazi pamoja na watumishi wengine wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema Wilaya ya Misenyi inasimamiwa na taasisi mbili, chini ya Mheshimiwa Waziri Aweso; pamoja na *RUWASA* tunayo *BUWASA*. *BUWASA* yenyewe inaendelea kufanya kazi nzuri chini ya Ndugu yangu John Slatt, ambaye ni Mkurugenzi na kijana wake Mheshimiwa Aweso, ambaye ni *Engineer* Lucas Mbaga ndani ya Wilaya ya Misenyi, anafanya kazi nzuri kusimamia Mradi mkubwa wa Maji kutoka Chaka – Bunazi mpaka Kasambya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushuhuda wangu wa kwanza ni, katika historia tangu nchi imeumbwa Wilaya ya Misenyi, kata 15 zilikuwa hazina maji, lakini ndani ya kipindi cha miaka mitano kwa ushuhuda huu, ndani ya Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kipindi cha Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, kata 15 sasa zina maji. Maji yanaendelea kusambaa na wananchi wangu wa Wilaya ya Misenyi waendelee kuvumilia, yale maeneo machache ambayo maji hayajafika katika hizo kata 15 yataendelea kusambazwa kwa sababu, jumuiya za watumia maji zinaendelea kufanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ninaomba, Mheshimiwa Hamidu Aweso, katika kata tano zilizobaki; Kata ya Minziro, Kata ya Bugorora, Kata ya Bugandika, Kata ya Bwanja na Kata ya Kakunyu, tuimarishe. Tuhakikishe na zenyewe sasa zinapata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushuhuda wangu wa pili ni vyanzo vya maji ndani ya Wilaya ya Missenyi. Missenyi tumebarikiwa kuwa na vyanzo vya maji, tunalo Ziwa Victoria ambalo linazunguka Wilaya ya Missenyi, tunao Mto Kagera na Mto Ngono. Hii yote ilikuwa haijawahi kutumika kwa hiyo, sasa tunaona historia imeandikwa, kote maji yamefika kutoka vyanzo hivyo. Namwomba sasa, Mheshimiwa Aweso, ndani ya wilaya yetu maeneo yaliyobaki yote miradi ifike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Eneo la Mtukula kuna Mradi mkubwa wa *BUWASA*, mkandarasi anadai fedha, mradi uko 70%. Ninaomba alipwe shilingi 929,000,000 amalizie, lakini ninakushukuru kwa fedha shilingi milioni 200 maeneo ya Bwengabo, Biyawala, Kagarama, Kashaba mpaka Buliyambo Kona, fedha zimefika tunaendelea kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Lazaro Komba, ataufata Mheshimiwa Emmanuel Khambay; Mheshimiwa *Engineer* Amosy Maganga na Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, wajiandae.

**MHE. DKT. LAZARO K. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia katika hotuba hii ya Bajeti ya Wizara ya Maji. Ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi hii ya uhai na afya njema aliyonipatia iliyoniwezesha kupata kibali cha kusimama hapa kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Peraminho, ambao kimsingi wamenituma nije nizungumze habari ya maji katika vijiji vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mama yetu kipenzi cha Watanzania, kwa kazi kubwa aliyoifanya katika Jimbo la Peramiho. Miaka mitano iliyopita sisi wananchi wa Jimbo la Peraminho tulikuwa tunapata maji kwa 67.7%, lakini leo tunavyozungumza mpaka sasa tumefika 79.3%. Haya ni mafanikio makubwa na tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Peramiho wana utamaduni wa kushukuru, lakini huwa wanaamini kushukuru ni kuomba tena. Sisi tunaomba tena katika maeneo matatu; eneo la kwanza, tunaomba miradi ile ambayo tayari ilikuwa imepatiwa fedha zaidi ya shilingi 4,451,000,000 ilianza utekelezaji na iko katika vijiji sita, lakini imesimama kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali na kwa bahati nzuri ndugu yangu Mheshimiwa Waziri yuko hapa ananisikia. Miradi iliyoko katika Kijiji cha Mpandangindo, Kijiji cha Makwaya, Kijiji cha Maleta, Kijiji cha Liweta na Kijiji cha Mdunduwaro, maeneo haya yamekuwa na changamoto kwa muda mrefu, lakini ipo miradi ambayo utekelezaji wake ulikuwa umesogeasogea kwa kiwango kikubwa, ukiwemo wa Kijiji cha Kitulo. Ninaomba sana, Mheshimiwa Waziri, Serikali iweze kutupatia katika bajeti hii fedha iliyobaki, ili kukamilisha, maji yaliyo safi na salama yaweze kupatikana kwa wananchi takribani 17,565 katika vijiji hivi sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko vijiji viwili vilivyokuwa na miradi ya maji. Miradi ile chakavu kwa sababu, vijiji hivi vipo tangu mwaka 1960 na miradi hii ilikuwepo tangu wakati huo, kabla hatujapata uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiko Kijiji cha Mpitimbi A na kiko Kijiji cha Magazini. Vijiji hivi idadi ya watu imeongezeka, imekuwa kubwa sana. Ninaomba sana sasa Wizara yetu ya Maji itusaidie kufanya ukarabati katika maeneo haya ili wananchi hawa waweze kupata maji yaliyo safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema tu ninakushukuru sana kwa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Lazaro Komba. Tuendelee na Mheshimiwa Emmanuel Khambay, atafuata Mheshimiwa *Engineer* Amosy Maganga; Mheshimiwa Agnes Lambert, Mheshimiwa Thomas Kampala na Mheshimiwa Fadhili Chilombe, wajiandae.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara yetu ya Maji, ambayo ni Wizara muhimu kwa nchi yetu. Ninatumia nafasi hii, kwanza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Dhamira yake ya dhati kabisa ya kuhakikisha anamtua mwanamama ndoo kichwani ameitekeleza kwa vitendo katika maeneo mengi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo ni mchakato. Tunajua kwamba, zipo changamoto, lakini kwa namna ambavyo bajeti hii ya zaidi ya shilingi trilioni moja tukiipitisha, sisi Wabunge wote leo, ni dhahiri fedha hizo zikisimamiwa kwa weledi zitakwenda kutatua changamoto ya maji katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda nitajikita kwenye mambo machache. Kwanza, ninaipongeza Wizara, kupitia Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kubuni Mpango mzima wa Gridi ya Taifa ya Maji. Ninaamini ukikamilika utakwenda kutatua changamoto ya maji katika maeneo mengi nchini, lakini pamoja na ubunifu huo, ninapenda kuishauri Wizara kujikita katika mfumo wa kutumia mita janja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mita janja itasaidia, kwanza Wizara yenyewe kupitia wasaidizi wenu, kuweza kusimamia upotevu wa maji nchini. Katika mitandao yetu yote ya maji nchini tukiweka mfumo huu utasaidia kudhibiti maji yasipotee na Serikali iweze kuendelea kupata fedha ambazo zitaendelea kusaidia miradi mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la mita janja litatusaidia hata katika maeneo mengine ambayo wananchi wamekuwa wakibambikiziwa bili za maji kwa sababu, mwananchi ataweza kununua maji kama anavyonunua vocha, kama anavyonunua umeme. Hivyo itakuwa ni *pre-paid*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii, wanasema asiyeshukuru kwa yai hata akipewa kuku hatashukuru. Sisi watu wa Jimbo la Babati Mjini tunaishukuru Serikali, chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa miradi mbalimbali ambayo ipo

katika Jimbo la Babati Mjini. Hapa karibuni tumepata miradi ya visima katika Kata ya Bonga, Kata ya Singe na Kata ya Nangara, ambayo tunatazamia gari hilo likitoka upande wa Babati Vijijini litaelekea Babati Mjini na kuendelea kuchimba visima katika maeneo hayo na wananchi waendelee kupata huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kuipongeza Serikali kwa kutupa Mradi wa Mto Eri, Maisaka, Eneo la Sawe, ambapo tenki kuu litakwenda kujengwa na kuweza kuhudumia Eneo la Maisaka, Katani, ambako Mji wa Babati ndio unakoelekea. Ninamwomba Waziri wa Maji, zile shilingi 16,000,000,000 katika hii shilingi trilioni 1.2 ambayo tunakwenda kuidhinisha leo, fedha zitoke kwa sababu, utaratibu wa ujenzi au mchakato wa maji umeanza. Tunamwomba Waziri atupatie fedha hizo, ili mradi uweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatumia nafasi hii kuipongeza Wizara ya Maji, ndiyo Wizara pekee inayotumia mfumo wa *Force Account* na kuonesha *performance* ya hali ya juu nchini. Hivyo, ninawaomba katika miradi ambayo imesalia, Mradi wa Maji Taka wa Babati muweze kusaidia kuukamilisha. Tunashukuru wametoa shilingi 700,000,000 lakini mkandarasi anahitaji shilingi bilioni 1.9, ili aweze kurudi *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba waweze kutupatia fedha hizo, ikiwezekana kabla ya Bajeti ya Mwaka Mpya wa Fedha wa Serikali kuja, ili mkandarasi aweze kurudi *site* na fedha ambazo Serikali imetoa ziweze kuonesha thamani, tuone *best value for money* na wananchi wa Jimbo la Babati Mjini waendelee kunufaika na huduma ya maji taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, ninaomba kuunga mkono hoja kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Mkurugenzi wangu wa Maji, Iddi Msuya, pale Babati. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Amosy Maganga; Mheshimiwa Asia Halamga na Mheshimiwa Thomas Kampala wajiandae.

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kabla sijaanza mchango wangu ninaomba, kwanza nilete salamu za wananchi wa Mji wa Sikonge wenye kata mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa kupitia kwa Madiwani wao, Mheshimiwa Joyce Ng'amba wa Kata ya Mishen na Mheshimiwa Hamisi Saidi Kumba wa Kata ya Sikonge, wanaleta shukrani zao za dhati na za upendo kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuwaondolea kero ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa sasa wanapata maji ya uhakika kutoka Ziwa Victoria. Wanachokiomba sasa ni Mheshimiwa Rais aweze kufika kule Sikonge, ili yeye mwenyewe aweze kuuzindua huo mradi. Mwisho wa shukrani hizo kutoka kwa wananchi wa Sikonge, ninaomba sasa ili niweze kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, ninaanza kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa anayoifanya. Leo tunavyoongea wananchi wa Sikonge takribani 68% tayari wana miundombinu na vilevile wana maji. Kuna changamoto ndogondogo ambazo zipo kule, wakati mwingine maji hayatoki kama jinsi ambavyo wanavyotaka, lakini tunasema safari ni hatua. Ninaamini kuna siku wananchi wote wa Skonge watapata maji ya uhakika, saa 24 kwa siku saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana vilevile Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri amefika kule Sikonge akashuhudia tone la kwanza la maji yaliyotoka Ziwa Victoria, ambayo ndiyo mwanzo wa Gridi ya Taifa. Ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Maji, ninawapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mradi wa Maji kutoka Ziwa Victoria umepita, lakini ninamwambia Mheshimiwa Waziri kwamba, kuna kata takribani tisa ambazo ziko ndani ya kilometa

12. Nilipopita wakati ninamwombea kura Mheshimiwa Rais, pamoja na mimi mwenyewe na Madiwani, niliwaambia kwa uthabiti na kwa ujasiri kwamba, wasiwe na wasiwasi Mheshimiwa Mama Samia atawaletea maji kwa sababu, bomba linapita hapo katikati yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata hizo ni pamoja na: Pangale, Mpombwe, Igigwa, Kisanga, Tutuo, Mole, Mkolye, Chabutwa pamoja na Kata ya Ipole, hawa wananchi toka juzi wananipigia simu, tena wengine kwa machozi kabisa na nikawaambia machozi yenu ninayabeba na nitayafikisha kwa Mheshimiwa Aweso na ninaamini Waziri atakapokuwa ana-*wind up* atakuwa na jambo la kuwaambia wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, …

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. AMOSY W. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nimeshachangia kwa maandishi utayaona, basi ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Agnesta Lambert, atafuata Mheshimiwa Thomas Kampala; Mheshimiwa Fadhili Chilombe, Mheshimiwa Twaha Mwakioja na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika wajiandae.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili jioni ya leo niweze kuchangia kwa ufupi katika hii bajeti ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza kabisa niungane pamoja na Wabunge wengine ambao wamempongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na jitihada njema ambazo anazionesha kwa upande wa maji kwa maana ya kumtua mwanamke ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza kwa sababu ndani ya Jimbo langu la Segerea mpaka hivi ninavyoongea tayari tumepata tabasamu kutoka kwa Mheshimiwa Rais, kwani tumeweza kuchimbiwa visima vitatu ndani ya Kata tatu, Kata ambazo zilikuwa hazina maji kabisa, lakini hivi ninavyoongea, siku chache zijazo Kata ya Kimanga, Kata ya Kisukuru na Kata ya Segerea watakwenda kupata maji baada ya kuwa wameyakosa maji kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpongeza Mheshimiwa Rais, ninaomba kwa haraka sana niende kumpongeza Waziri Aweso pamoja na timu yake. Niseme ninaunga hoja bajeti hii ambayo Mheshimiwa Aweso ameiwasilisha kuanzia siku ya jana na ninaiunga mkono kwa sababu, imebeba ndoto za Mheshimiwa Rais za kumtua mwanamke ndoo kichwani, wakiwemo wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam, hususan wanawake wa Jimbo la Segerea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka pia niipongeze timu nzima ya *DAWASA,* Mkoa wa Dar es Salaam chini ya mtu bingwa kabisa *Engineer* Bwire kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam tunapata maji safi na salama. Kwa ajili ya muda ningeweza kuwapongeza hata mameneja wangu wa Jimbo la Segerea, lakini itoshe kusema kwamba kazi yao ni kubwa na ninawashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa ambao wananipatia mpaka hivi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Segerea lina Kata 13, Mitaa 61. nimekuwa nikisema ndani ya Bunge hili na uzuri Waziri amekuja ndani ya Jimbo la Segerea, amejionea kwa macho, tulitembea mguu kwa mguu aliona jinsi gani ambavyo wananchi wa Jimbo la Segerea wana uhaba mkubwa wa maji safi na salama. Kwa sababu hii Mheshimiwa Waziri, uhaba wa maji ndani ya Jimbo la Segerea una sababu nyingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ya kwanza, ukiangalia takwimu ya uzalishaji wa maji kwa sasa takwimu zinasema

kwamba uzalishaji ni ujazo wa lita 534,000,000 kwa siku, wakati mahitaji ya Mkoa wa Dar es Salaam ni lita 750,000,000 na ukiangalia hapa ina maana kuna pungufu ya lita 216,000,000. Waziri ni wazi kabisa mapungufu haya, ndiyo yanayopelekea wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam na hususan Jimbo la Segerea tusipate maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua upo mpango mkubwa kabisa wa Mheshimiwa Rais kutoka kwenye mradi mkubwa wa Kidunda. Ninaipongeza Serikali kwa sababu itakwenda kusaidia kwa sehemu kubwa kwa maana kipindi cha ukame, wananchi wa Mkoa wa Dar es Salaam wataweza kupata maji safi na salama. Kutokana na huo upungufu ambao nimeusema Mheshimiwa Waziri, ningeomba kwa haraka haraka ule Mradi wa Rufiji uwekewe kipaumbele Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu wazi kabisa kwamba ni pesa nyingi inahitajika, lakini wengine wamesema kwamba pasipo maji hakuna uhai kwa sababu uhai ndiyo maisha. Hivyo Mheshimiwa Waziri hatuna budi kuwekeza katika uhai kwa kuwapatia wananchi maji safi na salama. Hivyo, niishauri Serikali ya Mama Samia Suluhu Hassan, Serikali ambayo ninajua kwamba ni sikivu kabisa iweze kuwekeza nguvu kubwa kwa ajili ya ule Mradi wa Rufiji, ili sasa wananchi wa Jimbo la Segerea na Mkoa wa Dar es Salaam kiujumla tuweze kupata maji safi na salama tofauti na jinsi ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema zipo sababu nyingi zinazopelekea Mkoa wa Dar es Salaam tusipate maji safi na salama, nyingine ni ubovu wa miundombinu. Mheshimiwa Waziri anafahamu tumekwisha kuongea sana, Jimbo la Segerea miundombinu ni chakavu inahitaji kubadilishwa. Hata ukiangalia kwenye Kata zote kule, yale mabomba tu yaliyotandikwa kule chini ni vile vibomba vidogo kabisa ambavyo, hata ukiyafungulia maji, namna gani maji yanakuja kwa presha ndogo kwa sababu watu wamekuwa ni wengi, *demand* ni kubwa, viwanda ni vingi na kwa sababu hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, chonde chonde tunaomba uboreshaji wa miundombinu ndani ya Jimbo la Segerea na Mkoa wa Dar es Salaam kiujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninaleta ombi kwako Mheshimiwa Aweso. Nimwombe wakati tunasubiria mradi huu mkubwa wa Kidunda pamoja na Rufiji na kwa sababu wananchi wa Jimbo la Segerea hatupati maji kabisa katika maeneo mengi, niko chini ya miguu yako Mheshimiwa Aweso, aende akatuchimbie visima kimoja katika kila Kata, ili wananchi wa Jimbo la Segerea, Mheshimiwa Waziri waweze kupata maji safi na salama huku wakisubiri mambo makubwa ambayo Serikali inayapanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya muda ninaomba nimalize kwa kusema, kaka yangu Mheshimiwa Aweso anaupiga mwingi, yeye na timu yake nzima. Jana wakati anahutubia aliona makofi mengi ndani ya hili Bunge siyo kwamba ni unafiki, mimi mwenyewe nilipiga makofi mpaka mikono ikaumia kabisa, ni kwa sababu yeye ni msikivu, lakini pia hapandishi mabega pale ambapo tunakwenda kwake kwa ajili ya kuhitaji huduma. Mheshimiwa Aweso Mwenyezi Mungu ambariki, lakini nitaomba wakati ana-*wind up* aniambie kaka yangu mpendwa je, visima atatuchimbia ndani ya Jimbo la Segerea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Thomas Kampala; Mheshimiwa Fadhili Chilombe, Mheshimiwa Twaha Mwakioja na Mheshimiwa Deodatus Mwanyika wajiandae.

**MHE. THOMAS K. MAGANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Maji. Ninaomba ku-*declare interest,* mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya na kwa ongezeko kubwa la bajeti. Mwaka 2021 bajeti ilikuwa ni shilingi 697,000,000,000 leo tunavyoongea Mwaka wa Fedha 2026/2027 ni shilingi trilioni 1.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ni kubwa sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. Watanzania tunayo kasumba moja, huwa hatumpongezi mtu akiwa kwenye nafasi, huwa tunasubiri mpaka atoke. Mheshimiwa Rais huko aliko Mama akae kwa kutulia. Ninaamini baada ya kuondoka mwaka 2030 hawa hawa leo ambao hawazioni kazi zake, watampongeza wala asiwe na wasiwasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, yeye na timu yake wanafanya kazi nzuri sana. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri ameitoa Wizara hii mbali, miaka tisa kwenye wizara hii iliyokuwa na changamoto nyingi na ametoboa. Ndugu yangu ni kidume, afanye kazi na sisi Wabunge tuko nyuma yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu wa tatu wa kumpongeza kwenye wizara hii ni dada yangu *Engineer,* Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, dada yangu, anafanya kazi kubwa sana ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri. Ninataka nimwambie dada yangu huko aliko apokee maua yake na ninataka nimwambie; ninaamini kwa kazi kubwa anayowasaidia akina mama wa nchi hii, ana kiti chake mbinguni. Kama Mheshimiwa Katibu Mkuu huko aliko apokee maua yake, dhambi zake nipewe mimi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nichukue fursa hii pia kuwashukuru watendaji wote *DG* wa *RUWASA* anafanya kazi kubwa sana kaka yangu. Sisi tulioko vijijini ndiyo tunajua umuhimu wa *RUWASA*, *DG* anafanya kazi kubwa nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti iliyopita mimi ni Jimbo la Katavi nimepata shilingi 8,000,000,000. Kati ya shilingi 8,000,000,000 nilizopata shilingi 4,000,000,000 tayari zipo kwenye miradi na miradi inaendelea. Shilingi 8,000,000,000 niliyoipata inakwenda kutekeleza miradi ifuatayo:-

Mradi wa Nsenkwa, Inyonga shilingi bilioni 1.5, mradi wa ujenzi wa Kamsisi, Nsenkwa, Inyonga, Ilela shilingi bilioni 2.8, ujenzi wa mtandao wa maji vijiji nane, ujenzi wa utumiaji wa maji Ilunde

shilingi milioni 700.3 na hivi ninavyoongea kuna mradi unaendelea kwenye Kata ya Kamsisi, Kijiji cha Imalauduki. Kazi yangu leo mimi ni moja tu kwa hizi raha anazonipa Mheshimiwa Waziri kwenye maji, kusukuma jahazi ili kazi kule ziendelee kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, wakati Rais anapita kufanya kampeni 2025, tulimwambia sisi wananchi wa Jimbo la Katavi tutampigia kura kama tumechanganyikiwa na sababu mojawapo tuliyokuwa nayo ni hii kwenye huduma za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimwombe sana Waziri kwa unyenyekevu mkubwa sana atakapokuja ku-*wind up* ninaomba atueleze wana mpango gani na kusukuma mtandao wa maji, Gridi ya Taifa ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo kwa sababu raha zimenizidi, ninataka nimwambie Mheshimiwa Waziri ninamshukuru sana, Bwawa la Nzengo linakwenda kwa kasi sana na ajitahidi baada ya kukamilika aje alifungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, ninasema ahsante sana, wamsalimie Mama Samia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Fadhili Chilombe, atafuta Mheshimiwa Twaha Mwakioja; Mheshimiwa Deodatus Mwanyika na Mheshimiwa Emmanuel Nuwas wajiandae.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Nimechangia kwa maandishi kwa hiyo hapa nitafanya mambo mawili tu; nitatoa shukrani na kutoa ushauri kidogo. Shukrani zangu za dhati ninaomba zimfikie Rais kama wanavyosema wenzangu, kazi inafanyika na tunaiona. Kwa namna ya pekee kabisa na kwa unyenyekevu mkubwa, ninaomba niwashukuru Waziri wa Maji, Naibu Waziri pamoja na Katibu Mkuu, pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninawashukuru kwa unyenyekevu? Wakati ninaingia kwenye Bunge hili kwenye Jimbo la Tunduru Kusini ninakotokea, kuna jumla ya miradi mitano imekwama kabisa. Miradi hii ni Tuwemacho, Msinji, Masugulu, Misechela na Mradi wa Igoma. Hii miradi ilikuwa imekwama kabisa kwa sababu ya changamoto ya fedha. Nilipokuja hapa nilimfuata Naibu Waziri, Waziri hakuwepo, watu hawa ni wasikivu sana, ninaungana na watu wote wanaowaombea kheri hawa watu. Waliniita tukaenda tukafanya mkutano kwenye ofisi zao pale pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara, tunajadili *issue* ya Tunduru. Wametoa *commitment* yenye mwelekeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ninavyoongea leo hawa watu wametoa jumla ya shilingi 200,000,000 kwenda kuanza kukwamua Mradi wa Tuwemacho, zaidi ya yote tumewekeana utaratibu kwamba Bunge hili likiisha kazi ya kwanza inayoenda kufanyika ni kwenda kuzindua ule mradi, wameenda mbali zaidi wametoa na gari jipya kwa ajili ya Wilaya ya Tunduru. Hawa watu tunawashukuru mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizi ninaomba nitoe ushauri, watu wameongea sana hapa habari za vyanzo vya maji na mambo mengi yameongelewa, lakini kwenye chanzo hapo kuna kitu ninataka nishauri. Dunia hii watu wanaongezeka na ardhi haiongezeki, haya maji tunayoendelea kuyatumia ni yale yale, lakini kuna chanzo kimoja ninaona hakiongelewi sana. Serikali pamoja na jitihada zote inazozifanya za kuwekeza kwenye maji, ninashauri ianze kufanya *sensitization* ya kuwafanya watu waweze kuvuna maji ya mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kitu hakieleweki, unaweza ukaenda kwenye eneo mfano labda Mkoa wa Morogoro pale, kuna kipindi watu kila mwaka wanahangaika na mafuriko, sasa kinachoshangaza ni kwamba, wiki hii wanahangaika na mafuriko, mafuriko yakiisha, wiki ijayo wanasema sisi hatuna maji. Hivi vitu haviumani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukijenga nyumba kwa mfano, yenye upana wa mita tatu, urefu wa mita tisa, ukaezeka, lile bati

kule juu linakuwa na upana wa *square metre* 38. Chukulia mfano hiyo nyumba umeijenga Dodoma, tafiti zinaonesha kwamba Dodoma ndiyo sehemu ambayo inapata maji kidogo, lakini kwenye tafiti pale inaonesha kwamba Dodoma *average* ya mvua inaonesha ni mililita 556.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu aliyejenga nyumba hiyo yenye urefu nilioutaja, mvua ikinyesha Dodoma, akiyavuna yale maji anapata lita zisizopungua 21,128, ambazo ukilinganisha na tafiti zinavyosema, kama ile nyumba imejengwa kijiijini na mtu akavuna maji maana yake ni kwamba, atakuwa na uwezo wa kupata maji ambayo anaweza kuyatumia siku 444, sawasawa na karibu mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huo huo….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fadhili ninakushukuru. Mheshimiwa Twaha Mwakioja, Mheshimiwa Deodatus Mwanyika na Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas wajiandae.

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie nafasi hii kukushukuru kwa nafasi hii.  Pili, nitumie nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya na uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie tena nafsi hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ambavyo anaendelea kuitendea mema na kuwatendea mema Watanzania. Mambo anayoyatenda yote, viashiria vyote vya kiuchumi na vya kijamii vinaonesha *positive trend.* Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kumshukuru, kumpongeza na kumwombea Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtume wetu Muhammad *(S.A.W)* anasema kwamba mtu yeyote atakayewafanyia wema, basi tumlipe mithili ya wema anaotufanyia na kama itatokea kushindwa kumlipa kwa wema huo, basi tumwombee Mungu. Mimi binafsi na wananchi wenzangu wa Mkinga na Watanzania wengine tunaendelea kumwombea Mungu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wema mwingi anaotutendea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue pia nafasi hii kumpongeza sana Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Juma Aweso, Ndugu yangu huyu ni mtu rahimu sana, ni mtu mnyenyekevu sana, ni mchapakazi sana na kwa kweli ndani ya Wizara yake wanaishi kama familia. Ukimwangalia *Engineer*, dada yangu huyu wa Kinyamwezi ni mtu mwema sana, anatusaidia sana na Wizara hii ina mwenezi kwa namna wanafavyofanya kazi, ninawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie katika maeneo matano kwa haraka haraka. Eneo la kwanza, nizungumzie suala la Gridi ya Taifa. Kwa kweli suala hili Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana, limekuja wakati sahihi, limekuja katika mazingira sahihi na mahitaji ya wakati wa sasa, tunahitaji hasa kuwa na gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wilaya yetu ya Mkinga haijajumuishwa katika mpango huu wa gridi ya Taifa, nimwombe Waziri kwa unyenyekevu mkubwa, wananchi wenzangu wa Wilaya ya Mkinga, hususan wa Tarafa ya Maramba, wanasumbuka sana na hali ya upatikanaji wa maji safi na salama, hususan kipindi cha kiangazi. Waziri atufikirie kama mradi huu unafika Muheza, mradi huu unafika Korogwe, mradi huu umefika Pangani na sisi watu wa Mkinga chonde chonde, ndugu zangu wa Maramba hawatanielewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshaliongea hili sana, ninaomba atakapokuja Mheshimiwa Waziri, kaka yangu sina maneno mengi ya kumwambia, lakini aniambie ni namna gani na Wilaya yetu ya Mkinga anakwenda kuijumuisha kwenye Gridi hii ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nizungumzie suala la ukamilishaji wa miradi iliyoanza. Katika Wilaya yetu ya Mkinga tuna miradi mingi ambayo haijakamilika, mradi mkubwa ni Mradi wa Tanga – Mkinga, Tanga – Horohoro. Mradi huu kwa kweli mpaka sasa tunamshukuru Mheshimiwa Samia ametuwekea shilingi 35,000,000, huo umeshaanza kutoa maji katika Kata ya Mtimbwani, tumeambiwa mwezi Oktoba utakamilika, tarehe hizi, Mheshimiwa Waziri nimwombe zisibadilike. Wananchi wa Mkinga wana hamu sana na maji haya, wameyakosa muda mrefu, wanaendelea kumshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa maji haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine ambayo haijakamilika ni Mradi wa Mhinduro, Mradi wa Gombero, Mradi wa Mapatano, Mradi wa Daluni na Mradi wa Bwiti. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri tukimpitishia bajeti hii, katika mwaka unaoanza Julai atukamilishie miradi hii ili na sisi watu wa Mkinga tuweze kufurahia mema ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, nizungumzie suala la upotevu wa maji. Wamesema wengi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. TWAHA S. MWAKIOJA:** Nimalizie kwa kusema, ninaona muda umenitupa mkono; nilitaka kuzungumzia suala hilo. Nizungumzie *pre paid meter* nalo ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa, niiombe Wizara ya Fedha na Serikali kwa ujumla ihakikishe Wizara hii inapatiwa fedha kwa wakati ili iweze kuwasaidia wananchi. Ni Wizara pekee ambayo huduma yake haikwepeki hata kwa dakika moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaomba niunge mkono hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Twaha, ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Deo Mwanyika; Mheshimiwa

Emanuel Nuwas na Mheshimiwa George Venance Lugomela wajiandae.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia katika hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme, kwamba sisi Wananjombe Mjini tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, tumekuwa na miradi mingi kwa mara ya kwanza. Njombe haikuwa na miradi mikubwa ya maji, lakini katika kipindi cha miaka mitano tumepata takriban shilingi 58,000,000,000 kwa miradi mikubwa mitatu ya maji kwa ajili ya Mji wa Njombe unaokua kwa haraka sana. Kwa hiyo tunaishukuru sana Wizara kwa utekelezaji mzuri, tunawashukuru sana *NJUWASA* ambao wamefanya kazi nzuri wakiongozwa na viongozi wa *NJUWASA* pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo yote Njombe Mjini bado haijaeleweka kwa Wizara ya Maji. Njombe Mjini ni halmashauri ambayo ina mji na vijiji. Tuna vijiji 44; lakini katika vijiji hivyo 44 tuna tatizo kubwa sana la maji. Nimelisema hapa, nimelirudia na kulirudia kila mwaka. Niombe Mheshimiwa Waziri atuangalie sana Njombe Mjini, kwa maana ya Njombe Vijijini. Katika miaka mitatu iliyopita yote hatujawa na mradi wowote uliotekelezwa katika maeneo ya vijiji. Mwaka jana nilisema hapa kwamba tumeondolewa mpango mzima wa *P4R* kwa sababu tunaonekana tupo mjini lakini tuna vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru mwaka jana tukapewa Mradi wa Kifanya, tukaingia kwenye makaratasi. Mradi huo ukafanyiwa usanifu, tenda zikatayarishwa, mikataba ikawa tayari kusainiwa, lakini ikasimamishwa; hata huo nao haukuendelea. Nimwombe sana Mheshimiwa Aweso sana, ninaomba atumie kila uwezo alionao angalau tuwe na mradi Njombe Vijijini katika kipindi hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kwamba tuna Mradi mwingine mkubwa wa Igongwi. Nimeongea kwa muda mrefu

sana na Mheshimiwa Aweso anaufahamu huo mradi. Mradi wa Igongwi ni mradi mdogo wa bilioni 4.7; cha kusikitisha ni kwamba mradi huu una miaka 10 haujakamilika. Mradi una lot nne, *lot* ya kwanza imekamilika, *lot* ya pili imekamilika, lakini tuna *lot* ya tatu na ya nne, ndiyo juzi, juzi. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri baada ya kumlilia akam-*authorise* Katibu Mkuu atupatie angalau fedha kidogo, tunashukuru kwa hilo limesukuma. Hata hivyo tunaomba huu Mradi wa Igongwi upewe kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kuwa upo kwenye mpango; lakini kuwekwa kwenye mpango ni jambo moja na kupata fedha za utekelezaji ni jambo lingine. Niombe sana upewe kipaumbele. Haiwezekani mradi wa *4.7 billion* ukakaa miaka 10. Niombe sana wananchi wa vijiji vinavyohusiana na mradi huu wapate hiyo haki yao ambayo kweli wanastahili kwa maana ni wa muda mrefu. Tuna Vijiji vya Kitulila, Madobole, Luponde, Buwemba, Njomlole, Magoda na Ikisa. Vijiji vyote hivi havina maji; na Kijiji cha Uwemba ndicho ninachotoka mimi, hakina maji. Nimwombe sana Mheshimiwa Aweso atusaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kifanya ambao umeondolewa kwa sababu za kitaalam pengine, mimi sizijui; lakini niseme mradi huu ni mradi ambao Mheshimiwa Rais marehemu Magufuli alipita eneo la Kifanya akiwa na Waziri wa Maji Mheshimiwa Mnyaa Mbarawa, wakawaahidi wananchi, wakawaambia kwamba utatekelezwa ndani ya miaka miwili, lakini hadi leo mradi huu haujatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika usanifu wananchi wamehusishwa, kwa hiyo wanaufahamu vizuri, wanauongelea lakini hawajaona huo mradi. Niombe sana, mradi wa Kifanya ninajua hajauweka kwenye bajeti kwa sababu anasema ni mradi mpya; lakini *in fairness* mradi huu ulitakiwa uwepo, kwa sababu hatujapata mradi vijijini katika miaka mitatu; hata huu uliowekwa umetolewa. Kwa hiyo nimwombe sana atuangalie kwa jicho la pekee sana watu wa Halmashauri ya Njombe Mjini na maeneo ya vijijini ambayo yanahitaji jicho la kipekee ili yaweze kuangaliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru tuna mradi wa majitaka; mradi huu unakwenda vizuri lakini unahitaji kukamilishwa. Njombe imefikia mahali ambapo inatakiwa iwe manispaa, haiwezi kuwa kama hakuna mradi wa majitaka. Tuombe sana mradi huu wa maji taka nao ukamilishwe kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa tuna mradi mdogo sana ambao niliomba nao uangaliwe. Tuna jengo la ofisi pale mjini la *NJUWASA,* tuombe sana nao uangaliwe kwa sababu pale Njombe tunatumia ofisi za mkoloni hadi leo. Tuombe kwamba angalau tuangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Deo, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea na wachangiaji wanaofuata ninaomba tuwatambue wageni ambao wapo katika ukumbi wetu huu siku ya leo muda huu. Hawa ni wageni kwanza waliokaa kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika; Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, Mbunge na Waziri wetu wa Maji. Hawa ni Shekhe Habib Bati, Naibu Amir Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Tanzania. Pia tuna Shekhe Karim bin Shamsi, Shekhe wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Mkoa wa Dodoma. Karibuni sana wageni wetu wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge: Wageni 13 wa Mheshimiwa Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Hawa ni wafanyakazi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *NSSF* kutoka mikoa mbalimbali nchini. Karibuni sana wageni wetu kutoka *NSSF*. *(Makofi)*

Tuna wageni wawili wa Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, ambao ni rafiki zake kutoka Chama cha Waigizaji Tanzania. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wawili wa Mheshimiwa Khadija Shaaban Taya, wafanyakazi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii *NSSF* kutoka Nyamagana Jijini Mwanza. Karibuni sana wageni wetu wote katika Bunge letu. *(Makofi)*

Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas; Mheshimiwa George Venance Lugomela, na Mheshimiwa Esther Midimu wajiandae.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti ya Wizara ya Maji. Awali ya yote, nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo anaendelea kuwezesha Wizara yetu ya Maji kupata bajeti nzuri ili kuweza kutekeleza miradi ya maji. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu wake pamoja na timu nzima ya Wizara kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika kuhakikisha kwamba tunamtua mama ndoo na tunawatua ndoo Watanzania wa maeneo ya vijijini na mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kumpongeza pia Meneja wangu wa *RUWASA* mkoa, lakini pia na wilaya kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini wanapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza Wizara kwa maono ambayo hasa yametokana na Mheshimiwa Rais ya kuanzisha Gridi ya Taifa ya Maji. Katika hili tuna uhakika kwamba mahitaji yetu ya maji, ambayo ni takribani *cubic meter* bilioni 42 ambayo ni sawa na 37% ya maji safi na salama yaliyoko chini ya ardhi, lakini pia na juu ya uso wa ardhi; ambayo kwa kweli tuna uwezo isipokuwa tunachohitaji ni miundombinu na hasa usambazaji na kikubwa ikiwa ni bajeti lakini pia na mpango. Kwa hiyo, ninaomba niitie moyo Wizara kushikilia jambo hili na kulitekeleza kikamilifu. Hata kama itachukua miaka ya kutosha, lakini tuweze kuiona ikitekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishukuru Wizara kwa miradi ya maji ambayo imeweza kuletwa katika Jimbo la Mbulu

Vijijini, lakini miradi mingi bado haijakamilika. Niiombe Wizara ikamilishe miradi hii. Hasa nitangulize kwa kutaja Mradi wa Dambia ambao utahudumia vijiji 21. Mheshimiwa Waziri ametutengea 500,000,000 lakini hadi sasa mkandarasi anadai takribani bilioni 1.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nilitamani nishike shilingi yake, ila kwa kuwa ameongeza bajeti ninaomba nisiishike shilingi yake wala mshahara wake. Ninaomba akamilishe lile deni, tupate na bilioni hizo ili mradi ule uweze kukamilika kwa ajili ya kuhudumia Kata za Bashay, Endamilay, Eshkesh, Dongobesh na Idachini, zikiwa ni vijiji 21. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nipende kushukuru pia Vijiji vya Laghangesh, Mangisa, Getesh, Esqaroda, Gitultaqao; lakini pia Multuru, Diomat na Endagao vitapata maji. Kwa kweli nipende kuleta shukurani za dhati kutoka wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Wizara ipeleke fedha hizi ili miradi hii iweze kukamilika na wananchi waweze kupata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilete maombi machache kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Mbulu Vijijini. Tuna Kata ya Masyeda ambayo ina Kijiji cha Endanyawish. Ni kijiji kikubwa sana ambacho kina wakulima na wafugaji. Tumechimba takribani visima vitano lakini havina maji. Ninaomba Mheshimiwa Waziri aitazame kata hii na kijiji hiki ili kiweze kupata maji. Tuna maji katika Bonde la Endagichan ambayo ni kata, tunaweza tukayachimba na kupeleka kule. Ninaomba nilete ombi hilo rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mji wa Dongobesh ambayo ni makao makuu ya halmashauri tuna maji ambayo ni machafu kutokana na kutokuwa na chujio na pia bado hayatoshelezi mahitaji ya mji. Niiombe Wizara itusaidie bajeti ili tuweze kupata chujio ili wananchi takribani 20,000 wanaokaa katika Mji wa Dongobesh wapate maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru pia Wizara kwa kukubali kuongeza upatikanaji wa maji kwenye mji huu kwa kuleta maji kutoka Mradi wa Dambia na hivyo ninaamini ndani ya miezi mitatu ijayo wananchi wa Dongobesh wataweza kushukuru kupata maji na kubaki salama katika mji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Kata ya Maghan ambayo ina chanzo cha maji kilichochimbwa mwaka 1975, wakati huo ikiwa na wakazi kama 500, leo tuna wakazi 15,000 na bado inategemea chanzo hiko kimoja. Niombe tuweze kupata chanzo kingine. Kwa bahati nzuri kata hii ina bonde zuri sana ambalo lina maji mengi. Tukipata visima viwili tayari wananchi hawa ambao ni takribani 15,000 watakuwa wamepata maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi ya mabwawa. Jimbo langu hili lina takribani kata tano, ambazo Mheshimiwa Waziri akitutengea bajeti maeneo yapo ya kuchimba mabwawa na kuyatengeneza ili wananchi waweze kupata maji. Ninaomba Kata za Masqaroda, Maghang, Gidhim, Eshkesh, Haydom, Masonyagwe, Labay, pamoja na Basoderer wachimbiwe mabwawa ili wapate maji safi na salama kwa ajili ya nyumbani na mifugo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru sana na ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja kwa ajili ya wananchi wetu kupata maji safi na salama. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa George Venance Logomela, atafuata Mheshimiwa Esther Midimu, Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa na Mheshimiwa Anna Lupembe wajiandae.

**MHE. DKT. GEORGE V. LUGOMELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia katika bajeti hii ya Wizara ya Maji. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uhai na nguvu na hivyo kuweza kutoa mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Rais wa nchi yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatua akina mama ndoo kichwani. Kusema kweli kazi hii ameianza tangu akiwa Makamu wa Rais. Tunampongeza sana kwa maono. Tumeona fedha nyingi ambazo ameweza kutoka katika kipindi chake katika Wizara hii ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Waziri wa Maji ndugu yangu Mheshimiwa Jumaa Aweso kwa kazi kubwa anayoifanya katika Wizara hii katika kutimiza maono ya Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Aweso kadiri anavyozidi kukaa kwenye hii Wizara ndivyo anavyokuja na matokeo makubwa zaidi, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri, pia tunampongeza Naibu wake *Engineer* Kundo kwa kazi kubwa anayoifanya ya kumsaidia kusimamia miradi na kufuatilia utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Katibu Mkuu wa Wizara hii, *Engineer* Mwajuma Waziri pamoja na watendaji wote kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kuhakikisha kwamba miradi ya maji inatekelezwa vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai na kila siku kukicha mahitaji ya maji yanaongezeka; kwa sababu watu tunazidi kuongezeka na kila mtu anahitaji maji na maji yanabaki kiasi kilekile. Wizara ya Maji imekuja na suluhisho kubwa na suluhisho hilo ni *SGR* ya maji, kwa maana ya *National Water Grid*. Niipongeze sana Wizara kwa kuanzisha mradi huu mkubwa wa *National Water Grid*. Kusema kweli utekelezaji umeanza. Mheshimiwa Waziri ametuambia kwenye hotuba yake kwamba tumeanza na ule Mradi wa *KASHIWASA*, kwa maana ya maji yanayokwenda Kahama – Shinyanga na sasa hivi yanaenda Tabora – Igunga – Nzega mpaka na wilaya zote za Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SGR* au *National Water Grid* imeanza pia kutekelezwa katika Mkoa wa Simiyu kupitia ule mradi wa *climate resilience*. Mradi ule unachukua maji pale Nyashimo na kupeleka Wilaya za Busega, Bariadi na Itilima kwa awamu ya

kwanza. Tunaishukuru sana Serikali kwa hatua iliyofikia katika utekelezaji wa mradi huu. Mradi huu uko zaidi ya 50% na utakuwa ni mkombozi mkubwa kwa Wanasimiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa Serikali, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri na watendaji wote, awamu ya pili ya mradi huu itaenda Maswa na Meatu na hizi ndizo wilaya kame kabisa katika Mkoa wa Simiyu. Tuombe kwamba utekelezaji wa awamu ya kwanza uende kwa wakati ili tukamilishe awamu ya kwanza na tuanze awamu ya pili ambayo wananchi wa Maswa pamoja na Meatu wanasubiri kwa hamu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mradi huu wa *climate resilience* tuna miradi midogo midogo ambayo inahitaji kukamilishwa wakati tunasubiri maji ya kutoka Ziwa Viktoria. Tuna mradi wa kuongeza mtandao wa maji Maswa Mjini; hapa tunahitaji tu milioni 257 ili kazi hii iweze kukamilika. Vilevile tuna mradi wa ununuzi wa dira za maji, 657,000,000 na mradi wa maji Sulu nao unahitaji 650,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, moyo usiyokuwa na shukrani ukausha yaliyo mema yote. Niishukuru Wizara kwa kazi kubwa waliyoifanya. Wameweza kutujengea mabwawa mawili katika mwaka huu wa fedha; Bwawa la Mwamashindike na Bwawa la Bugalama, jumla ya takribani 2,000,000,000. Wameweza kukamilisha ujenzi wa tenki la Induki la lita 2,000,000 kwa kutumia 2,000,000,000. Tenki hili limeboresha huduma ya maji katika Mji wa Maswa. Kuna mabwawa mengine mengi ambayo yamejengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kazi ya ujenzi wa mabwawa pia iendelee katika Kata za Mwamanenge, Sangamwalugesha, Mwabaratulu, pamoja na Binza, Bwawa la Nyamasaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa George Venance Lugomela. Nilimtaja Mheshimiwa Esther Midimu, atafuata Mheshimiwa Engineer Ezra Chiwelesa; Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Edifonsi Kanoni wajiandae.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri iliyosheheni matumaini ya akina mama, ninamshukuru sana. Pia nimpongeze Meneja wetu wa *RUWASA,* Mkoa wa Simiyu pamoja na *cabinet* yake, wanafanya kazi nzuri sana. Niwapongeze pia Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri ni majembe, wanafanya kazi nzuri sana, Mwenyezi Mungu awabariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais mama yetu kipenzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa nia nzuri ya kuwatua akina mama ndoo kichwani. Tangu Mheshimiwa Rais aingie madarakani na hata akiwa Makamu wa Rais alikuwa na nia nzuri ya kumtua mama ndoo kichwani. Hongera sana kwa Mheshimiwa Rais na ni lazima tumpongeze, tusipompongeza sisi Wabunge, hakika mawe yatapiga kelele. Mwenyezi Mungu amlinde Mheshimiwa Rais. Wanaomwombea mabaya washindwe na walegee katika Jina la Yesu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutuletea fedha nyingi za ujenzi wa miradi ya maji Mkoa wa Simiyu. Kutokana na kutoa fedha hizi hali ya upatikanaji wa maji vijijini imeongezeka kutoka 60.85% hadi 71% mwaka 2022. Upatikanaji wa maji Mjini Bariadi, Busega, Maswa na Mwanuzi umeongezeka kutoka 55.7% kufikia 67% mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kutupatia Mkoa wa Simiyu shilingi 440,000,000,000 kwa ajili ya Mradi wa Ziwa Victoria. Ujenzi wa Mradi wa Ziwa Victoria na wilaya zake unakuja Simiyu, Wilaya ya Busega, Itilima, Bariadi, Maswa na Meatu. Ujenzi huo umekwishaanza na umefikia 55%. Mheshimiwa Rais, ahsante sana. Awamu ya kwanza unaenda

katika wilaya tatu, ambazo ni Wilaya za Busega, Bariadi na Itilima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, Wilaya ya Maswa na Meatu ina ukame sana. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais ametupatia magari ya kuchimba visima, lakini katika wilaya hizo kuna baadhi ya maeneo hata visima vikichimbwa, maji hayapatikani na hata kama yakipatikana, yanakuwa na magadi hayafai katika matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri na Serikali itafute fedha awamu ya pili mradi uweze kuanza kujengwa. Ninaendelea kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kutupatia fedha. Jumla ya miradi 97 yenye gharama ya shilingi bilioni 63.7 imetekelezwa kuanzia mwaka 2021 hadi 2025 chini ya *RUWASA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ujenzi wa Mradi wa Maji Kabita, Wilaya ya Busega, umegharimu shilingi bilioni 3.1; Mradi wa Maji Mkula umegharimu shilingi bilioni 2.7; Maswa, ujenzi wa Mradi wa Maji Ipililo, shilingi bilioni 1.3; Itilima, ujenzi wa Mradi wa Maji Vijiji vya Madilana na Kinang'Weli, shilingi bilioni 2.3; na Meatu, ujenzi wa Mradi wa Maji Inonelwa, shilingi bilioni 4.8; Bariadi - Ngulyati, shilingi bilioni 1.1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka unaoendelea *RUWASA*, Simiyu itatekeleza miradi 27 yenye gharama ya shilingi bilioni 21.04. Mfano Bariadi, Mradi wa Ihusi shilingi bilioni 1.6; Meatu, Mradi wa Mbushi shilingi milioni 573; na Itilima, Mradi wa Habia shilingi milioni 931. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais. Mimi ni nani nisimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miradi yote hii aliyotuletea? Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mradi wa Maji Lagangabilili lakini pia, Wilaya ya Itilima. Ninaiomba Serikali visima vimekamilika, imebaki usambazaji. Ninaiomba Serikali iweze kusambaza maji, Lagangabilili. Pia kuna Mradi wa Nanga ambao haujakamilika,

niiombe Serikali ituletee fedha tuweze kukamilisha hiyo miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Miradi ya Bariadi inayoendelea kujengwa. Mradi wa Ihusi unaendelea kujengwa, Nkindwabiye unaendelea kujengwa, Mwasubuya, Mwauchumu, Mradi wa Sapiwi na Mradi wa Itubukilo. Ninaiomba Serikali iweze kutuletea fedha ili tuweze kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jumaa Aweso ni mmoja tu, ukimtafuta Mheshimiwa Waziri wa Maji, huwezi kumpata popote pale tofauti na Jumaa Aweso. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na Mungu awabariki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa; Mheshimiwa Anna Lupembe na Mheshimiwa Edifonsi Kanoni wajiandae.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwa mchangiaji katika hotuba hii ya Wizara ya Maji. Kipekee, kwa mara nyingine pia nishukuru, kwa sababu ya Mradi mkubwa wa Ziwa Victoria unaoletwa Biharamulo wenye thamani ya dola milioni 55.1, ambapo kwa *exchange rate* ya leo ya 2,650 unaongea shilingi 146,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mradi mkubwa wa kihistoria unaokuja kutua akina mama ndoo vichwani. Si akina mama wa Biharamulo tu, kwa sababu tunaongea habari ya gridi ya maji ya Taifa, ni kwamba tuna hakika, kwa sababu Ziwa Victoria ni chanzo cha uhakika na gridi ni vyanzo. Tuna uhakika mradi huu baada ya kufika Biharamulo, utahudumia watu wa Ngara, wanaweza kwenda Kakonko na maeneo mengine yote ya jirani pale ili watu waweze kupata maji safi na salama, lakini maji yanayotoka kwenye chanzo cha uhakika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhati ya moyo wangu, nikushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Jumaa Aweso. Nimshukuru

Naibu wako Mheshimiwa *Engineer* Kundo, lakini pia na Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Maji *Engineer* Mwajuma Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya. Wanafanya kazi kama timu, ninakumbuka mradi huu, hata ulipokuwa unaenda kufanya *presentation* huko nje ukiwa unatafuta fedha, ulikuwa unanitumia *clip* unanionesha. Mungu ambariki sana Waziri kwa niaba ya watu wa Biharamulo aendelee kuwa na afya njema, lakini mambo mazuri hayo yaje na jimboni kwake pia, asituletee sisi akasahau kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapa, ninataka niongelee, kwa sababu Wabunge wengi wamekuwa wanaongea visima vimechimbwa, maji hamna, hiki kimechimbwa maji hamna. Ni kweli huwezi kupata mradi wa maji kama maji hamna, kwa sababu kiasili maji hayako kila sehemu. Ndiyo maana, tumeona Serikali imechukua hatua hii ya kutumia vyanzo vichache, lakini vikubwa vilivyopo kwenye hii nchi ili maji yaweze kwenda kila sehemu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina hakika baada ya miaka mitatu, minne, mitano, hatutakuwa tunakuja hapa tena kulia na masuala ya kisima kimechimbwa umeme hamna, kwa sababu kama maji yanatoka kwenye chanzo kimoja, tuna hakika maji yataweza kufika kila sehemu vijiji vitapata maji, lakini na maeneo mengine yatapata maji. Hii ndiyo ajenda kubwa tunayoongelea leo ya gridi ya maji ya Taifa. Kwa hiyo, tuendelee kuwa wavumilivu, jambo hili lipite, tulipitishe kwa kishindo na bajeti hii ipite hatimaye tuweze kuyaona haya ambayo tunayapigia kelele yakifanyika kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *experience* yangu kipindi cha nyuma, wote tunaelewa, hususan bajeti hii iliyopita, ni kama vile hatukufanya miradi mipya, kwa sababu kulikuwa na maelekezo ya kutekeleza miradi mingi ya zamani. Kwa hiyo, tulione hilo na ni vizuri, kwa sababu, unapokuwa na mradi umeishia katikati wananchi hawawezi kupata maji. Tunapomaliza miradi michache tuliyoianza kipindi cha nyuma, tukatoa fursa ya kuanzisha miradi mingine mipya, hatimaye tunakuwa na kitu cha kusema kwa wananchi, na wananchi wale wachache waliopata maji, wanaona na wanakuwa mashuhuda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipongeze kwa ajili ya *plan* hiyo nzuri, tuna hakika miradi hii ambayo imewekwa kwenye bajeti kwa sasa, itaenda kutekelezwa sawa na ambavyo imewekwa kwenye bajeti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa, Wizara ya Maji kumekuwa na shida. Pesa zao nyingi hazitoki kwa wakati, *especially* pesa za Mfuko wa Maji. Mheshimiwa Aweso huyu, maeneo mengi wakandarasi wanafanya kazi kwa heshima yake tu, amekuwa mtu rahimu, akija ofisini, kila anapofuatwa. Kuna kipindi unamwangalia anataka akusaidie lakini pesa hana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tunaomba, *ring fenced money* ambazo zimepitishwa na Bunge, zisiguswe, zirudi zikafanye kazi huku. Huyu baba anahangaika na Katibu Mkuu, lakini kama hawawapelekei pesa, leo wanalaumiwa wao. *This is not fair*, kwa hiyo, tungeomba wasaidiwe kwa kupelekewa pesa, zilizopitishwa kwenye bajeti ya Bunge, ili tusaidie miradi hii hata tusipoongea na wananchi kule, wananchi wayaone haya matunda mazuri ambayo tunayaongelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mjumbe wa Kamati ya *PIC*. Tulipokuwa kwenye ziara tukitembelea miradi, tulipita *DAWASA* pale. *DAWASA* wana *expansiyon* kubwa ya chanzo cha maji cha Ruvu Chini, lakini wale watu wanahitaji *only* 38.7 *million dollars*. nadhani. Tungeomba tuwape hii pesa wamalizane kule. Unajua ni aibu mimi wa Biharamulo nalilia maji, nipewe pesa 1,000,000,000, *DAWASA* inayobeba nchi nzima nayo inalilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakishampa huyo wakamalizana naye, mwakani watupe sisi wadogo. Kuliko leo unampa 1,000,000,000 haimalizi, unampa 2,000,000,000 haimalizi, mimi kwangu unanipa 500,000,000 haimalizi. Amalizane naye afanye biashara, hizo hela nyingine mwakani watuletee sisi, tukawapelekee wananchi tuwape huduma. Hilo jambo tuliliona, tunaomba wasaidiwe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tuliliona, ni suala la kutoza *VAT* kwenye umeme na *VAT* kwenye maji. Maji tunajua,

*VAT* anatozwa *end user*. *End user* kwenye maji hakuna *VAT*. Hizi mamlaka zinatozwa *VAT*. Saa nyingine zinakaa na madeni *TANESCO* haziwezi kulipa, zinadaiwa *TRA*. Tulione hili, basi tuwasaidie, kama hamna *VAT* kwa *end user, why are we charging them VAT* kwenye masuala ya umeme na huduma nyingine wanazozitoa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka mamlaka zisimame, zifanye biashara, zilete gawio Serikalini, kwa sababu Serikali imeweka mtaji kwenye hizi mamlaka. Sasa hazitaweza kufanya hivyo kama bado tunazibana. Kwa hiyo, ninaomba hilo lionekane, tuwasaidie, waweze kufanya kazi, ili na sisi wa vijijini tunaowawakilisha wananchi walio wengi, wanaohitaji huduma ya maji, kwa sababu bado wanakunywa maji kwenye sehemu nyingine. Tumeambiwa ni zaidi ya 70%, haijafika 90% wala haijafika 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba watusaidie, ili bajeti inayofuata, pesa nyingi zielekezwe vijijini zitusaidie sisi, kuliko kuendelea kupeleka pesa tunagawanya nusunusu, inakuwa haitoshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona *mic* imewashwa muda mrefu, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi. Ninaunga mkono hoja, pesa ipelekwe, Mheshimiwa Aweso na watu wake wakafanye kazi, sisi tuko nyuma yao tunawa-*support*. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, *Engineer* Ezra Chiwelesa. Nilimtaja Mheshimiwa Anna Lupembe; Mheshimiwa Edifonsi Kanoni na Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi wajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Ninaomba nimpongeze sana Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya pamoja na Naibu Waziri, pamoja na Katibu Mkuu na *Management* yote ya Wizara, pamoja na viongozi wote wanaosimamia mamlaka ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *RUWASA* ndiyo inafanya kazi vijijini. Tulikuwa tunaomba *RUWASA* ipewe kipaumbele, kwa sababu ndiyo inashughulika na miradi yote ya vijijini, kuhakikisha wanawake wa vijijini wanapata maji safi na salama. Ninaomba nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa *RUWASA* Mhandisi Kirita, kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kusimamia mamlaka zote za mikoa, ma-*RM* wote, kwa ajili ya kuhakikisha miradi inakwenda vizuri. Ninaomba *RUWASA*, ma-*RM* hawana *OC* ya kwenda kuhakikisha kufuatilia miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba *RUWASA* iongezewe bajeti na isimamiwe vizuri ili miradi ile ya vijijini iweze kwenda kusimamiwa vizuri. Ma-*RM*, ma-*MDs* wanafanya kazi vizuri katika maeneo yetu. Ili tuweze kufanya kazi vizuri, Mfuko wa Maji lazima uongezewe pesa. Mfuko wa Maji ndiyo utafanya kazi vizuri kuhakikisha nchi yetu inakwenda vizuri, maji yanapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mkurugenzi Mkuu, Haji kwa kazi kubwa ambayo anausimamia Mfuko wa Maji kuhakikisha pesa zinapatikana. Serikali nayo ihakikishe inaongeza pesa kwenye Mfuko wa Maji ili maji yaweze kupatikana katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna miradi mbalimbali katika maeneo yetu, ndiyo maana nimesema *RUWASA* na Mfuko wa Maji waongezewe bajeti kwa sababu kuna miradi sasa hivi imesimama. Jimbo la Nsimbo, kuna Mradi wa Ivungwe, kuna Mradi wa Tumaini, kuna Mradi wa Kabuga, yote imesimama kwa sababu wakandarasi hawajapata pesa zao. Ninajua Serikali ina malengo mazuri, lakini tukiweza kuweka nguvu kwa *RUWASA* wakapewa bajeti nzuri na Mfuko wa Maji ukapewa bajeti nzuri, hawa wakandarasi wote hatutaweza kupata nao tabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunakwenda haraka, katika Jimbo langu la Nsimbo, Halmashauri ya Nsimbo, nina Kata pale za Mtapenda, Kapalala, Nsimbo yenyewe pamoja na Urwila, pamoja na vijiji vyake. Tunahitaji mradi mwingine mpya, Mradi wa Ikolongo, kwa sababu watu wameongezeka na vilevile ni Makao

Makuu ya Halmashauri yetu ya Nsimbo, kuna Hospitali ya Wilaya, kuna mambo mengi katika halmashauri ya Nsimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Aweso, ninajua ni msikivu, nimpongeze sana, kwa sababu amefika katika maeneo yale. Alikuja katika Kijiji cha Mtakuja, alikuja katika Kijiji cha Songambele, alikuja katika Kijiji cha Isinde, unajua adha ya wananchi, maji bado hayatoshelezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Waziri, Aweso, yeye ni msikivu. Tunampenda, tunaomba maji, Mradi wa Ikolongo uanze mara moja, ili kuweza kuondoa adha ya Hospitali ya Wilaya ya Nsimbo, Halmashauri ya Nsimbo pamoja na wananchi, hususan Kijiji cha Kapalala, hakina maji kabisa. Ninajua alifanya jitihada kubwa, alipeleka gari mara mbili, ninaomba nimpongeze *RM* wa Mkoa wa Katavi, Iddi Pazi, alipeleka gari mara mbili kuhakikisha kuchimba visima, lakini maji hayakupatikana. Tukianzisha mradi huu wa Ikolongo, ninafikiri vijiji vyote, vya kata zote, watapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa, wametuletea pesa, miradi inaonekana, wananchi wanapata maji safi na salama. Hiyo ni kazi kubwa ambayo amefanya Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ajili ya kuwatua ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wote wa Wizara, *Engineer* Mwajuma amefanya kazi kubwa na nzuri. Amejitahidi kuhakikisha wanawake anawachimbia visima. Ninaomba nimpongeze Katibu Mkuu pamoja na *management* yake yote kwa kazi kubwa na ufuatiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niunge mkono hoja kwa kazi kubwa na nzuri ya Wizara ya Maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anna Lupembe. Nilimtaja Mheshimiwa Edifonsi Kanoni, Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi ajiandae.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hotuba ya Wizara ya Maji. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali siku ya leo, lakini pia nimwombee Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan awe na afya njema, kwa sababu ninajua maombi ninayomwombea Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mwenyezi Mungu halali, huwa maombi yangu yanafika kwa Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri mwenyewe, imani ni kubwa sana kwa Watanzania na hasa akina mama walipo vijijini. Anafanya kazi kubwa sana, nimpongeze sana, lakini pia ni kijana. Kwa hiyo, tuna imani kwamba atakimbia zaidi. Mheshimiwa Waziri aongeze *speed*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani ni kubwa na Wabunge wote wanaoweza kuchangia hapa wana imani kubwa na Waziri kwa jinsi ambavyo anasimamia miradi ya maji. Ndoa nyingi zimepungua, zilikuwa zinavunjika kwa sababu ya akina mama kufuata maji umbali mrefu, lakini sasa amejaribu kupunguza changamoto na akina mama wengi, asilimia kadhaa wanaendelea kupata maji katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mradi wa Maji ambao tumeupokea katika Wilaya ya Kalambo Mji wa Matai ambao huu mradi ni ujenzi wa chujio la maji wa shilingi 1,623,000,000. Mheshimiwa Waziri, tunamshukuru sana kwa kupokea huu mradi, lakini pia katika huu mradi, nimwombe Mheshimiwa Waziri, atoe kibali kuweza kuongeza mtandao wa maji katika Mji wa Matai ambao unakuwa kwa kasi, katika vitongoji vya Kateka, Kasisiwe, na Keleni, ambavyo vipo katika Mji Mdogo huu wa Matai. Pia, katika Mji wetu wa Matai, tuko *border* kati ya Zambia na Congo. Tunapokea wageni wengi, tunahitaji kuwa na miundombinu ya maji ili kuboresha maisha ya Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi wa maji inayoendelea katika Wilaya ya Kalambo, hususan katika Kata ya Legezamwendo ambayo ina vijiji sita, katika Kijiji cha Mombo, Mkombo, Utengule, Mlenje pamoja na Kalembe. Mheshimiwa

Waziri, huu mradi, mkandarasi anadai shilingi 803,000,000. Nimwombe Waziri katika bajeti tutakayopitisha, basi aangalie jinsi ya kuweza kukamilisha mradi huu, tuweze kunufaisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mradi wa Maji Kisumba ambao ni Kijiji cha Kisumba, Kafukoka, Kisenga pamoja na Kasote. Huu mradi, mkandarasi anadai shilingi 537,000,000. Nimwombe kwa heshima, imani yangu ni kubwa, huu mradi uweze kukamilika ili unufaishe wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mradi wa Maji katika Kata ya Mnamba ambao mkandarasi anadai shilingi milioni 165. Nimwombe nao asukume ili katika bajeti tutakayoitoa aweze kupita, wananchi waweze kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Mradi wa Maji wa Mbuluma katika Kata ya Mbuluma ambao upo katika Kijiji cha Mbuluma, ambapo Kalemasha na Lolesha ni wanufaika wa mradi huu ambao mkandarasi anadai shilingi milioni 165. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu kwa Mheshimiwa Waziri, ni kubwa na sina mashaka na si mimi tu, hapo na Waheshimiwa Wabunge tutapitisha bajeti, kuhakikisha kwamba haya ambayo ametusomea katika bajeti yako yanapita ili utekelezaji wa miradi uende kukamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo ambayo hayana maji kabisa, kuna Kijiji cha Kasusu, Sengakalonje, Mpanga, Chalatila, Kanyezi pamoja na Ilambila. Haya maeneo Mheshimiwa Waziri, hayana maji kabisa katika hivi vijiji katika Wilaya ya Kalambo. Nimwombe katika bajeti itakayopita waangalie kwa jicho lingine, akina mama kwa maeneo hayo wanapata shida sana kufuata maji kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshawasilisha katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Kata ya Mpombwe - Kijiji cha Kapozwa; na Kalambo, katika Kata ya Samazi - Kijiji cha Samazi na Kipanga; hivi vijiji havina maji. Tunaomba kwa bajeti itakayopita Mheshimiwa Waziri atujali na sisi tupate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa mradi ambao sasa umewasilishwa katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri, kwamba sasa kunaenda kujengwa Mradi wa Gridi ya Maji ya Taifa. Nimwombe, huu mradi ni mkubwa, lakini utachochea uchumi sana, siyo kwa matumizi tu ya maji ya kuoga na kufua, lakini utachochea uchumi kwa maana wananchi watafanya kilimo kwa wakati wote wa kuanzia mwezi Januari mpaka Desemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mradi katika pointi ambazo alizitaja Mheshimiwa Waziri kutoka Kigoma, Katavi, Kalema, ukija Rukwa unaitaja Kalambo lakini pointi yake iko Samazi. Nina imani kubwa na Mheshimiwa Waziri, niko tayari kupitisha bajeti yake hii kuhakikisha kwamba yale ambayo ametusomea katika bajeti yake yanatimia ili tukamilishe miradi yetu wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kanoni. Tunaendelea na Mheshimiwa *Engineer* Kija Ntemi, Mheshimiwa Masanja Kadogosa ajiandae.

**MHE. KIJA L. NTEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kupata nafasi hii kuchangia katika Wizara ya Maji. Mheshimiwa Waziri Aweso, awali ya yote niipongeze sana ofisi kwa ujumla. Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, wanafanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu mmoja anasema, anaweza ukawa simba ukawa peke yako, lakini pia anaweza akawa simba akawa na wenzake wakafanya kazi vizuri. Mheshimiwa Aweso ni simba na ana simba wenzake wanaofanya kazi vizuri, niwapongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, sitasoma sana mafungu na mimi ni msomaji wa mafungu, ataenda asome mwenyewe pamoja na Naibu wake. Watasoma Isaya 44:2, wakiusoma utawasaidia kwa ajili ya manufaa yao. Mheshimiwa

Waziri, sisi kule kwetu Katoro, nadhani *O-Kundo agomanile, okobhise Katoro.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ametuletea maji yenye gharama kubwa sana, kupitia Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitupatia maji nadhani hata yeye kwenye kampeni alikuja na wale watu wa Katoro tuliwaeleza kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameleta maji ya zaidi ya shilingi bilioni 6.3 pale Mji wa Katoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiwekeza lazima pia ujipange kuvuna ulichokiwekeza, umewekeza mradi mkubwa sana wa maji tunaomba, hoja yetu ni ndogo sana tunatamani watuletee mabomba ili tuweze kusambaza maji katika Mji wa Katoro maana maji yapo. Hadi sasa maji yanapampia kutoka Chankorongo nadhani ukipata muda utatembelea Katoro twende Chankorongo maji yapo yako mengi sana yanayosukumwa kwenye matenki ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, changamoto ukishayapampu unayapeleka wapi? Yanabaki kwenye matenki kwa sababu mabomba ya kusambaza maji ili wananchi wapate maji katika Mji wa Katoro na kata zake bado ni mdogo sana. Kwa hiyo, nimwombe, watu wanasema kushikilia shilingi, mimi sitaki nishikilie shilingi yake ila ninaomba anisaidie kupata mabomba ya kutosha ili watu wa Katoro waweze kusambaziwa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ukishayasambaza haya maji wale idara ya maji wana uwezo wa kujiendesha kwa sababu watalipa madawa, watalipa watumishi watafanya, kwa sababu maji yamepata nafasi na maji yamesambazwa na wananchi wetu wamepata maji ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, Waziri anapofanya hivyo anatuletea mabomba tukumbuke kwamba ili watu wetu waweze kupata huduma sasa maana siyo watu wote wanalingana kiuchumi, basi watupunguzie gharama za kuwasambazia watu hawa maji kwa sababu wanapokwenda

kuwasambazia ikiwa gharama kubwa, watu watakaosambaziwa maji watakuwa ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimwombe sana Waziri baada ya bajeti yake ajitahidi kutuhudumia, awasaidie wananchi wetu waweze kupata huduma ya kutosha ambayo itawasababisha wao kuamini kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipopita katika Mji wa Katoro alitoa ahadi pamoja na kwamba kuna maji yanayokuja yenye mradi mkubwa kutoka Geita, alisema yatakuwepo maji ya kutosha katika Mkoa wa Geita kiujumla.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kabla ya huo Mkoa wa Geita kwa ujumla kwa kuwa Mheshimiwa Rais alishawekeza katika Jimbo la Katoro, basi ahakikishe anakwenda kusambaza hayo maji ili wananchi hawa waweze kupata huduma nzuri na Waziri tunamwamini na ndiyo maana tunatafuta nafasi sana ya kuzungumza, tumpongeze kwa kazi nzuri uliyoifanya. Miaka tisa yuko ndani ya hii Wizara na ameonekana kuwa simba jasiri anayeweza kuleta maendeleo makubwa kwa wananchi wetu na katika Nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, baada ya haya machache, kubwa sana kwangu ninaweza nikazungumza mambo mengi sana, lakini hoja yetu sisi ni moja tu akatusambazie maji ya kutosha maana maji yalishayafika katika Mji wa Katoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, ninaunga mkono hoja, ninamwombea heri Mungu ambariki, achape kazi, asonge mbele pamoja na Mheshimiwa Naibu wake Mheshimiwa Injinia Kundo, wachape kazi, Mama amewaamini kwa moyo wa hali ya juu sana, waende wakapige kazi walete maendeleo kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Masanja Kadogosa, Mheshimiwa Dougras Massaburi ajiandae.

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuweza kuweka sauti yangu kwenye Wizara hii muhimu sana katika Taifa letu. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu amekuwa *champion* mkubwa sana tangu akiwa Mheshimiwa Makamu na sasa hivi Mheshimiwa Rais wa nchi yetu kwa suala la kutua ndoo mama zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nimpongeze sana mdogo wangu Mheshimiwa Injinia Aweso anafanya kazi nzuri sana katika Taifa hili na Mwenyezi Mungu amembariki kwamba Wizara hii amekuwa nayo kwa muda mrefu kidogo sasa hivi, lakini ame-*grow* nayo na ninaamini kwamba Watanzania tunayoyaona humu na wao wanayaona hayo kwamba, kuna kuna maendeleo makubwa sana. Niungane kukubaliana na Waziri kwamba *evolution* kubwa ya kuleta *RUWASA* imeleta mabadiliko makubwa sana. *(Makofi)*

*Hapa Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti*

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Spika, vilevile nimpongeze ndugu yangu mdogo wangu Mheshimiwa Injinia Kundo kwa kazi kubwa sana anayoifanya ni jirani yangu huyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nimpongeze *Engineer DG* wetu, Bwana Wolta Kirita, anafanya kazi nzuri sana katika *RUWASA*, lakini Injinia Mwajuma ambayo ni *PS* wetu amekuwa ni mama kinara sana na tunampongeza kwa kupata hiyo zawadi. Pia kuna Injinia Mwampungo, kwa maana ya Wilayani Bariadi na Injinia wa *RUWASA* wa Mkoa wetu, Ndugu Esatula. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeanza kwa kupongeza za kwa sababu wananchi wa Bariadi Vijijini wangenishangaa nisingezungumza haya. Sisi Bariadi Vijijini mpaka wakati tunafanya kampeni tulikuwa na upatikanaji wa maji ilikuwa kama 79.8% lakini kwa sasa hivi baada ya visima kadhaa kufunguliwa upatikanaji wa maji kwenye 84%, kwa hiyo, tuko *above* kidogo ya *average* ya 83%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunashukuru sana katika hili. Kwanza Waziri kwa maana ya Wizara kwa kazi kubwa wanayotufanyia. Pamoja na kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri na watendaji wote, ni kweli ni lazima niseme kwamba kuna miradi ambayo wanaifanya katika Jimbo la Bariadi Vijijini, kuna miradi kama saba hivi na bahati nzuri dada yangu ameitaja. Mojawapo ni Husi kuna Nkindwabie, Mwauchumu, Sapiwi, Ikunguliyambeshi kwa maana ya Kilalo ninajua miradi hii ina thamani ya bilioni 4.7 na pesa ambazo zimeshatolewa mpaka sasa hivi ni bilioni 1.6. Ninajua katika bajeti hii wametenga kama bilioni 1.1, lakini tunahitaji ili tuweze kumaliza hii miradi bilioni 3.03.

Mheshimiwa Spika, sasa kwa namna yoyote ndugu yangu ningependa kwamba nishike shilingi, lakini sasa ukaka mzito sitaweza kushika shilingi. Kwa hiyo, haya tutayazungumza kinyumbani kwani tunapenda sana hizi fedha zije ili tuweze kumalizia miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuna mradi mkubwa sana wenzangu, nisingetaka kurudia unaotokea Ziwa Victoria ambao ninajua itakuwa ndiyo tiba kubwa sana. Bahati nzuri ametupendelea sana kuwa na *component* mbalimbali mle ndani ikiwepo kwa maana ya ujenzi wa mabwawa ambayo yatatusaidia sana kwenye umwagiliaji, lakini kwenye mifugo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ningetaka nizungumzie la mwisho kwa sababu ni dakika tano tu la Kitaifa. Duniani imefunikwa na maji kwa 71%, lakini katika 71%, 97.5% ni maji ya chumvi na ni 2.5% ndiyo maji ya kunywa au ambayo yanaweza kutumika katika majumba *eco system,* lakini vile kwa ajili ya *agriculture*. Sasa hiyo ina maana gani, maana yake ni kwamba kuna kuna *scarcity,* uhaba wa maji upo.

Mheshimiwa Spika, hiyo inasababisha kusema ni lazima tuwekeze kwenye maji, kama uwekezaji mwingine. Wamezungumzia mambo ya *SGR* ni lazima tuwekeze kama tutekeza kwenye Bwawa la Nyerere na bila uwekezaji kwa kweli hatuwezi kufika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwenzangu hapa amezungumzia kuhusu hali ya maji sasa hivi kwenye miji yetu mikubwa. Ukiangalia uchakavu wa miundombinu au na mambo mengine ambayo yanasababisha uhaba wa maji haya ni mambo ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, sasa kuna jambo moja ambalo ninapenda kukumbusha na alizungumza yeye mwenyewe; ushirikishaji wa sekta binafsi ni muhimu sana. Sasa hivi *DAWASA* wanahitaji kama bilioni 200 na ngapi, bilioni 250 kwa ajili ya kumaliza uchakavu tutapata wapi hizo pesa?

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ili tutoe yale maji kutoka Rufiji tunahitaji zaidi ya trilioni moja tutapata wapi hizo pesa. Kwa hiyo, uwekezaji kwa maana ya kuvutia sekta binafsi kama Mheshimiwa Waziri alivyozungumza wakati fulani nilikuwa namfuatilia ni muhimu sana ili tuweze kufikia malengo ya kuwa na maji ya kujitosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza, ninaomba niishie hapo na ninaomba kuunga mkono wa hoja. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Massaburi.

**MHE. DOUGRAS D. MASSABURI:** Mheshimiwa Spika, nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema. Leo nimepata nafasi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kivule kuongea masuala yanahusu maji ndani ya Jimbo letu la Kivule.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mwanadiplomasia nguli, mara ya mwisho niliposema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, humu ndani ni mwanadiplomasia nguli, wako watu walibeza kauli zile kwenye vyombo vya habari, lakini leo wameuthibitishia umma na dunia, Tanzania na Bara la Afrika kwa kumteua aliyekuwa Katibu Mkuu wa Chama cha Upinzani kuwa kwanza si tu Mheshimiwa Mbunge, lakini pili Naibu Waziri wa Kazi

Ajira na Mahusiano. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan oyeee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ni kiongozi anaye kwenye siasa za kujenga, ni kiongozi anayeamini kwenye hoja mbadala; ni kiongozi aliyevuka mipaka ya kisiasa ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan sisi wananchi wa Jimbo la Kivule wakati anaingia madarakani, kwa takwimu za watu wa *SINOVET* mwaka 2008, Jimbo la Kivule lilikuwa na maji 0%, lakini leo miaka 15 baadaye Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amejenga tenki kubwa la maji la lita 9,000,000 pale pale Pugu Bangulo na maji yale yanatiririka kwenda kwenye Majimbo ya Segerea, Jimbo la Ukonga na Jimbo letu jipya la Kivule na hivyo kufanya Jimbo la Kivule kuwa na maji sasa 48%. Kati ya kata sita tayari kata tatu zimekwishapata maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, katika muktadha huo ninayo heshima kubwa kumshukuru kaka yangu Mheshimiwa Jumaa Aweso, mtoto wa Fatma Omari Masanga, mtoto wa mamalishe, anayefahamu nini shida ya maji, alikuja ndani ya Jimbo la Kivule, akakutana na mamalishe, babalishe, wauza mboga mboga akaahidi kuchimba visima 10. Kati ya mitaa 29 tayari visima vitatu vimekwishaanzachimbwa na viwili vimekwishaanza kutoa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Aweso na *management* yote kwa ujumla wake akiwemo dada yetu Katibu Mkuu, dada yetu Injinia Mwajuma. Pia nimpongeze sana kaka yangu Bwire na watu wote wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa namna ambavyo wamekuwa wakifanya kazi ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nijikite kwenye ushauri wakati ninamsikiliza ndugu yangu Mheshimiwa Aweso, jana aliishia na maneno mawili alisema anataka Taifa lenye uhakika wa maji na akasema nataka kuwe na wizara ya kuchochea uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nimwambie ninaunga mkono kazi kubwa anayoifanya, lakini namtaka ajifunge mkanda yeye na watu wote kwenye Wizara ya Maji inatupaswa tuwe na *total turn around* watu wote waliosimama kwenye Bunge hili Tukufu kila mmoja amezungumzia upotevu wa maji mahitaji ya maji Mkoa wa Dar es Salaam zaidi ya lita milioni 700,000.

Mheshimiwa Spika, mahitaji maji yanayotengenezwa ni zaidi ya lita 500,000,000 yanayopotea ni lita 250,000,000 ukiya-*quantify* ni zaidi ya shilingi 138,000,000,000. Fedha hizi tungeweza kuziokoa zingeweza kujenga vituo vya afya, zingeweza kujenga barabara za Kivule, zingeweza kuleta madawa na zingeweza kujenga mabwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali umetuambia kwamba 70% itokane na *alternative financing*. Nami ninaishauri Serikali yangu kama kuna mahali ambako Serikali na sekta binafsi wanaweza kuwa na *interest* ya kuwekeza wasisite kufanya hivyo. Unapowekeza kupitia sekta binafsi unaokoa kodi za Watanzania, unapookoa kodi za Watanzania unali-*allocate* pesa kwenda kwenye maeneo muhimu na mtambuka kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, hivyo niombe sana na nitashika shilingi siku ya mwisho kwenye bajeti yetu ya mwisho kwenye kitengo cha *PPP*. Tumekubaliana 70% itokane na sekta binafsi, lakini bado kitengo cha *PPP* hakijapewa *muscles* ya kutosha kwa maana ya bajeti tulioisikia kwenye Wizara ya Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niunge mkono hoja lakini nimtie moyo kaka yangu Mheshimiwa Jumaa Aweso kwa kazi kubwa anayoifanya. Mwenyezi Mungu ambariki, wananchi wa Kivule wanamshukuru na kumpongeza na kumkaribisha wakati wote katika mapambano ya kuwatafuta maji na kumtua mama ndoo ya maji kichwani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ninaomba niunge mkono hoja na ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, jiandae Mtoa Hoja.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaanza kwanza kwa kuunga mkono hoja Wizara na bajeti hii. Hongera sana kwa Waheshimiwa Wabunge kwa kuliheshimisha Bunge la Kumi na Tatu, Mkutano wa Tatu, michango yao mizuri ya kusisimua na inayojenga na hakika dhana ya kuishauri na kuisimamia Serikali wameionyesha kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumshukuru sana na kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniteua kwa mara ya pili kuwa Naibu Waziri wa Maji. Hii ni heshima kubwa kwangu binafsi kwa familia na wananchi wa Jimbo langu la Bariadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhamana nzito ninayoipokea kwa unyenyekevu na moyo wa kujituma kwa ajili ya Watanzania wote. Imani yake kwangu ni kubwa, nami ninaahidi kuilipa kwa vitendo vinavyoonekana na matokeo yenye tija kwa Taifa letu. Nitafanya kazi kwa bidii kwa uzalendo wa hali ya juu na kwa kuzingatia maadili na uwajibikaji na uadilifu katika utekelezaji wa majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, nikupongeze wewe kwa kutusimamia vizuri Bunge lako hili la Kumi na Tatu, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi, Makamu wa Rais kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kuteuliwa na kuanza kazi yake kwa kasi kubwa sana nimeshiriki ziara zake nimeona namna ambavyo anawatetea Watanzania. Nimeona namna ambavyo anasimamia haki itendeke, ninaona tumaini kubwa la Watanzania kupitia maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo yanatekelezwa na Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba.

Mheshimiwa Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wangu Jumaa Hamidu Aweso, huyu ni kiongozi, huyu ni kaka, huyu ni rafiki, huyu ni ndugu ambaye namna ambavyo anaijenga Wizara katika mshikamano na umoja inatufanya kutekeleza majukumu yetu kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, bila kusahau niwashukuru sana sana wananchi wa Jimbo la Bariadi walionipigia kura za kunifanya niwe mwakilishi wao. Ninafahamu kuna Madiwani wako hapa, kuna watendaji wa kata wako hapa, kuna Makatibu wangu wako hapa, lakini pia kuna vijana ambao wanatokana na vijiwe vya kahawa wamekuja kushuhudia mwakilishi wao nikisimama nao kutetea maslahi ya wananchi wa Bariadi na wananchi wa Tanzania nzima.

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba kazi hii kama ambavyo alisema Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, tunao wasaidizi wetu ambao wanatufanya tutekeleze majukumu yetu, ninatambua kwamba kazi zetu ni nzito. Hata hivyo, kwa upekee kabisa nimshukuru sana mke wangu Grace Kundo kwa kazi nzuri sana ya kunivumilia na kuhakikisha kwamba anaendelea kuwa sehemu ya mafanikio ambayo tunaendelea kuyapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua kazi kubwa ambayo imefanywa na Waheshimiwa Wabunge kwa siku ya leo mambo ya msingi ambayo leo nimeyasikia. Jambo la kwanza, ni kuhusiana na utekelezaji wa miradi viporo ambayo haijakamilika. Tumeyapokea kwa uzito stahiki maelekezo ya Wabunge na sisi tutaenda kuhakikisha kwamba tunasimamia.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, nimesikia kuhusu upotevu wa maji, hili ni jambo ambalo sisi kama Wizara tumejipanga. Tunayo mikakati, tumebainisha changamoto, tumebainisha vyanzo vya matatizo, lakini tumejipanga kuweka mikakati ya kwenda kupambana na upotevu wa maji.

Mheshimiwa Spika, lengo ni kwamba tusipate changamoto ya maji kupungua kwa wananchi wetu. Tunafahamu kwamba ukidhibiti upotevu wa maji ni njia mojawapo ya kuongeza

upatikanaji wa maji. Hilo tunaenda kulisimamia kuhakikisha kwamba linaweza kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Spika, pia, tumesikia suala la vitendea kazi. Waheshimiwa Wabunge tumelipokea tunayo maelekezo, lakini mpaka sasa *RUWASA* wameshapewa fedha kwa ajili ya kununua...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu muda wako umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa nafasi hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mtoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, asiyeshukuru watu hata Mungu hawezi kumshukuru. Kwa dhati ya moyo nikushukuru wewe binafsi hasa kwa uendeshaji wako wa Bunge na mageuzi makubwa ambayo umefanya katika Bunge letu, Mungu akubariki sana.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuniamini katika Wizara yetu hii ya Maji. Ninataka nimhakikishie mimi Jumaa Aweso ambaye nimepewa dhamana katika Wizara hii ya Maji sitokuwa kikwazo kwa Watanzania na kwa Waheshimiwa Wabunge kupata maji safi salama na yenye kutosheleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kumshukuru sana Makamu wa Rais, lakini kwa dhati ya moyo nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu tangu ameaminiwa kwa muda mfupi amefanya ziara katika maeneo mbalimbali katika sekta yetu ya maji, lakini amekutana na watendaji wote wa Wizara yetu ya Maji. Nini maana yake? Mheshimiwa Rais ameelekeza kwamba anapoondoka aache

tabasamu. Mtendaji Mkuu anasimamia kuhakikisha tabasamu inapatikana kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kwa dhati kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. Wametoa maoni, ushauri na mchango, sitaki nisimame hapa kujitetea. Maoni na ushauri ambao wameutoa sisi tunaupokea kwa ajili ya kwenda kuufanyia kazi na kwenda kuimarika zaidi katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuaminiwa kwa mara nyingine kuwa Waziri wa Maji, jambo la kwanza ambalo tumelifanya sisi kama Wizara ya Maji tumesema kwanza tufanye tathmini. Tumejitathmini kama Wizara, lakini tumefanya tathmini hasa juu ya watendaji wetu hasa katika taasisi zetu. Waheshimiwa Wabunge wamezungumza hapa juu ya suala la ukamilishaji wa miradi.

Mheshimiwa Spika, ukisoma katika hotuba yangu ya bajeti moja ya vipaumbele vyetu saba tulivyoviweka katika Wizara yetu ya Maji ni ukamilishaji wa miradi ambayo tumeianza. Ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tuna miradi 992 vijijini, tuna miradi 196 mijini, tuna miradi ya maji 26 ya maji taka mijini. Ninataka nikuhakikishie hii ndiyo vita tunayokwenda kupigana kuhakikisha miradi hii ambayo tulioianza tunakwenda kuikamilisha ili Watanzania wao mijini na vijini waweze kupata huduma maji safi na salama.

Mheshimiwa Spika, uongozi ni kuacha alama. Waheshimiwa Wabunge wamezungumza miaka yote kuhusu suala la maji. Ninataka niwaambie huwezi kujua unapokwenda kama hujui ulipotoka, tumetoka mbali. Nchi yetu ya Tanzania ina vijiji 12,333 mpaka 2006 tulikuwa kwenye vijiji 3,000. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliapa na akaja na kauli ya kumtua mwanamama ndoo kichwani na alihutubia katika Bunge hili, akasema mimi ni mama na asilimia kubwa wanaoteseka juu ya adha ya maji ni akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, akaenda mbali kunielekeza mimi Waziri wa Maji nikimzingua atanizingua. Ninataka niseme tumeanzisha

Wakala wa Maji Vijijini, leo tumefika vijiji 10,758, mama apewe maua yake.

Mheshimiwa Spika, ninataka niseme vijiji vilivyobakia katika nchi yetu ya Tanzania ni vijiji 1,575. Waheshimiwa Wabunge lazima tuingie katika historia. Moja ya kazi ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuisimamia Serikali. Ninaomba watusimamie sisi Wizara ya Maji katika kipindi hiki cha miaka mitano nikiwa kama Waziri wa Maji, ninaona nchi yote ya Tanzania na vijiji vyote vinakwenda kupata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi kama Wizara ya Maji tumeweka mikakati. Mkakati wa kwanza; ili tuhakikishe vijiji vyote vinafikiwa na huduma ya maji safi na salama tumesema tuwekeze kwa watendaji kwa maana ya rasilimali watu. Tunataka Mtendaji wa Wizara ya Maji aseme inawezekana. Tunataka mtendaji wa Wizara ya Maji awe ni mtu ambaye analeta matokeo. Hatutaki Mkurugenzi suti. Hatutaki mtendaji anayojua *AC* imeisha. Hatutaki mtendaji anayesema *Wi-Fi* imekwisha. Tunataka Mtendaji wa Wizara ya Maji asizoee shida za wananchi katika kuhakikisha watu wanapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo tulokubaliana kama watendaji wa Wizara ya Maji, *alternative financing*. Tunajua kabisa Wizara ya Maji, Mheshimiwa Rais anatupatia fedha, lakini lazima tujiongeze kwamba tuwe na *alternative financing*.

Mheshimiwa Spika, tumekwishaanza Tanga. Tuli-*aim* tupate shilingi 53,000,000,000, tumepata shilingi bilioni 54. Hayo ni mafanikio makubwa. Tunazielekeza mamlaka zingine ziige. Hili tumeanza na sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji hivi karibuni tutaanzisha *water infrastructure bond* ambayo itakwenda kutatua matatizo ya maji na kujenga miradi ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tumeona fursa ya Mheshimiwa Rais ya mahusiano ambayo ameyafanya kwa muda mfupi katika Wizara yetu na katika Taifa letu. Amenipa kibali nimekwenda Ufaransa. Nimekwenda Ufaransa, nimerudi

tumepata shilingi 220,000,000,000, tumesaini Morogoro. Morogoro wanakwenda kupata huduma ya maji safi na salama. Tumekwenda Korea kwa muda mfupi kwa kibali cha Mheshimiwa Rais. Tumekwenda tumerudi na fedha kwa ajili ya majitaka katikaJjiji la Dar es Salaam, kwa ajili ya majitaka kwa ajili ya Jiji la Dodoma, kwa ajili ya majitaka kwa Jiji la Iringa, kwa Mji wa Iringa. Hayo ndiyo mapinduzi ambayo anayafanya Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo tumelifanya tumeweka timu katika Wizara yetu, Wataalamu, kazi yao asubuhi… *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tusubiri. *Mic* yako haifanyi kazi?

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, katika jambo lingine ambalo tumeliona ni kwamba tutumie *private sector* kwa maana *involvement* ya *private sector*. Lazima tukubali *involvement* ya *private sector* siyo mpaka tajiri awe mzungu. Leo tunashuhudia kama mtu anaweza kununua *coaster* vijijini, anaweza kununua basi vijijini, anaweza kujenga mradi wa shilingi milioni 30 na watu wakapata huduma ya maji safi na salama. Sisi Wizara ya Maji jukumu letu ni kusimamia gharama na ubora.

Mheshimiwa Spika, tumeona leo Wizara ya Elimu pamoja ni jukumu la Serikali kutoa elimu, zipo shule za *private* zinatoa elimu. Tunaona kuna Wizara ya Afya jukumu lake ni kutoa afya, lakini vipo vituo vya afya vya *private,* watu wanapata huduma. Ninataka tuseme na sisi kwa nia moja lazima tulimalize tatizo la maji. Pia, wapo wadau mbalimbali kwa maana ya *NGOs* pamoja na wadau wengine wa benki, taasisi za dini, leo tunazialika kuhakikisha nguvu zetu tunazielekeza katika vijiji 1,575 ambavyo vimebaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka niwatie moyo Waheshimiwa Wabunge tumeweka huu mkakati wa vijiji 1,575 na tumeviwekea kauli. Wizara ya Maji inaitikia, 1,575 tupo *site* kikazi zaidi. Huo ndiyo uelekeo wa Wizara yetu ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeanza kuwatangazia wenzetu. Tumepata *Water for People* amekuja kwa muda mfupi ametupa zaidi ya shilingi bilioni 77 ameenda kufanya kazi pale Mpwapwa. Kwa hiyo, huo ndiyo uelekeo wetu wa Wizara ya Maji.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine Wizara ya Maji lazima tukubali kubadilika tutumie teknolojia kwa ajili ya mageuzi ya Wizara yetu ya Maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni zilipendwa leo kusikia mwananchi wa Tanzania anabambikiziwa bili za maji. Ni zilipendwa kusikia kwamba kuna upotevu wa maji. Teknolojia lazima zitumike. Yapo baadhi ya maeneo kisima kinachimbwa, lakini wananchi wanatumia maji chumvi, haiwezekani. Ipo mitambo ambayo tunaweza tukatumia kubadili maji chumvi na kuwa maji baridi ili Watanzania waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Huo ndiyo mwelekeo wa Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, Nchi yetu ya Tanzania si maskini wa vyanzo vya maji. Tuna Ziwa Victoria, tuna Ziwa Nyasa, tuna Ziwa Tanganyika, tuna Mto Ruvuma na Mto Pangani, uelekeo wetu tukatumie vyanzo toshelevu katika kuhakikisha tunatatua matatizo ya maji.

Mheshimiwa Spika, tunajua kabisa tunakwenda katika Dira 2050. Tunapokwenda katika Dira ya 2050 lazima tuwe na maji toshelevu. Tunakwenda kwenye kongani ya viwanda. Kilimo ambacho tunachotaka kulima tusitegemee kudra za Mwenyezi Mungu, tunataka kilimo cha umwagiliaji. Kwa hiyo, ili tuweze kuwa na kilimo cha umwagiliaji maana yake lazima tuwe na rasilimali toshelevu zitakazoweza kutumika.

Mheshimiwa Spika, niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge jambo lolote kubwa au maono yoyote makubwa unayotaka kuyafanya mara nyingi yanaanza na 'haiwezekani.' Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kiongozi ambaye mambo yaliyoshindikana leo yanawezekana.

Mheshimiwa Spika, miaka tangu 1954 lilizungumzwa Bwawa la Kidunda leo linatekelezwa. Miaka tangu ya 1973 lilizungumzwa Bwawa la Farkwa tukimaliza Bunge tunaenda kumkabidhi mkandarasi kwa ajili ya kuanza kazi. Tunapozungumza *National Grid* ya Taifa siyo kama tutaenda kufanya tumeshaanza kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nenda zako Kilimanjaro, tuna Mradi wa Same - Mwanga zaidi ya shilingi bilioni 400 umekamilika. Maelekezo ya Mheshimiwa Rais kwamba Mradi wa Same Mwanga ufike Korogwe. Ukifika Korogwe tuna Mradi wa zaidi ya shilingi bilioni 172 wa Miji 28. Uungane na maji ya Mradi wa Same Mwanga yaende Handeni, Korogwe, Muheza, yafike mpaka Chalinze kwa Mheshimiwa Ridhiwani yatakutana na maji ya *DAWASA* yataungana.

Mheshimiwa Spika, ukienda zako kule Ziwa Victoria maji yamefika Tabora. Malengo ya Mheshimiwa Rais maji yale sasa yafike hapa katika Jiji la Dodoma. ukienda Simiyu tuna mradi wa zaidi ya shilingi 440,000,000,000 tunayatoa maji ya Ziwa Victoria kwa ajili ya kuyaunganisha wilaya zote katika Mkoa wetu wa Simiyu. Huo ndiyo uelekeo wa Wizara yetu ya Maji na huo ndiyo uelekeo wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan hapatikani kila mahali. Tumempata lazima tumtumie kwa maslahi ya Watanzania na sisi tuweze kukumbukwa katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba kutoa hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kaeni. Mnakaa sana humu. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kifungu 1001 - *Administration and Human Resource Management*......................Sh.3,564,205,000

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa kifungu hichi kina mshahara wa Waziri na nina majina hapa manne. Tunaanza na Mheshimiwa Abdallah Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Sikusudii kushika mshahara Waziri kwa sababu ninafahamu utendaji wake wa kazi. Sina mashaka na utendaji wa Naibu Waziri, sina mashaka na utendaji wa Katibu Mkuu *Engineer* Mwajuma Waziri, lakini lengo langu ni kutaka kupata *commitment* ya Serikali juu ya utekelezaji wa Mradi wa Miji 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma kitabu cha Waziri ukurasa wa 68, utaona kuna utofauti wa utekelezaji wa miradi hii. Miji 24 kasi yake ya utekelezaji imekwenda vizuri. Miji minne bado ipo utekelezaji wake ni wa kiwango cha chini sana. Mradi wa

Makonde 24%, Mradi wa Mafinga 16.5%, Mradi wa Rorya Tarime 15.6% na Mradi wa Songea asilimia sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii tunaita kwa pamoja Miji 28. Ninataka nipate *commitment* ya Serikali kwamba miji hii minne ambayo utekelezaji wake upo chini itapewa fedha haraka na wakandarasi kwa sababu wameshatoka *site*, hawapo *site* ili warudi *site* ili na miji hii minne miradi yake ikamilike kama ile miji 24 ambayo utekelezaji wake unakwenda vizuri. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kwamba *issue* iliyokuja hapa ni juu ya suala la Miji 28.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Miji 28 ni miradi ambayo inatekelezwa baina ya Serikali ya Tanzania pamoja na Serikali ya India. Historia yake ilitakiwa ijengwe miradi 17. Tulipata ufadhili wa dola 500,000,000 tukasema hapana lazima tuipitie. Tunaweza tukapata miradi mingi. Baada ya kuipitia, tukapata miradi 24. Tukamwambia Mheshimiwa Rais kwa kuwa sisi tuna malengo ya kuhakikisha hii miji tunaikamilisha ili watu wapate huduma ya maji safi na salama, akasema ongezeni miji minne. Kwa hiyo, tukawa na miji 28. Tuna hii miji 24 ya ufadhili lakini miji hii minne inafanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Makonde ni Mradi ambao unagharimu zaidi ya shilingi 80,000,000,000. Ninataka nimhakikishie hivi karibuni tulikuwa na kikao kwa ajili ya malipo ya wakandarasi ambapo Kamati ya uongozi ilikaa pamoja na baadhi ya Wizara za kisekta. Maelekezo ya Kibunge yalitolewa kwamba fedha zianze kutolewa na Wizara ya Fedha imeji-*commit*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nilithibitishie Bunge lako, tulipokea shilingi 40,000,000,000 kwa mara ya kwanza, sasa hivi tumepokea shilingi 29,000,000,000. Maeneo ya miradi hii minne

ambayo inatakiwa kulipwa imo. Tunaenda kulipa na kazi itaendelea kama kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Abbas Tarimba.

**MHE. TARIMBA G. ABBAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Nimesimama kuhusiana na suala la uhaba wa maji katika Jiji la Dar es Salaam. Mheshimiwa Waziri wakati akitoa hotuba yake alieleza kwamba hali ya upatikanaji wa maji na hasa uzalishaji haukidhi, kwa maana maji yanayozalishwa sasa hivi ni lita milioni 550 hivi na hata hayo yanayozalishwa hayafiki Dar es Salaam yote kwa sababu ya upotevu wa maji. Akasema dawa ni kuwa na Bwawa la Kidunda limalizwe kwa haraka ili maji yajazwe na Mto wa Ruvu uweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimesimama kumtaka na kumwomba Mheshimiwa Waziri atupatie *commitment* juu ya upatikanaji wa fedha, kwamba fedha zitaenda kutolewa kila *certificate* inapokuwa *raised* ili ikifika mwezi wa Disemba bwawa lile liwe limekamilika na watu wa Dar es Salaam tuweze kupata afueni. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Tunapozungumzia Bwawa la Kidunda ni ndoto ambayo iliotwa tangu mwaka 1954. Aliyefanya maamuzi ya kuhakikisha bwawa hili linajengwa ni Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mradi ulichelewa kwa muda mrefu kwa sababu tulitaka ufadhili. Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ninanukuu maneno yake alisema:

"Tunapotaka kutatua matatizo ya watu hatuwezi kuangalia gharama. Mradi huu tutajenga kwa fedha za ndani." Amefanya uthubutu huo shilingi 329,000,000,000 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kuujenga mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulivyopata *crisis* ya maji Jiji la Dar es Salaam Mheshimiwa Rais alimtuma Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Lameck Nchemba alifika mpaka katika Bwawa la Kidunda na tulivyofika pale mkandarasi alikuwa anadai shilingi 24,000,000,000. Maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, shilingi 24,000,000,000, zile zipatikane ndani ya wiki. Zimepatikana ndani ya wiki na tumekwisha mlipa. Ameielekeza Wizara ya Fedha ikae na Wizara ya Maji pamoja na mkandarasi uwekwe utaratibu kila mwezi ili kuhakikisha fedha zinatolewa ili mradi ule usikukwame. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge hivi ninavyozungumza katika hizo shilingi bilioni 29 ambazo nimezizungumza hapa, tulipata 40 hizi 29, shilingi bilioni 12 tunamlipa tena Mkandarasi wa Bwawa la Kidunda. Ninataka nikuhakikishie pia katika ujenzi wa bwawa kuna *civil structure* lakini pia kuna kazi zingine. Katika Bwawa la Kidunda ni mradi ambao una *component* nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kuna *component* ya umeme, kuna *component* ya barabara, pia kuna *component* ya ujenzi wa ofisi. Sisi tunaliangalia kwanza bwawa, ofisi inaweza ikasubiri. Kwa hiyo, katika *civil structure* zipo 70%, kwa hiyo, hakuna kitu kitakachotuzuia. Tumemwambia mkandarasi mwisho wa mwaka huu tunataka maji sasa yaingie katika hilo bwawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Abubakari Asenga.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi hii. Nimesimama kutokana na hali ya mafuriko katika nchi yetu maeneo mbalimbali, hasa maeneo yale ambayo yanapata mafuriko kwa sababu Mamlaka za Mabonde yetu kutokuwa na uwezo wa kutosha wa kufukua baadhi ya mito ambayo imeziba na watu waliochepusha maji na kuboresha matuta ili kupunguza adha ya mafuriko kwenda kwa

wananchi. Kwa mfano, Kilosa, Mvomero na kule Kilombero tuna Mamlaka ya Bonde la Wami, Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kupata *commitment* ya Serikali, namna gani Wizara itaziwezesha Mamlaka za Mabonde ili kufukua mito hiyo na kupunguza adha ya mafuriko kwa mfano Mto wa Lumemo pale Ifakara? Lakini sina nia ya kushika shilingi. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni nilielekeza Wizara yetu ya Maji, Wiki ya Maji tuifanyie Morogoro na tuliamua makusudi tuifanyie Morogoro. Kuna maamuzi kama Wizara na uelekeo ambao tumeuweka ili tuweze kutatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia Mkoa wa Morogoro wakati mwingine mvua inaweza isinyeshe Morogoro lakini unakutana na mafuriko. Nini maana yake? Morogoro inakuwa kama bakuli. Mvua zinazotoka Mkoa wa Manyara na maeneo mengine yanakwenda Morogoro na yanaleta athari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Wizara moja ya maelekezo ambayo tumeyatoa na uelekeo wetu na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, mvua isiwe maafa, mvua iwe fursa kwa Wizara yetu ya maji. Kwa hiyo, mkakati wetu Wizara ya Maji kwa kushirikiana na sekta nyingine mtambuka, mkakati wetu ni kujenga mabwawa ya kimkakati, tuweze kuyavuna maji haya ili kuokoa mafuriko katika Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine amezungumza katika eneo lake la Ifakara, wamepata hiyo athari nielekeze timu ya Wizara kesho itafika pale na tutakuwa na vifaa kwa ajili ya kuyachepusha yale maji ili kunusuru mafuriko kwa wananchi wa Ifakara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na niseme kwamba sina dhamira ya kushika shilingi ya Mheshimiwa Waziri hasa kwa majibu mazuri aliyoyatoa na namna alivyojipambanua. Hata hivyo, ninataka nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri juu ya miradi ambayo Serikali imepeleka fedha nyingi, miradi imekamilika nchini, lakini kunakuwa kidogo kuna kusuasua kwa miradi ile katika utoaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitoa mfano hapa wakati ninachangia; kwamba mfano wa mradi ambao upo ni Mradi wa Nyihara, Serikali imegharamia zaidi ya shilingi bilioni moja. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kutoa fedha ile lakini unashindwa kutoa maji kwa mwaka wa tatu kwa sababu ya ukosefu wa shilingi milioni 20 peke yake ya kununua *transformer*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii Mheshimiwa Waziri mingi tunajipambanua kwamba imekamilika na kweli tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, lakini vitu vidogo sana vinatutia doa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nipate kauli tu ya Serikali kuhusiana na miradi aina hii pamoja na mradi huu. Nini kauli ya Serikali na namna ilivyojipanga kuhakikisha kwamba jambo hili linaondokana kabisa na miradi ile inaendelea kutoa maji kama kusudio lilivyokuwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kaka yangu Mheshimiwa Jafari, lakini kubwa ambalo ninataka nimweleze sisi tulivyopokea Wizara hii ya Maji, jambo la kwanza tuliainisha miradi chechefu ambayo maelekezo ya Mheshimiwa Rais ilikuwa 177, ikiwemo kuna Mradi unaitwa Komuge katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie kwamba miradi ile 177 tumeikamilisha, lakini kubwa ambalo sasa hivi tunakwenda nalo katika uendelezaji ni kuhakikisha kwamba maji

yanakuwa endelevu, tumeweka jumuiya za watumiaji maji na hapa ninaomba nieleze. Jumuiya za watumiaji maji zinakusanya fedha wakati mwingine mtu hapati maji kwa sababu eti LUKU ya umeme imekwisha, haiwezekani. Tumesema wakusanye fedha wapeleke benki, wanajua muda wa umeme unapokwisha, watumie maandiko watume fedha ili watu waweze kupata huduma ya maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza hapa mradi hautoi maji kwa sababu ya shilingi 20,000,000. Ninataka nimwelekeze Mheshimiwa Katibu Mkuu alisimamie na shilingi 20,000,000 zitoke haraka wananchi wale waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Katibu, *guillotine*.

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*………….Sh.1,217,858,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Unit*....................Sh.8,466,553,536
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*......Sh.513,911,000
Kifungu 1005 - *Legal Services Unit*................................Sh.512,691,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*.........Sh. 790,331,000
Kifungu 1007 - *Management Information System Unit*..........................................................Sh.523,585,000
Kifungu 1008 - *Internal Audit Unit*.................................Sh.664,481,000
Kifungu 1009 - *Project Preparation, Coordination and Environmental Management Unit*........Sh.586,475,000
Kifungu 1011 - *Monitoring and Evaluation Unit*...........Sh.572,058,000
Kifungu 1012 – *Environmental Management*..............Sh.465,499,000
Kifungu 2001 - *Water Resources*..............................Sh.12,656,471,000
Kifungu 2003 - *Water Laboratory*..............................Sh.3,544,952,000

Kifungu 3001 - *Water Supply and Sanitation Divisiyon*............................................Sh. 46,572,973,464
Kifungu 5001 - *Water Development and Management Institute*..........................................Sh. 0

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 49 – Wizara ya Maji**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*.......................Sh.801,700,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*................Sh.227,345,749,000
Kifungu 2001 – *Water Resources*..............................Sh.27,183,347,955
Kifungu 2003 – *Water Laboratory*..............................Sh.1,713,105,000
Kifungu 3001 – *Water Supply and Sanitation*

*Divisiyon*............................................Sh.782,498,668,045

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN, *ndc* – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Mtoa hoja. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni 126(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Agosti, 2025, ninaomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake. Ninaomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Sasa nitawahoji kuhusiana na Hoja ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Walioafiki wameshinda.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji kwanza nichukue nafasi kukupongeza wewe na timu yako kwa kweli mnafanya kazi vizuri sana. Mnazo changamoto lakini kwenye changamoto ndiyo kwenye njia hapo hapo. Kwa hiyo, hongereni sana wewe na timu yako nzima ya maji, endeleeni kuhudumia. *(Makofi)*

Bwawa hili la Kidunda lilianza *project* yake 2002. Kipindi hicho mimi nilikuwa Naibu Meya wa Manispaa ya Ilala na baadaye wafadhili wa *MCC* wakautoa huu mradi, lakini ukakwama mpaka alivyoingia Mheshimiwa Rais Samia ndiyo ameurudisha tena huu mradi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, upo umuhimu, ninaona kuna mjumbe alizungumza kuwa tunapoteza maji kwa siku lita siyo chini ya 600,000,000 ambayo yanakwenda moja kwa moja Bahari ya Hindi kutoka mito

yetu mbalimbali. Kwa hiyo, mradi huu ukikamilika utahakikisha maji yanapatikana katika maeneo mengi sana. Kwa hiyo, nikupongeze sana, lakini ninawapongeza Wabunge kwa kazi nzuri waliyoifanya na kwa kweli umeiheshimisha Wizara hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninaahirisha Shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.46 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 7 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*